*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA SABA

### Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 22 Aprili, 2022

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu!

**NDG. ATHUMAN HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri. Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge, Katibu!

**NDG. ATHUMAN HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali tutaanza na Ofisi ya Rais TAMISEMI. Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 87

**Kuiongezea *TARURA* Uwezo wa Kifedha**

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaiongezea *TARURA* fedha ili iweze kuzihudumia barabara za Wilaya ya Kyerwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anatropia Lwehikira Theonest, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kyerwa ni Wilaya ambayo kwa jiografia ina milima, miteremko pamoja baadhi ya barabara kupita katika maeneo yenye ardhi oevu. Serikali imekuwa ikitenga fedha kila mwaka kwa ajili ya matengenezo ya barabara na madaraja.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeongeza bajeti ya kuboresha miundombinu ya barabara katika Wilaya ya Kyerwa kutoka Shilingi bilioni 1.39 katika mwaka wa fedha 2020/2021 hadi Shilingi bilioni 2.89. Ongezeko hili linatokana na Serikali kuongeza vyanzo vingine ambavyo ni tozo ya

mafuta Shilingi bilioni 1.00, Mfuko Mkuu wa Serikali Shilingi milioni 500.00 na Mfuko wa Barabara Shilingi bilioni 1.39.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuongeza wigo wa matengenezo ya barabara pamoja na kufungua barabara mpya katika Wilaya ya Kyerwa kadri ya upatikanaji wa fedha. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Anatropia Theonest, swali la nyongeza.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Jiografia ya Jimbo la Kyerwa ni milima na mabonde, hivyo kuhitaji madaraja na barabara kwa maana maeneo mengi hayapitiki. Bajeti ya bilioni mbili haitoshi, nataka kujua *commitment* ya Serikali ni kwa kiwango gani itaongeza bajeti ili kuweza kusababisha maeneo mengi yafikike?

Mheshimiwa Spika, swali la pili barabara ya Nkwenda-Kakanza-Kimuli mpaka Mabira inatumika na kata zaidi ya 5 na kwa *TARURA* wamepewa *scope* ya kilometa tatu ambayo ina urefu wa zaidi ya kilometa 30. Je, ni sahihi kweli kutoa kiwango hiki cha fedha kwa barabara hii nataka kujua mkakati wa dharura kupeleka fedha?

**SPIKA:** Umeshauliza swali Mheshimiwa. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Anatropia Lwehikira Theonest, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Anatropia kwa namna ambavyo anashirikiana na Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Kyerwa Mheshimiwa Innocent Bilakwate na hoja hizi zote ambazo Mheshimiwa Mbunge amezileta Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo

amekuwa mara kwa mara anazileta, kwa hiyo niwapongeze kwa ushirikiano huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na fedha kwa maana za madaraja, hali ya milima na mabonde na hali ya mvua tunafahamu na ndio maana Serikali imeendelea kuongeza fedha kutoka bilioni moja mpaka bilioni mbili na milioni mia nane na tisini katika Wilaya ya Kyerwa ili kuhakikisha inaendelea kujenga madaraja, makalveti na barabara. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Serikali itaendelea kuweka jitihada hizo.

Mheshimiwa Spika, hii barabara ambayo inahudumia kata nyingi na inahitaji fedha zaidi ndio maana Serikali imeongeza bajeti na tutaendelea kuongeza bajeti ili tuhakikishe tunafikia kilometa zote 30 ili kata zote ziweze kunufaika. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Juliana Shonza, swali la nyongeza.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Barabara za Wilaya ya Ileje zinakabiliwa na changamoto kubwa sana ya kutopitika hasa wakati wa masika. Naomba kufahamu ni lini Serikali itaipatia fedha *TARURA* Wilaya ya Ileje ili kuwaondolea adha wananchi wa Wilaya ya Ileje? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Juliana Shonza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka huu wa fedha, moja ya halmashauri ambazo zimeongezewa bajeti ili kuweza kukidhi matengenezo ya barabara za vijijini na mijini

ni Halmashauri ya Wilaya ya Ileje. Hivyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, hiyo barabara ambayo ameitaja ni sehemu ya bajeti ya mwaka ujao wa fedha na tutahakikisha kwamba tunaendelea kuitengeneza kwa awamu ili iweze kupitika vizuri. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, swali la nyongeza.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na Serikali kuongeza bajeti kwa Wilaya ya Kyerwa, lakini tulileta ombi maalum kwa ajili ya barabara ya Kibingo kwenda Rwesinga, Barabara ya Mabira kwenda Nyamiri-Makamuri, barabara ya Kikukuru -Mkunyu - Lwele, barabara ya Kakanya - Lwele pamoja Bushongore. Ombi hili ni lini litatekelezwa ili kuondoa changamoto iliyopo Kyerwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, Mbunge wa Jimbo la Kyerwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Bilakwate kwa namna ambavyo anaendelea kuwapambania wananchi wa Jimbo la Kyerwa.

Mheshimiwa Spika, pia nimhakikishie ni kweli ameleta maombi maalum ya barabara zenye urefu wa takribani kilomita 55 ambazo amezitaja. Tayari Ofisi ya Rais, TAMISEMI tumepokea na tutaanza utekelezaji mwaka ujao wa fedha kuhakikisha barabara zote zinapitika vizuri. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Mkundi, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Je, ni kwa nini Serikali isipeleke pesa za miradi hii ya *TARURA* kwa meneja wa wilaya badala ya mkoa ambako mara nyingi zimekuwa zinasababisha urasimu kwenye utekelezaji wa miradi hii ya barabara zilizo chini ya *TARURA?*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)**: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba fedha za matengenezo ya barabara zimekuwa zikipelekwa katika ngazi ya mikoa na siyo ngazi ya Mameneja wa Wilaya na sababu ya msingi ilikuwa muundo wa *TARURA* uliweka watendaji wengi zaidi kwenye ngazi ya mkoa kwa maana ya wataalam; Wahasibu, wataalam wa manunuzi na wengine. Kwa hiyo ilikuwa ni vyema sana kupeleka fedha kwenye ngazi ya mkoa ambayo ina watendaji wengi kuliko halmashauri. Utaratibu huu tunaendelea kuutekeleza, lakini pale tutakapoona tuna sababu ya kupitia upya tutafanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sebastian Kapufi, swali la nyongeza.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Barabara ya Katesi - Iteka inaunganishwa na daraja muhimu katika Mto Mpanda, kwa bahati mbaya daraja hilo limekatika. Je, ni lini Serikali itaongezea fedha *TARURA* ili walitengeneze daraja hilo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)**: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sebastian Kapufi, Mbunge wa Jimbo la Mpanda Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka ujao wa fedha Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda pia ni moja ya halmashauri ambazo zimeongezewa bajeti ya barabara. Lakini nimhakikishie kwamba mpango wa Serikali ni kuainisha na tayari nimeshainisha madaraja korofi yote na makalvati ili kuhakikisha tunaongeza fedha za ujenzi wa madaraja hayo yaweze kupitika. Hivyo nawaelekeza *TARURA,* Mkoa wa Katavi na Manispaa ya Mpanda wahakikishe wanaleta andiko la daraja hili ili TAMISEMI tuweze kuona namna ya kutafuta fedha kwenda kufanya ujenzi wa daraja hilo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Twaha Mpembenwe, swali la nyongeza.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Wilaya ya Kibiti tumepatiwa fedha shilingi bilioni 6.2, tumejenga daraja zuri sana pale Mbochi ambalo linaunganisha wananchi wa Mbwela na Mbochi na kuja Kibiti Mjini. Hata hivyo, kuna kipande cha kilometa 35 ambacho ikinyesha mvua kinakuwa kipo katika hali mbaya sana.

Je, ni nini tamko la Serikali ili kuweza kuhakikisha kwamba tunakwenda kutengeneza kipande kilichobaki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Twaha Mpembenwe, Mbunge wa Jimbo la Kibiti, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge na tuendelee kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu mama Samia Suluhu Hassan kwa fedha nyingi sana ambazo amezileta katika majimbo yetu ikiwepo Jimbo la Kibiti. Nimhakikishie kipande cha kilomita tatu ni kipaumbele kwa sababu kama tumepeleka billions za fedha katika daraja lazima tukamilishe kilomita tatu ili hilo daraja liweze kuwa na tija. Kwa hiyo namhakikishia kwamba tutatafuta fedha kuhakikisha kilomita hizi tatu zinatengenezwa ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipatia fursa hii ya kuuliza swali la nyongeza. Mazingira ya Kyerwa na Muleba yanafanana kutokana na mvua nyingi, milima na mabonde. Tuna barabara nyingi ambazo hazipitiki hasa kipindi cha mvua. Tulileta ombi letu kwa ajili ya barabara ya Kimea Burigi na Luhanga- Kiholele. Je, ni lini Serikali itatupatia pesa kwa ajili ya kutengeneza hizo barabara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Oscar Kikoyo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba jimbo hili pia lina changamoto ya milima, mabonde na linahitaji kupata fedha za kutosha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizi na ni kweli kwamba Mheshimiwa Mbunge alileta ombi maalum. Nimhakikishie kwamba maombi maalum yote yaliyoletwa yanafanyiwa tathmini na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kupitia *TARURA* na tutahakikisha yanatafutiwa fedha ili yaweze kufanyiwa kazi. Kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge nimhakikishie kwamba tutalipa kipaumbele pia eneo ambalo wameomba maombi maalum. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na swali lingine Mheshimiwa Musukuma Joseph Kasheku Mbunge wa Geita swali lake litaulizwa; sasa hapa nakuona umesimama Mheshimiwa Nyongo, lakini ujumbe niliyopata ni kwamba anauliza Mheshimiwa Getere. Sasa sijui kati yenu nani ana majibu ya Mheshimiwa Musukuma. Kati yenu wawili nani ana majibu?

**MHE. STANLAUS NYONGO:** Mheshimiwa Spika, wote hatuna majibu, tunategemea kuyasikiliza.

**SPIKA:** Wote hamna majibu saw abasi nilimwona Mheshimiwa Getere kwanza kabla yako.

**MHE. STANLAUS NYONGO:** Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere kwa niaba ya Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma.

Na. 88

**Serikali Kurudisha Hekta 8,000 Zilizopo Kwenye Pori la Rwande Katika Jimbo la Geita Vijijini**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE K.n.y. MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itarudisha hekta elfu nane zilizopo kwenye Pori la Ruande Jimbo la Geita kwani pori hilo limepoteza sifa ya kuwa Hifadhi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali

la Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, Mbunge wa Geita Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Msitu wa Hifadhi Ruande ulianzishwa kwa GN Na.106 ya mwaka 1956 una ukubwa wa Hekta 15,550. Msitu huu unaosimamiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Geita umekuwa ukivamiwa kwa shughuli za kilimo na ufugaji unaofanywa na wananchi wa vijiji 13 vinavyouzunguka.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilipokea maombi kutoka katika Vijiji viwili (2) vya Kagu na Kakubilo ya kumegewa sehemu ya hifadhi hiyo kwa shughuli za kilimo. Serikali inayafanyia tathmini maombi hayo kupitia Kamati ya Mawaziri Nane wa Kisekta inayoshughulikia migogoro ya vijiji 975 nchini kote na itatoa maamuzi muafaka kwa kuzingatia maslahi ya pande zote.

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Getere, swali la nyongeza

**MHE. BONIPHACE M. GETERERE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, nina swali moja tu la nyongeza. Kwa kuwa kumekuwepo na maeneo mengi hapa nchini yaliyokosa sifa ya kuwa hifadhi na yamekuwa na migogoro mikubwa sana na wananchi. Ni lini Serikali sasa itafanya tathmini ya maeneo yote haya na kuyaleta hapa ili tuyagawe kwa wananchi, yote yaliyokosa sifa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tumekuwa na maeneo mengi ambayo yamekuwa hifadhi kwa muda mrefu,

lakini baadhi ya maeneo yamekuwa na changamoto ya migogoro kati ya wananchi pia na mamlaka za hifadhi.

Nimhakikishie kwamba Serikali inatambua changamoto katika maeneo hayo na tathmini inafanyika kwa kuzingatia sheria, taratibu na miongozo ya maeneo ya hifadhi ili kuhakikisha yale ambayo yanaendelea kukidhi sifa za kuwa maeneo ya hifadhi yaendelee kuwa maeneo ya hifadhi lakini yale ambayo yamepoteza sifa, Serikali inachukua hatua za kuendelea kuwapatia wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba jambo hili tunalifanyia kazi ikiwemo la msitu huu ambao tumeujibia. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, swali la nyongeza.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Napenda kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba kwa mfano sisi pale katika Mkoa wa Simiyu tuna Pori la Maswa na ni pori kubwa na ni maarufu. Je, Serikali ina mkakati gani wa kutangaza mapori haya kimataifa ili yaweze kutumika kwa maana ya kukaribisha watalii, vilevile kuhakikisha kwamba wananchi wa maeneo haya wananeemeka na mapori haya?

**SPIKA:** Mheshimiwa ni swali la nyongeza, kwa hiyo linaweza kuwa moja tu, hapo umeunganisha mawili.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa najaribu kutengeneza hoja, basi Serikali ina mkakati gani? N naomba atueleze?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la

nyongeza la Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, Mbunge wa Jimbo la Maswa Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli katika Halmashauri ya Maswa na Mkoa wa Simiyu kuna Pori maarufu la Maswa na kwamba Serikali imekuwa na mkakati wa kuhakikisha kwamba inatangaza mapori haya ili watalii waendelee kuja na Serikali yetu iendelee kupata mapato. Ndio maana hivi sasa tunaongea Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan anaendelea kuitangaza *Royal Tour* ili tuhakikishe watalii zaidi wanaendelea kuongezeka katika hifadhi zetu lakini maeneo ya kitalii ikiwepo Pori la Maswa. Kwa hiyo nimhakikishie kwamba mpango wa Serikali ni huo na utahakikisha kwamba wananchi wanaoishi maeneo ya jirani pia wananufaika na mpango huo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaelekea Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 89

**Kutatua Changamoto Zinazokabili Miradi ya Umwagiliaji Mkoga na Kitwiru – Iringa**

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka fedha kutatua changamoto zinazokabili Miradi ya Umwagiliaji ya Mkoga na Kitwiru iliyopo Manispaa ya Iringa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Mavunde majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Miradi ya umwagiliaji ya Cherehani Mkoga yenye hekta 750 na Kitwiru yenye hekta 100 iliyopo katika Manispaa ya Iringa inakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo uchakavu wa miundombinu ya umwagiliaji iliyojengwa muda mrefu; kutokamilika kwa miundombinu, pamoja na miundombinu kuharibiwa na mafuriko.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Umwagiliaji inaendelea kutafuta fedha kutoka kwa wadau wa maendeleo kwa ajili ya kukamilisha miradi ya umwagiliaji mbalimbali ikiwemo miradi ya Mkoga na Kitwiru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali madogo mawili. Kwanza nashukuru kwa majibu ya Serikali. Kilimo cha uhakika ni kilimo cha umwagiliaji. Napenda kufahamu hatua iliyofikiwa kwa utekelezaji wa miradi ya Mgombilenga iliyopo Kata ya Kitwiru na Mradi wa *UNI* wa Kata ya Nyanzwa, kwa sababu hii miradi, Wabunge wa Iringa ni muda mrefu sana tumekuwa tukiifuatilia.

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, katika Wilaya ya Mufindi Kaskazini tuna skimu ya Igoma, Kata ya Sadani na Ikwea. Hii miradi kwa mfano hii ya Ikweha ililetewa shilingi milioni 800, lakini utekelezaji wake mpaka sasa hivi bado haujaweza kueleweka. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atujibu, Mkoa wetu wa Iringa ni wa kilimo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu miradi ya Mgombilenga na Nyanzwa iliyopo Wilaya ya Kilolo, katika bajeti ya mwaka 2022/2023 Serikali itakwenda kuikabarati miradi hii na kuitekeleza. Hivyo nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye swali la pili la mradi wa Ikweha, ni kweli pale tuna mradi ambao mpaka hivi sasa umeshatumia shilingi milioni 800 ambazo zimetokana na fedha za *DADPs* pamoja na *DIDF.* Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tunafahamu changamoto iliyoko pale, hivi sasa Serikali tunatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa bwawa. Vile vile mimi mwenyewe nitakwenda kutembelea mradi huu ili kutatua baadhi ya changamoto zilizopo pale na kuwafanya wakulima wawe na amani na kufanya kilimo cha umwangiliaji katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namwahidi tu Mheshimiwa Mbunge, kama Serikali, tunafahamu changamoto iliyopo pale na tunatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa bwawa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Grace Tendega, swali la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Spika, Mradi wa Umwagiliaji wa Izazi uliyopo Jimbo la Isimani una changamoto ya uchakavu wa miundombinu pia. Ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya kukarabati miundombinu hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Grace Tendega, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mirada yote ya umwagiliaji tuliyonayo hapa nchini hivi sasa tumeweka mpango mkakati katika mwaka wa fedha ujao kuhakikisha kwamba Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, inaipitia miradi yote nchini Tanzania, tufanye uhakiki, tujue miradi gani inafanya kazi, ipi haifanyi kazi na ipi inahitaji marekebisho ya kiwango gani?

Mheshimiwa Spika, katika uhakiki huo pia tutagusa na miradi ambayo Mheshimiwa Mbunge ameitaja.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Almas Maige, swali la nyongeza.

**MHE. ALMAS MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Sisi tuna mradi wa Skimu ya Shitage, iligharimu fedha nyingi sana, haifanyi kazi. Lini ahadi ya Mheshimiwa Waziri ya kutengenezwa hiyo skimu itatekelezwa ili wananchi wapate faida ya mradi ule?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Almas Maige, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema pale awali, tunafahamu kwamba kilimo cha umwagiliaji ndicho kilimo hasa ambacho kitamkumboa mkulima wa Tanzania. Kwa umuhimu huo, tumeamua kwa dhati kabisa kuipitia hii miradi yote ikiwemo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameisema. Nimwondoe hofu ya kwamba tumejipanga kuhakikisha miradi hii inafanya kazi.

Kwa hiyo, katika eneo lake pia tutapita na hivi sasa tunaendelea kutafuta fedha na mtaona kwenye bajeti yetu inayokuja, nguvu kubwa hivi sasa imewekwa kwenye Tume ya Umwagiliaji kuwawezesha ili tuweze kufanya kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Charles Kajege, swali la nyongeza.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Jimbo la Mwibara ni kama limezungukwa na maji, lakini hatuna hata mradi mmoja wa umwagiliaji maji: Je, ni lini Serikali itajenga miradi hiyo katika Kata ya Namuhula, Igundu, Iramba na Kasuguti? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Charles Kajege, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ni jambo ambalo ameliwasilisha hapa, nami nitaelekeza wataalam wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji wakalitembelee eneo hilo na baada ya hapo waone namna ya kuwasaidia wananchi katika eneo hilo kufanya kilimo cha umwagiliaji.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Justin Nyamoga, swali la nyongeza.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Pale Ruaha Mbuyuni kuna mradi wa umwagiliaji ulikarabatiwa na Wizara kwa *force account*, lakini sasa mto ule umeanza kuchepuka tena: Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari tuongozane ili tuweze kuangalia tunafanyaje katika kuukarabati?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Justin Nyamoga, Mbunge wa Kilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, namwahidi tu kwamba Mheshimiwa Mbunge, kabla mimi na yeye hatujaongozana Jumatatu, Afisa wetu wa Tume ya Umwagiliaji walioko pale Iringa atakwenda kuukagua kwanza na kutupa taarifa, nami na yeye pia tutakwenda pamoja.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, swali la nyongeza.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Jimbo la Tunduru Kusini kuna miradi miwili ambayo ilifanyiwa kazi na imechukua hela nyingi zaidi ya shilingi bilioni tatu kutengenezwa pamoja na barabara, lakini miradi ile haifanyi kazi. Je, Serikali inampango gani wa kuweza kukamilisha miradi ile, mradi wa Mishaji pamoja na mradi wa Madaba, uliopo Azimio?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Daimu Mpakate, Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika majibu yangu ya awali, tumejipanga kuhakikisha miradi yote hii inafanya kazi. Hivyo, nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge ya kwamba katika uhakiki ambao tutaufanya, tutapitia pamoja na maeneo yake ili kuona miradi hii changamoto yake ni nini; na mwisho wa siku tuweze kuikwamua na wananchi waweze kufanya kilimo cha umwagiliaji.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini.

Na. 90

**Serikali Kupunguza Bei za Mbolea**

**MHE. ORAN M. NJEZA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kupunguza bei za mbolea zinazopanda kwa kasi kwenye Soko la Dunia ili kumpunguzia mkulima mzigo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika msimu wa 2021/2022 bei ya mbolea imeendelea kupanda katika Soko la Dunia kutokana na athari za UVIKO-19 na Vita ya Urusi na Ukraine zilizosababisha kupungua kwa uzalishaji na ongezeko la gharama za malighafi zinazotumika kutengeneza mbolea.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo, Serikali imeanza kuchukuliwa hatua za haraka, muda wa kati na muda mrefu katika kukabiliana na changamoto ya kupanda kwa bei. Hatua za haraka ni pamoja na kudhibiti upandaji holela wa bei usiozingatia gharama halisi za uingizaji mbolea nchini kwa kutangaza bei elekezi zinazopaswa kuzingatiwa na wafanyabiashara katika maeneo ya uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekutana na uongozi wa kiwanda cha mbolea cha Minjingu kwa lengo la kuzipatia ufumbuzi changamoto za kiwanda ili kuhakikisha kinaongeza uzalishaji wa mbolea kutoka wastani wa tani 30,000 hadi kufikia tani 100,000 kwa mwaka. Aidha, Serikali inaendelea kuhamasisha wawekezaji wapya wa viwanda vya mbolea ambapo kampuni ya *Intracom Fertilizers Limited* kutoka Burundi imejitokeza na inajenga kiwanda katika Mkoa wa Dodoma chenye uwezo wa kuzalisha tani 600,000 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, hatua hizo zinazochukuliwa na Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi zitasaidia kupunguza bei ya mbolea.

**SPIKA:** Mheshimiwa Oran Manase Njeza, swali la nyongeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ningependa kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa katika Wilaya ya Mbeya, kuna madini ya aina ya *calcium carbonate* kwa wingi na *NDC* katika miaka ya 2006/2007 walikuwa na mkakati wa kuanzisha kiwanda ili watengeneze mbolea, *CAN*: Je, ni lini Serikali itaanza kujenga kiwango hicho kwa kushirikiana na *NDC*?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa bei hizi za mbolea zinatishia upungufu mkubwa wa chakula: Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha inarudisha ruzuku kama ilivyo kwenye nchi nyingine za *SADC* na Afrika Mashariki?

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza la ujenzi wa kiwanda, ni dhamira ya Serikali kuona ujenzi wa viwanda vingi zaidi vya mbolea vinakuwepo hapa nchini ili kutatua changamoto ya upatikanaji wa mbolea na kupunguza bei ya mbolea na kupunguza bei ya mbolea kama ilivyo sasa. Nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba sisi kama Wizara pamoja na wenzetu wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, tutakaa pamoja ili tuhakikishe kwamba wazo hili ambalo lilianzishwa mwaka 2006 liweze kukamilika na kuwapungizia adha wakulima.

Mheshimiwa Spika, la pili, ni la kuhusu ruzuku. Katika bajeti yetu ambayo tutaisoma mwezi ujao na pia katika utekelezaji ambao utaanza mwaka ujao wa fedha, tumedhamiria kutenga mfuko maalum *(price stabilization fund)* kwa ajili ya kudhibiti upandaji wa bei ya pembejeo ikiwemo na bei za mazao.

Mheshimiwa Spika, hivyo, nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba hii ni sehemu ambayo pia tunaipa umuhimu mkubwa na Serikali imedhamiria kuanzisha mfuko wa ruzuku ambao utahakikisha unasaidia kupunguza maumivu ya wakulima na hasa katika upatikanaji wa bei ya mbolea ambayo itakuwa ni rafiki kwa mkulima.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zacharia Paul Issaay, swali la nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali na kwa kuwa viwanda vilivyotajwa ni viwili tu nchini: Je, Serikali haioni kuwa ni wakati muafaka sasa wa kuhamasisha wawekezaji wengine ili uzalishaji wa mbolea nchini uwe mkubwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zacharia Issaay, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema awali, moja kati ya mikakati tuliyonayo hivi sasa ni kuendelea kuwakaribisha wawekezaji wengi zaidi wa viwanda vya mbolea ili kwa pamoja tusaidiane kutatua changamoto iliyoko hivi sasa ya upatikanaji wa mbolea. Tunaamini katika misimu michache inayokuja, kiwanda cha *Itracom* na Minjingu ambacho sisi kama Wizara tumewasaidia kuzungumza na Benki za *TADB* na *CRDB* kuongeza *expansion*, tutakuwa tumetatua changamoto hii ya upatikanaji wa mbolea kwa kiwango kikubwa sana. Pia bado tunakaribisha makampuni mengine, na kama Serikali tunaendelea pia kukaribisha makampuni mengi zaidi ili tuondokane na changamoto hii ya upatikanaji wa mbolea hapa nchini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaelekea Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Elibariki

Emmanuel Kingu, Mbunge wa Singida Magharibi sasa aulize swali.

Na. 91

**Ujenzi wa Majosho Katika Kata za Ikungi**

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itajenga majosho ya mifugo katika Kata za Makilawa, Igelansoni, Iyumbu, Ighombwe, Mgungira na Mwaru Wilayani Ikungi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu Mbunge wa Singida Magharibi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/ 2022, Wizara inakamilisha ujenzi wa majosho 168 katika Halmashauri 80 kwa gharama ya shilingi bilioni 3.033. Aidha, kati ya majosho hayo, majosho mawili yanajengwa katika Kata za Mgungira na Siuyu katika Halmashauri ya Ikungi.

Mheshimiwa Spika, Wizara inatambua uhitaji mkubwa wa majosho katika maeneo mbalimbali nchini. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara itaendelea na ujenzi wa majosho katika maeneo yenye uhitaji yakiwemo ya Jimbo la Ikungi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Elibariki Kingu, swali la nyongeza.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nataka nijue sasa *commitment* ya Serikali kwa Kata zilizobaki, kwa maana katika majibu ya msingi inaonesha kwamba kuna Kata moja

tu imejengewa majosho na Jimbo la Singida Magharibi ni moja ya Majimbo ambayo yana wafugaji wengi sana:-

Je, Serikali lini itakwenda kutekeleza ujenzi wa majosho katika Kata za Igelansoni, Makilawa, Mwaru, Igombwe pamoja na Minyuge?

Swali la pili: Je, Waziri yuko tayari kuongozana nami Mbunge akajionee namna wafugaji wanapata adha kulingana na changamoto ya magonjwa katika mifugo yao kutokana na kutokuwepo kwa majosho?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu.

**WAZIRI MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Elibariki Kingu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, natambua ya kwamba uhitaji wa majosho nchini ni mkubwa na kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi tumeelekezwa kuweka josho kwenye kila Kijiji kilicho na mifugo. Kwa hiyo, kwenye mpango wetu wa Wizara, mwaka huu fedha tutakaouanza tumeweka pia mpango wa kuendelea kujenga majosho kwenye maeneo mbalimbali hapa nchini. Sasa tutatoa kipaumbele kwenye maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Kingu; Gelansoni, Iyumbu, Igombwe na maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juu ya suala la kuambatana naye ili twende kukutana na wafugaji wake. Niko tayari kufanya hivyo na pengine kama tutapata wakati, *weekend* mojawapo tunaweza kuambatana ili tukutane na hao wafugaji.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Michael Mwakamo, swali la nyongeza.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Spika, kwenye Jimbo la Kibaha Vijijini kwenye Kata ya Magindu, Ruvu, Gwata na Dutumi kuna wafugaji wa kutosha lakini

majosho hakuna: Je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kunipatia sehemu ya majosho aliyoyataja kwamba yapo kwenye bajeti? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwakamo, Mbunge wa Kibaha kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tutapanga vizuri kwenye majosho ambayo Serikali itatupa fedha kwa mwaka wa fedha ujao ili kuhakikisha kwamba Jimbo la Kibaha pia linapata majosho, yanaweza yasiwe yote lakini angalau maeneo yaliyo muhimu yenye wafugaji wengi, tutaongea pamoja na Mheshimiwa Mbunge ili tuone kwamba maeneo hayo yanapata majosho pia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya, swali la nyongeza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Tatizo la majosho lipo maeneo mengi. Halmashauri ya Mji wa Bunda, nadhani mjomba unajua kuna wafugaji wengi, lakini kuna malambo ambayo hayako kwenye hali nzuri; Kinyambwiga, Gushigwamara, Kisangwa pamoja na Rwabu: Ni lini mtayakarabati hayo malambo ili wananchi wa Bunda waweze kupata huduma ya kulishia mifugo yao?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bulaya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nilishafika Bunda, nilishayaona hayo malambo, tulishaenda na Mheshimiwa Getere tukazunguka tukaona maeneo ya malambo ambayo

yameharibika. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwenye mwaka ujao 2023 tuna mpango wa kukarabati malambo mengi kidogo. Pia tuna mpango wa kujenga malambo mapya, yatakuwa mengi, zaidi ya manne ambayo mlitupa bajeti ya mwaka huu. Kwa hiyo, tutafikiria kuangalia wananchi na wafugaji wa Bunda ili tuone malambo yao ambayo yameharibika ni kwa namna gani tutaweza kuyakarabati.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Nicholaus Ngassa, swali la nyongeza.

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Changamoto ya majosho iliyopo kwenye Singida Magharibi ni sawa na changamoto iliyopo kwenye Jimbo la Igunga, kwenye Kata ya Kinikinila, Isakamaliwa, Mamashimba, Kilungu pamoja na Igulubi:

Je, ni lini Wizara itatatua changamoto hii, ukizingatia Jimbo la Igunga ni miongoni mwa majimbo yenye mifugo mingi nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nicholaus Ngassa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Igunga na Wilaya ya Igunga kwa ujumla tulipangia mwaka huu wa fedha kwamba tungeweza kujenga majosho zaidi ya matano, lakini majosho matatu hatukuweza kuyajenga kwa sababu hatukupata ushirikiano mzuri na Ofisi ya Mkurugenzi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaamini kwenye bajeti ijayo, kwa sababu pia tumetenga majosho kwa Wilaya ya Igunga, tutapata ushirikiano wa kutosha na kwa hivyo maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge tutayapangia kujenga majosho. Tupate ushirikiano wa kutosha ili kwamba

majosho yatakayopangwa kwa wilaya hiyo basi yaweze kukamilishwa.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Miraji Mtaturu, swali la nyongeza.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Jimbo la Singida Mashariki ni miongoni mwa majimbo yenye wafugaji wengi sana, na Mheshimiwa Waziri alishawahi kuniahidi majosho takribani matatu kwenye Kata za Siuyu, Ulyapiti, pamoja na Isuna.

Sasa ni nini kauli yake kwa mwaka huu wa fedha?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri unao uhuru wa kujibu; lakini kwa sababu swali lake linahusu hasa bajeti ambayo bado haijaletwa hapa ndani. Unao uhuru wa kujibu sasa hivi ama utamtafutia majibu wakati huo wa bajeti.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, namtafutia majibu.

**SPIKA:** Sawa. Atakutafutia majibu Mheshimiwa ili awe ameipitia ile bajeti yake. Mheshimiwa ili awe ameipitia ile bajeti yake. Mheshimiwa Monni, swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Katika Vijiji vya Ombiri, Muungano, Golopaguma, Dalayi navyo vina matatizo makubwa ya majosho kwa ajili ya mifugo. Na ikumbukwe kwa Mkoa wa Dodoma Wilaya ya Chemba ndiyo yenye mifugo mingi. Naomba kujua *commitment* ya Serikali sasa ni lini tutaenda kujenga majosho kwenye vijiji hivyo? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi majibu.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa Wilaya na Mkoa wa Dodoma kwa ujumla una mifugo mingi sana. Kwa mwaka huu wa fedha tunaoenda nao angalau kila wilaya tulikuwa tumewapangia majosho si chini ya manne, tuliwapa upendeleo kidogo. Sasa safari ijayo tutaangalia pia hasa kwa Jimbo la Mheshimiwa Mbunge wa Chemba, tuone ni kwa namna gani tunaweza kupanga kujenga majosho mengine ili Mheshimiwa Mbunge na wafugaji wake waweze pia kufaidika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Amar, swali la nyongeza.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa hadi leo ni mwaka wa kumi na mbili niko Bungeni na sijawahi kutembelewa na Waziri wa Mifugo katika jimbo langu, je, Waziri atakuwa yuko tayari kutembelea jimbo langu kuja kuongea na wafugaji ikiwemo na changamoto hizo za majosho na mambo mengine?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu Mbunge wa Nyang'hwale, huyu.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Nyanghwale, Mbunge ambaye pia ana wafugaji wengi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, niko tayari kumtembelea Mheshimiwa Mbunge na jimbo lake. Najua wapo wafugaji wengi na kwa hiyo kumkosa Waziri wa Mifugo au msaidizi wake itakuwa ni tatizo. Sasa niko tayari kufanya hivyo kipindi hiki cha bunge tunaweza kutafuta wikiendi mojawapo twende au baada ya Bunge ili ya kwamba tuweze kukutana na wafugaji wake tutatue matatizo na changamoto zilizoko zinazohusiana na mifugo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dunstan Kitandula, swali la nyongeza.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa, naomba niulize swali moja la nyongeza. Mheshimiwa Waziri ulipokuja kutembelea mnada wa Hororo, mojawapo ya changomoto tuliyoizungumza ni ukarabati wa lambo la Ng'ombeni. Je, ahadi iko pale pale, kwamba litakarabatiwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kitandula kama ifuatavyo: -

Ahadi yetu Mheshimiwa Mbunge iko pale pale, na tutafanya hiyo kazi mpaka ikamilike ikiwa ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa mnada huo. Kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge kuwa na uhakika kwamba sisi kazi hiyo tulishaanza kuifanya na kwa hivyo tutaikamilisha kama ambavyo tumepanga. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Waheshimiwa Wabunge sasa tunaelekea Wizar a ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Ally Anyingulile Mlaghila Jumbe aulize swali lake.

Na. 92

**Ujenzi wa Barabara ya Kyela - Ludewa**

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE** aliuliza: -

Je, ni lini Barabara inayounganisha Wilaya ya Kyela na Ludewa kupitia Matema, Ikombe mpaka Liuli itaanza kujengwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Naibu wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFRY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ally Anyingulile Jumbe Mlaghila, Mbunge wa Kyela kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara inayounganisha Wilaya ya Kyela na Ludewa yenye urefu wa km 156 inapita kwenye safu ya milima ya Livingistone yenye miteremko mikali na miamba kubwa ya mawe.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza kufungua barabara hii kwa awamu kwa kufyeka misutu na kupasua miamba. Azma ya Serikali ni kuifungua barabara yote kuanzia Lupingu (Ludewa/ - Lumbila-Matema (Kyela).

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Ikombe, tangu kuumbwa kwa dunia hii hawajawahi kuona gari. Zimebaki kilomita moja na nusu, ili barabara ifunguke mpaka Kijiji cha Ikombe, na mwezi wa kumi tuliambiwa kwamba mkandarasi yuko tayari, amepatikana.

Je, Mheshimiwa Waziri anajua kwamba mkandarasi mpaka sasa hivi hayuko *site?*

Mheshimiwa Spika, mbili, barabara ya Ngamanga – Lusungo Matema inaenda moja kwa moja Ikombe, pale kuna daraja la bilioni 4.50 lakini eneo la Ngolwa halina daraja. Je, unaonaje sasa ni wakati sahihi wa kujenga daraja la Ngorwa, ili barabara ipitike kirahisi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi. Waheshimiwa Wabunge mnaongea kwa sauti kubwa sana tupunguze sauti kidogo. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFRY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya mheshimiwa Ally Anyingulile Jumbe Mlaghila, Mbunge wa Kyela kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba wananchi ambao hawajaona gari nimuhakikishie kwamba barabara hiyo tunaifikisha kwenye hicho kijiji ili wananchi hao waweze kuiona gari katika maisha yao.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, naomba nichukue nafasi hii kumuagiza Meneja wa Mkoa wa Mbeya, ahakikishe kwamba mkandarasi anarudi *site* na anafanya kazi ambayo anatakiwa kuifanya. Lakini kuhusu daraja hili ambalo amelisema, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali italijenga hili daraja ili paweze kuwa na mawasiliano ambayo yamekosekana kwa sasa. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Judith Kapinga, swali la nyongeza.

**MHE. JUDITH S. KAPINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Je, ni lini barabara ya kutoka Tanga, Mkumbi, Lugali inayoenda kuunganika na barabara ya Lutoho, Nyasa yenye takribani kilomita 18 itajengwa kwa kiwango cha lami, ikizingatia imekuwa na adha kubwa za kiuchumi kwa wananchi wa maeneo hayo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFRY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kapinga, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoainisha ni kweli ipo na imeahidiwa na ipo hata kwenye ilani. Nataka nimhakikishie

Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami kulingana na upatikanaji wa fedha. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jonas William Mbunda, swali la nyongeza.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Barabara ya Mbinga, Litembo, Kili ilitolewa ahadi na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nilitaka nijue je, Serikali ina mpango gani wa kuanza kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFRY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunda Mbunge wa Mbinga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ahadi zote ambazo zimetolewa na Waheshimiwa viongozi wakuu wa nchi, ni ahadi ambazo tunazitekeleza. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunda, Mbunge wa Mbinga, kwamba barabara hii ipo kwenye mpango kwa ajili ya kuijenga kama ambavyo viongozi wetu walioahidi na sisi tutamhakikishia kwamba ahadi hiyo tutaitekeleza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Joseph Mhagama, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, wananchi wa Jimbo la Madaba, na wananchi wa Ludewa wamesubiri kwa hamu sana ujenzi wa Barabara ya Mababa – Mkiu – Ludewa kwa kiwango cha lami na hii imekuwa ahadi ya kudumu ya Serikali. Ni lini sasa Serikali itatekeleza azma hii?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFRY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Mhagama, Mbunge wa Madaba kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mkiu kwenda Madaba ni barabara ambayo inaanzia Itoni, Lusitu, Mkiu kwenda Madaba ambayo ndiyo inaenda kwenye madini ya chum ana makaa ya mawe. Usanifu ulishakamilika kwa kipande cha Mkiu kwenda Luhuu hadi Madaba, Serikali inaendelea kutafuta fedha sasa kuianza kuijenga kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hiyo itajengwa kwa sababu pia ni barabara muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu ya Tanzania, Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Fiyao, swali la nyongeza.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Nataka kujua ni lini Serikali itaanza upanuzi wa barabara kutoka Mpemba mpaka Tunduma – Transfoma ili kuepusha changamoto ambayo wananchi wamekuwa wakiipata kutokana mlundikano na msongamano mkubwa wa magari makubwa ambayo yamekuwa yakivuka mpaka wa Tanzania?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFRY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Stella Fiyao, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Songwe kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja imeshafanyiwa usanifu na ni sehemu ya barabara ya kuanzia Igawa – Mbeya hadi Tunduma. Na barabara hii kipande cha Mpemba hadi Tunduma kitapanuliwa kuwa njia nne. Kwa hiyo iko kwenye mpango na tunategemea mwaka ujao wa

fedha tutaanza kupanua hii barabara kuwa njia nne ili kupunguza msongamano ambao upo katika mji wa Tunduma. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Spika, nauliza je ni lini barabara ya kuunganisha kutoka Mbambay hadi Ludewa itajengwa kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFRY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, barabara inayotokea Mbambay Wilaya ya Nyasa kuja Litui na kuvuka daraja la Luhuu tayari tumeshakamilisha daraja na usanifu umeshakamilika kati ya Mbambay hadi Litui, fedha inatafutwa ili sasa tuanze kuijenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na swali la Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Mbunge wa Korogwe Vijijini.

Na. 93

**Ujenzi wa Barabara ya Korogwe – Dindira – Bumbuli Hadi Soni**

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara ya Korogwe – Dindira – Bumbuli hadi Soni

ambayo ilitengewa fedha kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi katika mwaka wa fedha 2020/2021?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFRY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Mbunge wa Korogwe Vijijini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, upembuzi yakinifu na Usanifu wa Kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami Barabara ya Korogwe – Dindira – Bumbuli – Soni (km 77) unafanyika kwa awamu. Sehemu ya kutoka Soni hadi Bumbuli (km 21.7) upembuzi yakinifu na usanifu wa Kina umekamilika. Kwa Sehemu iliyobaki ya kutoka Bumbuli hadi Korogwe (km 55.3), kazi ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina inaendelea na imefikia asilimia 81.

Mheshimiwa Spika, baada ya Kazi ya Upembuzi Upembuzi yakinifu na Usanifu wa Kina kukamilika na gharama za ujenzi kujulikana, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami.

**SPIKA:** Mheshimiwa Timotheo Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kama tutakwenda na majibu haya mpaka wakati wa bajeti, hali itakuwa tete hapa. Pamoja na hayo naomba kuuliza swali mawili ya nyongeza. Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umekuwa ukifanyika kwa awamu na tayari kipande cha kwanza kimekamilika na kipande cha pili kiko asilimia 81. Serikali haioni sasa ni vizuri kuanza pia ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami, kwa awamu kwa vipande tukianza na bajeti inayokuja mwaka 2022/2023?

Mheshimiwa Spika, Pamoja na ahadi hizo za barabara ya lami, Serikali imekuwa ikijitahidi kutenga fedha kwa ajili ya matengenezo na ukarabati wa barabara hii pamoja na barabara ile ya Korogwe - Magoma kwenda mpaka Maramba. Lakini matengenezo yamekuwa yamekuwa yakifanyika kwa kuchelewa sana lakini pia kifusi kinachowekwa kinakuwa hakina ubora unaoendena na mazingira tuliyokuwa nayo. Na hivi tunavyoongea sasa hivi barabara ya kwa Shemshi haipitiki...

**SPIKA:** Swali Mheshimiwa Mnzava.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Haipitiki kwa sababu vifusi havijasambazwa, ni nini kauli ya Serikali juu ya wakandarasi hawa wanaofanya kazi chini ya kiwango na kuwasababishia wananchi wetu matatizo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFRY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mnzava, Mbunge wa Korogwe Vijijini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inafanya usanifu wa kina wa barabara hii yote aliyoainisha Mheshimiwa Mbunge, ya kutoka Soni, Bumbuli, Dindira hadi Korogwe ili gharama halisi iweze kufanyika na tuone kama kutakuwa na ulazima wa kuwa na loti moja ama mbili. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa tukishakamilisha usanifu wa hiyo barabara tuona namna ya kuanza kuijenga hiyo barabara; na ni azma ya Serikali kuijenga barabara yote hii kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, na kuhusu barabara aliyoitaja ya pili, ambayo inaanzia Korogwe, Bombo Mtoni, Maramba hadi Mabokweni, barabara hii inapita kwenye sehemu nyingi ya miinuko. Kwa kawaida arabara kwa kawaida nyingi ambazo zinapita kwenye miinuko zinaoshwa na mvua, tumewaagiza mameneja, wa mikoa waweze kuainisha maeneo yote korofi,

ili tutafute namna ya kudhibiti maeneo yote yaliyo bondeni na kwenye miinuko ili tuweze kutafuta utaratibu muhimu wa kuweza kudhibiti hayo maeneo ikiwa ni pamoja na kuweka lami nyepesi ama zege ama strip za mawe ambazo tunahakika barabara hizi zitakuwa na uwezo wa kuitika kwa muda mrefu bila kuitika.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Stanslaus Mabula swali la nyongeza.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa swali la nyongeza, naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri barabara ya kutoka Tambuka Reli, Nyagulugulu mpaka Mahina ni lini Serikali itaanza kuijenga kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFRY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Stanslaus Mabula, Mbunge wa Nyamagana kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeza Mheshimiwa Mabula, amekuwa akija ofisini kuhusu barabara hii. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Nyamagana kwamba Serikali inakamilisha usanifu wa kina wa barabara hii na ina mpango wa kuanza kuijenga barabara hii kwa haraka sana kwa kiwango cha lami kwa sababu kwa watu ambao wamefika Mwanza, ndio barabara pekee ambayo inapotokea changamoto yoyote kati ya Mkuyuni, Igogo kwenda mjini ndiyo inaweza kuwa ni bypass kwa ajili ya watu kufika mjini.

Mheshimiwa Spika kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mpango wa Serikali ni kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami haraka inavyowezekana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi Mbunge wa Muhambwe sasa aulize swali lake.

Na. 94

**Hitaji la Mawasiliano ya Simu na TBC Redio Muhambwe**

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itajenga minara ya simu na TBC Redio katika Jimbo la Muhambwe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi, Mbunge wa Muhambwe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kuhusu Ujenzi wa Minara ya simu, Serikali itajenga minara ya mawasiliano katika Kata za Bunyambo, Murungu na Nyaruyoba ambazo zimebainika kuwa na changamoto ya upatikanaji wa huduma za mawasiliano katika Jimbo la Muhambwe. Zabuni ya minara hiyo itatangazwa kabla ya mwaka wa fedha wa 2021/2022 kukamilika.

(b) Kuhusu TBC Redio, mtambo wa masafa ya *FM* katika Jimbo la Muhambwe, Mwezi Machi, 2022 mtambo huo ulipigwa na radi iliyoharibu vipuri vyake. Vipuri hivyo vimeshaagizwa na tayari vimeshawasili nchini. Kazi ya kufunga vipuri hivyo itakapokamilika, na kuwashwa na kufanyiwa majaribio ya kiufundi kabla ya tarehe 30 Mei 2022

hivyo kurejesha usikivu wa TBC katika Jimbo la Muhambwe na maeneo ya jirani. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi swali la nyongeza.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ninaishukuru Serikali kwa kutuwekea mpango mzuri wa kutuletea minara katika Jimbo letu. Hata hivyo, Jimbo la Muhambwe lina mnara mmoja tu wa *TTCL* ambao umelemewa na badala yake inatumia kufanya *roaming* kwa minara ya kampuni nyingine.

Je, Serikali haioni sasa ni muda muafaka wa kuweka minara mingi ya *TTCL* ili tuweze kupata usikivu lakini pia mawasiliano ya bei nafuu?

(b) Mheshimiwa Spika, tunaishukuru Serikali pia kwa kutuletea kifaa hicho ambacho kitaenda kuboresha usikivu wa *TBC* Redio katika Jimbo letu, hata hivyo usikivu wa *TBC* Redio katika Jimbo letu ni hafifu sana inayopelekea wananchi wa Muhambwe kusikiliza zaidi Redio ya Burundi kuliko ya *TBC* Redio.

Je, nini mkakati wa Serikali kuboresha zaidi usikivu wa Radio katika Jimbo zima la Muhambwe? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi Mbunge wa Muhambwe kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri ambayo anaifanya, hivi

leo nimejulishwa na Mheshimiwa Waziri amekuwa akiwasiliana nae kukumbushia kuhusu zile ahadi zake katika kipindi cha kampeni, Mheshimiwa Waziri ameshatoa maelekezo na ahadi hizo ambazo zinalenga katika Wizara yetu zitafanyiwa kazi zote. Vilevile suala la usikivu kama ambavyo nimejibu katika swali la msingi ni kwamba kifaa hiki kitakaporejeshwa na kufanyiwa majaribio nina uhakika kabisa kwamba tatizo la usikivu katika Jimbo la Muhambwe litakuwa limemalizika kabisa. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwantumu Zodo swali la nyongeza.

**MHE. MWANTUMU M. ZODO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana changamoto za mawasiliano kwa Jimbo la Muhambwe zinafanana sana na changamoto za mawasiliano kwa Jimbo letu la Muheza katika Tarafa ya Amani ambayo ni Kata ya Amani Kisiwani Mbomole, Misalai, Zirai na Kwezitu,

Je, ni lini sasa Serikali inakwenda kujenga minara ya simu ili kutatua changamoto ya mawasiliano kwa wananchi wa Tarafa ya Amani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari Mawasiliano na Teknolojia ya Habari majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwantumu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuwekeza kuhakikisha kwamba inatatua changamoto ya mawasiliano kulingana na maelekezo ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Jimbo la Muheza tumeliingiza katika mpango wa utekelezaji wa mradi wa Tanzania kidigitali, hivyo tunaamini kwamba kabla ya mwaka wa fedha huu haujaisha zabuni hii itakuwa imeshatangazwa na hatimaye mtoa huduma atapatikana kwa ajili ya Jimbo la Muheza. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari Mawasiliano na Teknolojia ya Habari tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara Mheshimiwa Esther Lukago Midimu Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 95

**Kuongeza vyanzo vya Mitaji kwa akinamama Wajasiriamali**

**MHE. ESTHER L. MIDIMU** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza vyanzo vya mitaji kwa akina Mama wajasiriamali mbali ya fedha zinazotolewa na Halmashauri?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji Viwanda na Biashara, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, napenda kujibu Swali la Mheshimiwa Esther Lukago Midimu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikiwawezesha kimtaji akina mama kupitia Mifuko ya Uwezeshaji inayoratibiwa na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Serikali ilianzisha Mifuko hii ili kuwasaidia wananchi wake hasa makundi maalum kwa lengo la kupunguza changamoto ya upatikanaji wa mitaji yenye masharti nafuu.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali ilianzisha Benki ya Wanawake Tanzania na ili kuboresha huduma shughuli za Benki hiyo zilihamishiwa katika Benki ya Tanzania *Postal Bank*

sasa hivi inaitwa Tanzania *Commercial Bank.* Aidha, katika mwaka wa fedha wa 2020/2021 Benki hiyo kupitia dirisha la wanawake imeendelea kutoa mikopo kwa wanawake, ambapo kiasi cha Shilingi Bilioni 22.3 kimetolewa kwa wanawake 6,327. Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Midimu swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwanza kabisa nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kufuta riba kwa mkopo wa asilimia 10 kwa wanawake.

Mheshimiwa Spika, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa wanawake wengi ni waaminifu sana katika masuala ya kurudisha mikopo, Je Serikali ina mpango gani wa kuongeza muda wa marejesho? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili kwa kuwa mahitaji ya mikopo ni mengi kwa wanawake, vijana na walemavu. Je, Serikali au Wizara ina mpango gani wa kuongeza asilimia 15, asilimia Saba wakopeshwe wanawake, asilimia Tano wakopeshwe vijana, asilimia Tatu watu wenye ulemavu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji Viwanda na Biashara majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Esther Midimu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Esther Midimu kwa kufuatilia kwa makini sana kuhusiana na maendeleo ya wanawake na hasa kushiriki katika shughuli za kiuchumi kupitia ujasiriamali.

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali imekuwa ikifanya juhudi mbalimbali kama nilivyosema kwa kuanzisha mifuko pia kwa kuweka mfuko maalum ambapo kuna Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake, pia mfuko wa asilimia 10 zinazotengwa katika Halmashauri lakini pia kupitia taasisi za fedha nyingine zinazolenga kuhudumia makundi mbalimbali yakiwemo wanawake.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaendelea kuongeza fedha kwa namna tofauti tofauti ili kuhakikisha wanawake wanashiriki kikamilifu katika kuongeza uchumi wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu hitaji la pili nipende kumshukuru Mheshimiwa Esther kwamba ametoa mawazo ya kuona namna gani Serikali itaongeza asilimia kutoka zile asilimia 10 zinazotengwa katika Halmashauri kwenda asilimia 15. Nadhani hili ni suala zuri tunalichukua ili kulifanyia kazi pamoja na wenzetu wa TAMISEMI. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Waheshimiwa Wabunge tumalizie Wizara ya mwisho, Wizara ya Fedha na Mipango Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka Mbunge wa Liwale, sasa aulize swali lake.

Na. 96

**Halmashauri ya Liwale kurejeshewa fedha za Miradi ya Kimkakati**

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani kuirejeshea Halmashauri ya Liwale fedha za kutekeleza miradi ya kimkakati iliyorudishwa Hazina ili iweze kujenga Stendi ya Kisasa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka, Mbunge wa Liwale kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa stendi ya kisasa ya Liwale ni moja kati ya miradi ya kimkakati ya kuongeza mapato kwa Halmashauri, ambapo mwaka 2018 Serikali iliingia mkataba na Halmashauri ya Wilaya ya Liwale Mkoani Lindi kutekeleza mradi huo kwa gharama ya Shilingi Bilioni 1.2.

Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali ni kuhakikisha kuwa mradi huu unatekelezwa. Hivyo, kutokana na umuhimu wa mradi huu, katika mwaka 2021/2022 Halmashauri ya Wilaya ya Liwale imetengewa Shilingi Bilioni Moja kwa ajili ya ujenzi wa stendi ya kisasa ya Liwale. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Liwale kupitia Ofisi ya Rais TAMISEMI inahimizwa kukamilisha taratibu za maombi ya fedha na kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zuberi Kuchauka swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza nishukuru Serikali kwa kuonesha *commitment* ya kutaka kujenga stendi hii ya kisasa, lakini nimewasiliana na watu wa Halmashauri, wanasema kwamba kwa upande wa Halmashauri mchakato umeshakamilika kutoka kwenye ngazi ya Wilaya mpaka kwenye ngazi ya Mkoa. Sasa hivi Je, Mheshimiwa Waziri upo tayari kuwasiliana na watu wa TAMISEMI kwa kuona kwamba mradi huu umekwama kwenye ngazi hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili kwa sababu kumebakizwa miezi miwili bajeti aliyoitaja hapo inakwenda kukamilika. Je, Mheshimiwa Waziri upo tayari kututengea tena

fedha kwenye bajeti hii iwapo kama fedha zile za mwanzo zitakuwa bado hazijatumika? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu maswali hayo naomba nimpongeze sana Kaka yangu Kuchauka kwa kazi nzuri anayoifanya katika Jimbo la Liwale.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha na Mipango ipo tayari kuwasiliana na Wizara ya TAMISEMI nachukua nafasi hii nitoe maelekezo kwa wataalam wetu kufanya mawasiliano ya haraka sana kuona hadhi ya *project* hii imefikia wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la pili kwa kuwa Serikali ina nia njema ya kujenga stendi ya kisasa, basi kama haikukamilika mwaka wa 2021/2022 basi bajeti inayokuja tutatenga tena fedha hiyo ili kusudi tuone mradi huo umekamilika. Ahsante.*(Makofi)*

**SPIKA:** Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge na majibu kutoka Serikalini. Ninaleta matangazo niliyonayo hapa mbele, tutaanza na tangazo linalohusu wageni waliopo hapa ndani.

Waheshimiwa Wabunge, kwanza ni wageni waliopo jukwaa la Spika na hawa ni wageni wangu 10 kutoka Benki ya *NMB* na yupo Ndugu Filbert Mponzi ambaye ni Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi na Biashara, karibu sana. Yupo pia Ndugu Juma Kimori ambaye ni Mkuu wa Kitengo cha Fedha, karibu sana. Ndugu Emmanuel Akonaay ambaye ni

Mkuu wa Kitengo cha Rasilimaliwatu, karibu sana. Ndugu Richard Mtapa ambaye ni Meneja Mwandamizi Huduma kwa Taasisi za Serikali, karibuni sana. Bi. Aikansia Muro ambaye ni Mkuu wa Idara ya Wateja Binafsi, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo pia Ndugu Adelard Mang'ombo ambaye ni Meneja Mwandamizi Huduma kwa Serikali. Pia yupo Ndugu Vicent Mnyanyika ambaye ni Meneja Idara ya Mahusiano na Mawasiliano, karibu sana. Ndugu Ali Ngingite ambaye ni Meneja Mwandamizi Mikopo ya Wateja binafsi. Ndugu Nsolo Mlozi ambaye ni Meneja Kanda ya Kati Dodoma, Singida na Morogoro, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana nadhani Viongozi wenzake wa *NMB* watakuwa wameona kwamba Meneja wao wa Kanda waliomuweka huku anafanya kazi nzuri na Wabunge. Pia Bi. Grace Matemu ambaye ni Meneja wa Tawi la Bunge, *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana. naona makofi yamezidi Zaidi, Grace naye anatuhudumia vizuri hapa Bunge yakishapigwa makofi namna hii huwa tunatamani wapande Cheo lakini wasihamishwe hapa Bunge. Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi/Kicheko)*

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Naibu Spika ambaye ni Mheshimiwa Venance Mwamoto ambaye alikuwa Mbunge mwenzetu hapa ndani, karibu sana, karibu sana. Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka huyu alikuwa Mbunge wa Kilolo Mheshimiwa Justin Nyamoga ndiye Mbunge wa Kilolo sasa, karibu sana Mheshimiwa Mwamoto na alipokuwa hapa alikuwa na Vyeo vingi naona wanamichezo wamefurahi kumuona. Karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia tunao wageni Wawili wa Mheshimiwa Dkt. Joseph Mhagama ambao ni wageni kutoka *Universal Peace Federation* Tawi la Tanzania na hawa ni Dkt. Stylos Simbamwene ambaye ni Katibu Mkuu wa *Universal Peace Federation* karibu sana. Tunao wageni 24 wa Mheshimiwa Stanslaus Mabula ambao ni wanawake vinara

kutoka Mkoa wa Mwanza, Shinyanga na Kagera wakiongozwa na Mwenyekiti wao Ndugu Hadija Liganga. Karibuni sana wanawake vinara. *(Makofi)*

Tunao pia wageni Saba wa Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo hawa wanatoka Chuo Kikuu cha Dodoma wanasoma *Masters* lakini pia anao wageni 46 ambao ni wanafunzi pia kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma ambao wanasoma Digrii ya Kwanza, karibuni sana. Tunao wageni 29 wa Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu Dodoma kutoka Jimbo la Longido Mkoa wa Arusha, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunae mgeni wa Mheshimiwa Benaya Kapinga ambaye ni mpiga kura wake na Diwani mstaafu huyu ni Ndugu Alto Hyera karibu sana. Tunao wageni 15 wa Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma, karibuni sana. Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi ambao ni familia yake kutoka Mkoa wa Mwanza na hawa wameongozana na Mke wake Ndugu Jasmine Salumu, haya jamani naona wengine wamemuona wifi yao wengine wamemuona shimeji. Kwa hiyo karibuni sana familia ya Mheshimiwa Mbunge na Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi umefanya vizuri kabisa kuja kumtambulisha shemeji humu ndani na wifi humu ndani. *(Makofi/Kicheko)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Eng. Mwanaisha Ulenge ambao ni rafiki zake kutoka Tanga na mwingine anatoka *TBA* rafiki za Mheshimiwa Ulenge karibuni sana. Waheshimiwa Wabunge tunao wageni ambao wametutembelea kwa ajli ya mafunzo, tunao wageni 12 ambao ni watumishi wa Kanisa la Waadventista Wasabato kutoka Mkoa wa Dodoma wakiongozwa na Padri Emmanuel Andrew, karibuni sana. Tunaye mgeni mmoja kutoka Jijini Dar es Salaam na huyu ni ndugu Venance Babu karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 70 ambao ni viongozi wa Serikali ya Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya

- *MUST* ambao wameongozwa na Spika wa Bunge la Chuo hicho Ndugu Michael Ollomi, karibuni sana wanafunzi kutoka *MUST* Mbeya na wameongozana na mtu ambaye ana cheo kama changu kwenye Chuo chao karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo pia viongozi 45 wa Shirikisho la Vyuo vya Elimu ya Juu Tanzania *(TAHLISO)* kutoka vyuo mbalimbali nchini wakiongozwa na Makamu wa Rais wa Shirikisho hilo Ndugu Rabia Hassani. Karibuni sana kwa ajili ya mafunzo. *(Makofi)*

Lakini tunao wanafunzi 50 na Walimu 5 kutoka shule ya Sekondari ya Wasichana Sega ya Morogoro Mjini wakiongozwa na Afisa Utumishi wa shule hiyo ndugu Happiness Stephen. Karibuni sana Bungeni ndugu zetu ambao mmekuja hapa kujifunza namna ambavyo Shughuli za Bunge zinafanyika. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge nimewatangaza hapa wageni wetu kutoka *Bank* ya *NMB* na mmepiga makofi, sijui kama mlikuwa mnajua kuhusu hili tangazo. Haya! Siku ya leo ndugu zetu wa *NMB* watatupa *Iftar* baada ya kuhitimisha Shughuli za Bunge na *Iftar* hii itafanyika kwenye eneo lile la maegesho ya magari. Kwa hiyo mara baada ya kuhitimisha Shughuli za Bunge leo jioni tutakuwa na *Iftar* ambayo viongozi wa *NMB* na *Bank* yetu ya *NMB* imetuandalia. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wote na watumishi wote mnakaribishwa sana kwenye *Iftar* hiyo. *(Makofi)*

Hawa ndugu zetu wa *NMB* wajue tu humu ndani naona kuna watu wamevalia tayari ili wasije wakachelewa kubadilisha kwenda kuvaa namna ambayo ili wawe wametoa heshima inayostahili na nadhani tunakubaliana wote kwamba leo waliovalia wanaongozwa na Mheshimiwa Ester Matiko. Nadhani Mheshimiwa Ester Matiko ndiyo amejiandaa zaidi kuliko wengine humu ndani. *(Makofi/ Kicheko)*

Haya ahsanteni sana. Waheshimiwa Wabunge sasa kama ilivyo ada wageni wetu wameleta futari kwa hiyo, wacha tukaipokee hiyo futari vizuri.

Baada ya kusema hayo, anaingia Mwenyekiti sasa kuendelea na ratiba. *(Makofi)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. David M. Kihenzile) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Katibu.

**NDG. ATHUMAN HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na majadiliano. Ninayo orodha ya wachangiaji hapa. Mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa ni Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua akifuatiwa na Mheshimiwa Bahati Khamis Kombo, wakati huo Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao anajiandaa.

Kabla hajaanza kuzungumza, kabla sijamwita Mheshimiwa Mbunge, naomba utulivu, tumsikilize Mheshimiwa Mbunge anapo kwenda kuchangia mchango wake. Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunijalia kusimama mbele ya Bunge lako tukufu siku ya leo ya Ijumaa ili niweze kuchangia bajeti ya Ofisi ya Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nitangulize shukrani za dhati sana kwako wewe. Pili, naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa ambayo anaifanya kwa Watanzania ya kuwaletea maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningependa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, dada yetu Mhagama, kwa kazi kubwa na Naibu Waziri, hali kadhalika Katibu Mkuu na watumishi wote wa Ofisi hii, kwa sababu ofisi hii ndiyo jicho na tegemeo la watumishi wote wa Tanzania, wanafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, ningependa kujielekeza kwenye maeneo ambayo ni kama ushauri. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri katika maeneo mbalimbali alijitokeza na katika hotuba yake amezungumzia kwamba kuna umuhimu wa kufanya ukaguzi au *auditing* ya watumishi. Ni ukweli usiopingika kwamba hitaji la watumishi katika maeneo mbalimbali nchini ni kubwa sana, lakini ni ukweli pia usiopingika kwamba watumishi hawa kwa hakika bado hawajawekwa vizuri, kwa sababu kuna maeneo ambayo wapo watumishi wengi ukilinganisha na maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajenga vituo vya afya, tunajenga shule za sekondari, tunajenga shule shikizi na zote hizi zinahitaji watumishi. Bila kufanya *auditing* ya kutosha, itafikia wakati haya majengo yote yatakuwa kama ni *white elephant.* Kwa hiyo, jambo la kwanza kabla hatujafikiria kwenda kwenye kuongeza watumishi kwa sababu lazima tukubali Wabunge wote kwamba bajeti yetu haiwezi kutosheleza kuweza kuwaajiri watanzania wote. Kwa hiyo, hatua ya kwanza ni kufanya *auditing* ya kutosha. Hebu leo tuchukulie mfano kuna Maafisa Ugani Kinondoni au Ilala wanafanya kazi gani? Wakati katika majimbo ya vijijini hakuna Afisa Ugani. Kwa hiyo nimwombe Mheshimiwa Waziri jambo hili lina umuhimu mkubwa sana sana kufanya *auditing* na *auditing* ndiyo itakayosaidia kuhakikisha kwamba watumishi hawa wanaenda kutatua changamoto ya ajira kwenye maeneo yetu huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, naomba nizungumzie suala la kukaimu. Suala la kukaimu imekuwa ni changamoto kubwa sana. Kwenye vikao vyetu unakuta Kaimu Mkurugenzi, Kaimu Mtendaji, kwa nini iwe hivyo? Kuna

kitu kinaitwa Tange katika utumishi wa Serikali. Tange ndiyo inayoonyesha *seniority* ya watumishi ameanza kazi lini, ana elimu gani, tange hii haifanyi kazi? Hii ndiyo ambayo inaenda kutatua changamoto ya *promotion.* Unapomweka mtumishi kwenye nafasi ya kukaimu miezi sita, mwaka mmoja humtendei haki hata mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii sisi ambao tuliofanya kazi Serikalini miaka ya nyuma huko, kulikuwa na utaratibu nadhani utaratibu huu bado unaendelea kufanya kazi, kitu kinaitwa *succession plan.* Leo Katibu Mkuu anapokaribia kustaafu anajua yupo Naibu Katibu Mkuu, anajua yupo Mkurugenzi watu hawa wanaijua taasisi vizuri, kwa nini uende ukamkaimishe mtu kutoka eneo lingine wakati *institution memory* ya taasisi hiyo wapo watu wanayoielewa. Kwa kiasi kikubwa hii inadhoofisha utendaji wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba turudi kwenye historia, turudi kwenye utaratibu, kwa sababu mtu kafanya kazi miaka 20 au 25 unaenda kumtoa mtu eneo lingine hata kuandika dokezo hawezi, hili jambo halina afya hata kidogo katika utendaji wa Serikali. Nakuomba Mheshimiwa Waziri, twende turudi kwenye utaratibu huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, wapo watu mnapokuwa mnawateua kwenye baadhi ya mashirika wanawaondoa watumishi, wanaondoa watumishi takribani 30 mpaka 40 halafu analeta tena kibali cha kuomba kuajiri watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, hawa watu wanaoteuliwa na Mheshimiwa Rais wanapokuwa wanaondoa watumishi kuwapeleka maeneo mbalimbali, asitoe kibali cha kuajiri tena kwa sababu watumishi wale wengine ni *very senior,* hili jambo halina afya hata kidogo na hili jambo Mheshimiwa Waziri kwa kweli....

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge nimeona umesimama.

**T A A R I F A**

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti,...

**MWENYEKITI:** Ni kanuni gani Mheshimiwa.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, 77(1) nataka kumpa taarifa mzungumzaji kwamba wapo wanaokaimu zaidi ya miaka miwili, mitatu mpaka minne na kinachotokea ni kwamba anakuja kuletwa mtu mwingine kuthibitishwa kuwa Mkuu wa ile Idara. Kwa hiyo wanawaacha hawa watu wakiwa na magonjwa yasiyoambukiza ikiwemo sonona, *pressure* na magonjwa mengine. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kigua unapokea taarifa ya Mheshimiwa Amandus.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru na nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge anachozungumza ni sahihi na jambo hili halitoi *motivation* kwa watumishi wetu...

**MWENYEKITI:** Unapokea taarifa.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa.

**MWENYEKITI:** Ahsante, endelea.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kusema kwamba, dhana hii kwa kweli si dhana nzuri, tuendelee kuwaamini watumishi wetu, watumishi ambao wanafanya kazi kwa weledi mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine katika eneo langu la Jimbo la Kilindi, wapo watendaji ambao ni darasa la saba ambao wamefanya takribani miaka 20 sasa hivi, lakini watumishi hawa wapo baadhi yao ambao wamestaafu lakini

hawajapata *pension* kwa sababu wamekosa sifa. Sasa fikiria Mtanzania huyu ambaye ulimwambia afanye kazi za utendaji wa kijiji na hivi ninavyozungumza ni kwamba watumishi hawa tayari Mkurugenzi wa Halmashauri wa Jimbo la Kilindi alikwishaleta barua Ofisi ya Rais, Utumishi miezi sita hawajatoa majibu, wengine wanakaribia kustaafu hawapati *pension,* tunatoa ujumbe gani kwa Watanzania? Naomba sana Mheshimiwa Waziri jambo hili liweze kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, tuangalie namna ya kuwapa *motivation* watumishi wetu, *motivation* siyo cheo tu au *motivation* siyo fedha tu, hata wakati mwingine mtumishi anapofanya vizuri unamwandikia barua ya *reward* ya kumshukuru kwamba kafanya kazi vizuri hiyo ni njia moja ya *kum-reward*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba niunge mkono hoja hii. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua kwa mchango wako. Sasa namwita Mheshimiwa Bahati Khamis Kombo, atafuatiwa na Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao, wakati huo Mheshimiwa Dorothy Kilave anajiandaa.

Mheshimiwa Bahati Hamis Kombo hayupo, kwa hiyo namwita Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao, wakati huo Mheshimiwa Dorothy Kilave pamoja na Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, wanajiandaa.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu katika Wizara ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa dada yangu Mheshimiwa Mhagama kupata uteuzi huu katika Ofisi hiyo, lakini pia mdogo wangu Ndejembi kupata nafasi hiyo nina imani wanakuja kufanya kazi kwa weledi kwa ajili ya kuwasaidia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nimpe ushauri Mheshimiwa dada yangu Mhagama katika jambo la kwanza; namwomba sana atengeneze *clinic* za kusikiliza matatizo ya wastaafu katika nchi hii, atengeneze Makamishina Wasaidizi waende katika mikoa, wazee wastaafu wanapata shida sana, wanatembea na mafaili, mtu anakwenda kustaafu ana mwaka mmoja hajalipwa mafao yake. Sasa hili ni tatizo kubwa sana. Serikali inapata dhambi bila kujua tuna shangaa mvua hainyeshi, kwa sababu kuna watu wamedhulumika haki zao, hizo zinaitwa dhambi baridi. Kwa hiyo, wawatendee haki hawa wastaafu, mtu ameajiriwa, amefanya kazi Serikali miaka 40, halafu bado unamwomba akulete *salary slip* ya kwanza aliyoajiriwa nayo, akuletee barua ya uteuzi, ana miaka 40 ameitunzaje hiyo kitu. Sasa hii ni hatari kubwa sana, hizi dhambi hebu waziache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, akiweka makamishna wakasikiliza, wanatoka katika wilaya anakuja, kwa mfano, akitoka Sengerema katika Jimbo langu anakwenda Mwanza nauli Sh.3,000 anapeleka hoja zake pale, anasikilizwa, anarudi na wale makamishna waje pia katika Makao Makuu ya Wilaya wanasikiliza kesi za wastaafu. Kwangu kuna askari mmoja ana miaka 40 amefanya kazi Serikalini halafu amekosa pesa za kumsafirisha kurumrudisha kwao, hazipo. Sasa hii ni tatizo kubwa sana, ametumikia kwa uweledi na kwa uaminifu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, Mheshimiwa Waziri ni suala la hawa watumishi ambao ni Makatibu Tarafa na *DAS.* Sasa ifikie katika nchi hii tubadilishe huu Muundo wa Utumishi hawa wapo kwa Mheshimiwa Waziri kwenye utumishi lakini asilimia 98 wanafanya kazi TAMISEMI. Hebu waangalie huu muundo haujakaa vizuri, wanaishi kwa shida, wanafanya kazi, ni watumishi wa Wizara ya Utumishi, lakini wakati huo wanafanya kazi za TAMISEMI, wakiamka asubuhi ni kazi za TAMISEMI, lakini mwajiri wao ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais. Sasa hili ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia bajeti zao, unakuta Katibu Tarafa ana Kata 13, hana pesa za madaraka, lakini

waliopo chini yake Mkuu wa Shule, sijui nani, Waratibu, Watendaji wa Kata, wote wana fedha za madaraka, Katibu Tarafa hana, hana Ofisi Katibu Tarafa na hao Makatibu Tarafa wanahitaji wasaidizi, lazima wapate Makatibu Muhtasi wale wa kuwachapia barua zao, lakini wawe na matarishi wa kupeleka zile barua pia, Wahudumu wa Ofisi, sasa hao Makatibu Tarafa wanakaa kule kama nani, lakini wanafanya kazi kubwa sana za kumsaidia Mheshimiwa Rais, wao ndiyo wa kwanza kupata taarifa, wanapeleka kwa Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Wilaya anapeleka kwa Mkuu wa Mkoa, inafika sasa waheshimike hao Makatibu Tarafa. Makatibu hao hawana usafiri na kama wana usafiri hawana mafuta. Kwa hiyo, Mkurugenzi hawajibiki kumpa mafuta yule Katibu Tarafa, sasa hili ni jambo ambalo liangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa ma-*DAS* wetu sisi pia wanaishi kwa hisani ya Mkurugenzi wakati yeye *DAS* ndiyo anatakiwa akamsimamie Mkurugenzi katika utendaji wake wa kazi. Hili naomba Mheshimiwa Waziri aliangalie na kwake sina mashaka yoyote, hili atafanikiwa tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la kupata mafunzo Wakurugenzi wanaitwa sana, wao ndiyo watendaji, kwa miezi mitatu anaweza akaja Dodoma mara sita, lakini *DAS* ambaye ndiyo msimamizi wa shughuli zote za wilaya kupata mafunzo Mungu nihurumie sijui wanakuja lini kupata mafunzo, sasa hili ni tatizo. Akiitwa Mkurugenzi kupata mafunzo basi na *DAS* aitwe, kwa sababu ndiyo mtendaji wa shughuli za kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la pili ambalo nataka nizungumze na Mheshimiwa Waziri katika kukushauri, ni suala la *TASAF*, *TASAF* imekuwa ni mtihani mkubwa katika nchi hii. Waheshimiwa Wabunge wote anaowaona hapa katika majimbo yao wana malalamiko ya *TASAF*. Kwa kuwa yeye ni Waziri na ana Naibu Waziri basi mmoja ashughulike na kutembea nchi nzima kuona matatizo ya hawa wazee wetu wanaopata misaada hii ya *TASAF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu siyo mzuri unaambiwa kwamba wazee wanalipwa kwa mtandao, mzee hajui kusoma na kuandika, halafu leo alipwe kwa kutumia mtandao, pesa ya swadaka tena inakwenda kudhulumiwa umeshaona wapi. Serikali inatoa msaada na ule msaada unakwenda kuibwa tena. Sasa hili jambo la *TASAF* liangaliwe, hawa wazee wetu kwa sababu tayari tumeshawaweka katika huo mfumo.

Vilevile wanaokwenda kupewa hizi pesa za *TASAF* kuna wengine wana nguvu, lakini ni ndugu wa mtu Fulani, hilo ni tatizo na unaambiwa kwamba kwa sababu labda ni balozi wa CCM, hana sifa kwa sababu anafanya kazi kama balozi wa CCM au sijui balozi wa chama gani? Haiwezekani kwa sababu kile ni cheo ambacho anacho hakina mshahara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la watumishi nimesikia humu Wabunge wanalalamika kwamba watumishi wa kike wanakuwa hawakai katika maeneo yao, hapa natoa tu ushauri kwamba, wazungumze na watu wa Ustawi wa Jamii waliopo kule katika wilaya, lakini nataka nimshauri pia Waziri atuambie na sisi Wabunge kule waache malalamiko haya kwa sababu ukisikia mtumishi anahama kwamba eti hakuna huduma muhimu hasa hawa mabinti wa kike wanaokwenda katika maeneo kama Walimu, Manesi na watu wengine kwamba hakuna huduma muhimu, siyo huduma hizo ni huduma za kifamilia, waolewe kule tuwaambie watu wetu waoe. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakwenda kufanya mkutano kwenye kata anayelalamika, Diwani analalamika Mheshimiwa Mbunge wanakuja watumishi wanaondoka, analalamika Mwenyekiti wa Kijiji, sasa unamwambia mbona ninyi mna tatizo...

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya taarifa.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naheshimu mchango wa kaka yangu Tabasamu, mabinti au wafanyakazi wa kike hawahami kwa hicho anachokisema, wengi wanapata shida mazingira magumu ya kazi ikiwepo nyumba na gharama za usafiri kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine, halipo suala la uchumba au kuolewa hapa. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tabasamu, unapokea taarifa?

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei taarifa hii, kwa sababu ninachotaka kukwambia, akisikia kwamba mazingira magumu, ni haya ya kifamilia. Mwanamke akipata hayo, hawezi kukimbia wala kuondoka kwa sababu ya nauli. Kwa hiyo, ushauri wangu, hawa wananchi huko kwenye Majimbo yetu wasichague wakaweka ukabila kwamba amekuja Mzaramo asiolewe na Msukuma, waoeni Wasukuma. Hii *massage* mimi ndio napeleka. Amekuja Mgogo, eti kwamba kaletwa hapa *Nurse* Mgogo, muoeni huyo Mgogo. Kwa sababu utafiti uliopo kwanza ni kwamba familia ya Walimu, watoto wa Walimu ndio wanaofanikiwa kuliko Walimu. Sasa leo mnakuja kulalamika kwamba Mheshimiwa Waziri… *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kuna Mheshimiwa Mbunge amesimama. Mheshimiwa Esther Matiko, umesimama kwa kanuni gani?

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, akija Mnzanzibari aolewe.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tabasam!

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Naam.

**T A A R I F A**

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa taarifa...

**MWENYEKITI:** Umesimama kwa kanuni gani?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kwa kanuni ya 77 kutoa taarifa.

**MWENYEKITI:** Endelea.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa Mheshimiwa Tabasam taarifa kwamba wanaoomba kuhama ni *both sides,* wanaume kwa wanawake, lakini anapojielekeza kwa wanawake, nimpe tu taarifa tu kwamba *nature* ya wanawake ilivyo anaweza akavumilia muda mrefu hayo anayoyasema bila kuathirika kuliko wanaume walivyo. Kwa hiyo, naomba ajenge hoja yake bila kudhalilisha jinsia nyingine. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata wakati Mheshimiwa Mbunge anazungumzia kuhusu kuhamisha watumishi, wengine unakuta tayari wako kwenye ndoa zao, wanataka wahame wawafuate wenzi wao. Kwa hiyo, ajenge hoja bila kuweka udhalilishaji wowote ule. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tabasam, unapokea taarifa hii aliyoisema Mheshimiwa Matiko?

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei hiyo hoja yake. Siipokei kabisa taarifa yake. Naomba ulinde muda wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata wanaume wanaokuja katika maeneo yetu vijijini, nao wanakosa watu wa kuwaoa kwa sababu tu kwamba amekuja Mmasai pale au amekuja Mzaramo kule Usukumani, na huyo Mzaramo aruhusiwe kuoa Msukuma, ndiyo haja yangu mimi. Watumishi watabaki kuwepo.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, naona hizi taarifa zinakula muda wangu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tabasam muda wako umekwisha. Nakuongezea dakika moja kwa ajili ya kuhitimisha hoja yako. Kaa chini Mheshimiwa Bulaya.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la watumishi, Serikali itaajiri watumishi 32,000. Ushauri wangu ni kwamba katika hao watumishi 32,000 tunayo Majiji yetu saba, wapewe mia tatu, mia tatu; na Makao Makuu ya Wilaya tupewe mia mbili mia mbili. Huko ndiyo tunafanya upekuzi, tutawajua watu wetu. Huu ndiyo Utaifa. Habari ya kuingia *online* halafu wanaenda kuajiriwa watu wa mkoa mmoja, hatukubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsanteni sana kwa mchango huo. *(Makofi)*

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Tabasam Mwagao. Nilimwita Mheshimiwa Dorothy Kilave, wakati huo Mheshimiwa Saashisha Mafuwe anajiandaa.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona nami niweze kuchangia baadhi ya masuala ya Utumishi na Utawala Bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, namshukuru sana Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, ambaye ameweza kunisimamisha mimi hapa pamoja na Wabunge wenzangu tukiwa salama.

Pia napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wangu, Mama Samia Suluhu kwa kazi nzuri ambayo anaifanya na hata sasa naamini kabisa huko aliko anatufanyia kazi na anatutendea haki kabisa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Temeke kwa madarasa tuliyopata, ni madarasa mengi sana na ukizingatia kwamba Temeke tunazaliana sana lakini ameweza kutupa madarasa mengi ambayo sasa mabinti pamoja na wavulana hakuna *second selection;* wote wamekwenda *Form One* kwa pamoja. Hivyo namshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Kicheko/ Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumepata zahanati kila Kata na tumebakiza Kata mbili ambazo ninaamini Kata hizi kwa bajeti inayokuja tutapata. Vifaa ambavyo vimekwenda katika hospitali zetu, kweli ni vya maana sana na sasa tunaringa sana Temeke kwa jinsi ambavyo tunapata tiba za uhakika kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa jinsi ambavyo amewapa uwezo Wizara hii ya Utumishi na Utawala Bora, mdogo wangu Mheshimiwa Jenista pamoja na mdogo wangu Mheshimiwa Deogratius, kwa kweli kazi mnaifanya na tunashukuru sana, hakika hata sisi tunajivunia ninyi kuwa hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwenda tu moja kwa moja kwenye Jimbo langu la Temeke, hasa wafanyakazi wa Bandari. Wafanyakazi wetu wa Bandari kipindi kile wengi mliweza kuwasimamisha kwa sababu walikuwa na elimu ya Darasa la Saba, wengine walikuwa wamegushi vitu vingine. Hata hivyo mliwapa namna ya kuweza kujifunza au kujiendeleza ili waweze kuajiriwa tena. Wako baadhi ambao tayari kwa kweli nawashukuru sana waliweza kujiendeleza na wakaweza kuajiriwa upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalo tatizo moja la wengine ambao hawakuweza kwenda kujiendeleza na sababu kubwa tunapoongea nao wanasema kwamba pesa ambazo walitamani mngekuwa mmewalipa kipindi kile walipoachishwa kazi wangeweza labda kuzitumia kujiendeleza, lakini mpaka sasa fedha zao hazijalipwa, wala hawajui lini watalipwa fedha hizo kwa sababu wametumikia

Bandari muda mrefu sana. Pia walitamani wao wenyewe kwamba kama kweli, basi walikosea na hawakuweza kujiendeleza, lakini wanaomba sana wapate hata mafao yao waweze kuondoka ndani ya mji waliokaa hasa kule Temeke. Wakati mwingine wanaomba hata kuajiriwa mahali pengine, lakini umri umewatupa mkono, hawawezi kuajiriwa tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana Wizara hii iwaangalie hawa watumishi wa Bandari ambao wako kama 196 hivi kama sikosei, muwaangalie upya waweze kupewa fedha zao ili waondoke ndani ya miji hii na kurudi vijijini kwao kuendelea na maisha mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyakazi hawa wameshatufata mara nyingi, hata mdogo wangu Mheshimiwa Jenista ameweza kuongea na baadhi na kuliangalia hili jambo, naamini sasa kwa kusema kwangu, nao watasikia, kwa kweli mtawatendea haki ili waweze kurudi makwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado niko Bandari; wako madereva ambao wanaendesha magari yale makubwa. Siyo madereva tu wa yale magari makubwa, lakini naamini hata madereva hawa ambao wanaotuendesha, labda wanaweza wakawa wanawaendesha hata nyie viongozi wangu mlioko hapo; mishahara yao wanalalamika sana kwamba ni midogo sana, kiasi kwamba hata leo unapompa Dereva gari lile V8 kwa thamani yake na kumwendesha labda Waziri Jenista aweze kufika salama mahali anapokwenda kufanya kazi, hakika anakuwa amebeba mzigo mzito sana. Kwanza gari lilivyo na thamani, lakini pia utu wa Mheshimiwa Waziri. Kwa hiyo, naomba sana mwangalie upya mishahara yao. Tuone kwamba kazi wanayoifanya inalingana kidogo na mshahara wanaoupata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa siyo mkaaji sana kwenye vijiwe lakini nimependa sana wakati wote kuwa ndani ya vijiwe vya wale madereva wa malori kule Bandari.

Madereva wetu wa malori, inawezekana ni malori ya Serikali lakini pia ni malori ya wanafanyabiashara binafsi lakini. Mara nyingi nakuwa napita katika vijiwe vile, nakaa, naongea nao na wale Madereva kwa kweli wanalalamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wao wanasema unampa gari ambalo labda ni *Scania* la thamani kubwa sana, ameweka mzigo wa thamani kubwa sana, anaondoka nao hapa Tanzania kwenda nao labda Rwanda, Burundi, lakini mshahaara wanaopokea ni mshahara mdogo sana ambao utaona mara nyingi malori yetu yanakaa njiani, yanapaki njiani kwa sababu fedha uliyompa aweze kuacha nyumbani, lakini pia hiyo hiyo fedha aweze kujikimu yeye mwenyewe. Kwa hiyo, unaona wengi wanalala ndani ya magari yao katika baadhi ya vituo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba pia muwaangalie. Labda mtengeneze namna ya kuweza kuwafikia wale wenye magari makubwa, wafanyabiashara wakubwa wenye magari yao hayo ili mwone mtawasaidiajie hawa, kwa sababu huu ndiyo utawala bora ambao mama anataka. Hawa madereva nao ni wafanyakazi, ndiyo utawala bora unaohitajika uwaone nao wako katika utawala bora unaoelekezwa katika nchi yetu ya Tanzania. Kwa hiyo, ninaamini mnasikia na mtakaa na waajiri wao muone wanafanyiwa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niseme kuhusiana na Walimu. Walimu wetu pia ni waajiriwa, nao wanatamani kuwa katika utawala bora. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa jinsi ambavyo ameweza kujenga madarasa mengi sana nchi nzima, lakini Walimu wetu wanapotoka madarasani kufundisha wanakosa ofisi za kukaa. Ofisi zao wanaweza kutumia labda darasa ndiyo wakafanya ofisi na mahitaji yao ni madawati yale ya shule ndiyo wanafanya meza zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua hili linakwenda kwa Waziri wa Elimu, lakini nilikuwa naanzia hapo kwa sababu ya utawala bora, kwamba sasa Walimu hawa wapate namna

ya kukaa vizuri ili wanapotoka madarasani, basi wanavyokuja kusahihisha madaftari yale, wakae mahali salama ili wanafunzi wetu ambao tumewawekea madarasa nao wahudumiwe vizuri. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Ni kengele ya pili.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Saashisha Mafuwe. Naomba wafuatao wajiandae. Mheshimiwa Samwel Hhayuma, Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso na Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye hoja hii. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya na uzima. Pia nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanyia Taifa hili. Tumeshuhudia miradi kemkemu imeingia ndani ya Wilaya ya Hai na nchi nzima. Kubwa ni hili la filamu ya *Royal Tour* ambayo imefanyika. Uzinduzi huu kule kwetu Hai tayari tumeshaanza kuona matunda. Watalii wameongezeka kwa kiwango kikubwa sana. Kwa hiyo, tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza Mheshimiwa Waziri, dada yangu Mheshimiwa Jenista Mhagama na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya pamoja na Katibu Mkuu, Dkt. Ndumbaro na watumishi wote kwa ujumla. Mheshimiwa Waziri, kule Hai wanakuita wewe ni mtu bingwa sana. Wanakuita mtu bingwa kwa sababu pale Hai Rundugai tulikuwa na chuo cha ufundi, kilijengwa miaka 11 kikatelekezwa pale. Nilipokuja kwako nikakuomba,

umetuletea fedha na kile Chuo cha Rundugai kinajengwa sasa hivi. *(Makofi)*

Vilevile wewe ni mtu bingwa kwa sababu Kata ya Bondeni kulikuwa hakuna kituo cha afya, wala zahanati. Kupitia *TASAF* umetuletea fedha pale, tunaenda kujenga zahanati pamoja na vifaa tiba. Nakushukuru sana. Hizi ni sambamba na kumshukuru Mkurugenzi wetu wa *TASAF* kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya USEMI, tumetembelea Zanzibar, tumetembelea Tanzania Bara huku, tumeona ufanisi *(value for money)* kwenye miradi. Nazungumza kwenye eneo la miradi, sijazungumza kwenye ile ruzuku wanayotoa kwa wananchi. Kwenye eneo la miradi kwa kweli wanafanya vizuri sana. Kama kuna eneo la kwenda kujifunza, TAMISEMI wanatakiwa waende wajifunze hapa kuona namna ambavyo miradi hii imekuwa sahihi. Hayo makofi unayoyasikia ni ya Wajumbe wenzangu wa USEMI tumeona miradi inavyotekelezwa vizuri na *TASAF*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, naomba niende moja kwa moja kwenye kuchangia hoja yetu. Nianze kwa kazi kubwa ambayo Mei Mosi watumishi wa Umma nchini wanategemea kusikia jambo moja tu, ongezeko la mishahara. Naomba sana, ninafahamu hii ni ahadi ya Mheshimiwa Rais mwenyewe, lakini nawe Waziri mfanye mfanyavyo, Mei Mosi hii watumishi waongezewe mishahara pamoja na kupandisha kima cha chini. Sababu za kuwaongezea mishahara, wanafanya kazi nzuri. Kwa hiyo, naomba sana hilo kwa kweli mwaka huu tujitahidi ili kazi iweze kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ningependa kushauri kuhusu Muundo wa Utumishi wa Umma wa Mwaka 2002. Nadhani kuna haja ya kufanya marekebisho kwenye maeneo kadhaa. Moja ya eneo hili ni zile sifa zinazomtaka mtumishi kupandishwa cheo. Wako watumishi ambao kwenye kada tofauti wanatakiwa waende shuleni, wakasome na wafaulu

ndipo wapandishwe cheo. Wakati kuna kada nyingine hicho kitu hakipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe mfano kwenye kada ya Maafisa Tarafa na Maafisa Tawala, nafahamu zipo na kada nyingine. Ukienda kwenye ule Muundo wa Utumishi wa Mwaka 2002, sifa za kumpandisha Afisa Tawala kutoka Daraja la Kwanza kuwa Mwandamizi, moja ya sifa inayotakiwa, anatakiwa akafanye mtihani unaitwa *Qualified Examination Test.* Ukisoma kwenye kanuni hii inasema, siyo tu kufanya mtihani, anafanya mtihani halafu afaulu ndiyo apandishwe daraja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa jambo hili kwanza linaleta tofauti kwenye Utumishi wa Umma. Kuna kada nyingine hazifanyi, kuna kada nyingine zinafanya. Pia hebu tupime umuhimu wa mitihani hii. Mimi nimefanya huu wa Maafisa Tawala, unaenda pale umetoka kazini; hili linawasumbua sana watumishi wa kada zile. Kwanza Serikali yenyewe haiwalipii kupata hicho kibali cha kwenda kufanya mitihani hii. Ni changamoto kubwa. Kwa hiyo, mtu anaacha kupanda daraja tu kwa sababu hakuruhusiwa kwenda. Pia hana hela ya kwenda kulipia mitihani ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kulipia na kujitahidi kufanya hivyo, akienda darasani, mtu huyo anaenda kusoma vitu vingine tofauti. Mtu amesoma *degree* ya kwanza, *degree* ya pili, halafu unampeleka katikati ya utumishi wake, ameshakaa zaidi ya miaka mitano huko mtaani, aende akafanye mitihani ambayo ni *administrative law,* anatakiwa kwenda kumeza madude pale, ajibu kwenye mtihani na afaulu, lakini lina-*embarrass* sana watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtumishi anaomba ruhusa kwa Mkuu wake wa Mkoa, anaaga kwamba anaenda kusoma, anafika kule bahati mbaya anafeli, akirudi huku mtaani hapakaliki. Wewe fikiria Afisa Tarafa anaenda kwenye mtihani huo, anaaga Kata zote zinajua bosi kaenda kwenye mtihani. Anaenda kule anakwama, anarudije kufanya kazi? Naomba, kama ni muhimu sana, basi kile kipengele cha

kufaulu kifutwe. Waende wafanye kama *refreshers course,* lakini kusiwe na kigezo kwamba lazima afaulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nihamie kwenye eneo lingine kuhusu madeni ya watumishi. Ni kweli Serikali inalipa, lakini bado watumishi wanadai. Mheshimiwa Naibu Waziri, wewe ulikuja kule Hai, uliona wale wamama wanatulilia na kila siku wanatuma jumbe, wanapiga simu. Wamelipwa kiwango kidogo sana. Naomba ifike mahali madeni ya watumishi hawa myamalize. Fanyeni kazi hii mhakikishe tunamaliza, siyo jambo zuri, mtu ameshatutumikia vizuri, amemaliza utumishi wake wa Umma, bado tunaendelea kumsumbua na madeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na pesa yao ya kustaafu, wanazungushwa mno wanapodai. Bahati nzuri na Spika naye amekuwa akilipigia kelele hili. Mtu anakuwa kwenye Utumishi wa Umma, Serikali imetumia fedha nyingi kufanya *data cleaning,* kwa hiyo tunaamini taarifa za watumishi ziko safi. Sasa anapostaafu unaenda kumdai taarifa, zipi tena wakati unazo wewe? Tayari tuna mifumo ambayo inachukua taarifa zao? Naomba hili na lenyewe tulishughulikie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia mafunzo elekezi; kwenye Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za Mwaka 2009 zinazungumza mtumishi kabla hajaingia kazini apewe mafunzo elekezi. Naomba Serikali itenge fedha ya kutosha kwenye eneo hili na kazi hii wapewe Chuo cha Utumishi wa Umma. Tunaenda kuwalaumu watumishi kwa sababu hatukuwafundisha vizuri na ni kinyume na sheria ili mtumishi aajiriwe, tuhakikishe lazima aende apate mafunzo ili aingie kazini akijua ni jambo gani anaenda kulifanya. Hili ni pamoja na viongozi wote, hata viongozi wa kuteuliwa ni muhimu sana wakapata haya ili kuepuka mambo ambayo hayafai ya kinidhamu yanaoendelea kwenye maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumze pia kuhusu *e-GA*. Nawapongeza sana *e-GA*. Tulienda kutembelea pale tukaona vijana wa Kitanzania

wamechukuliwa kutoka nchi mbalimbali walikokuwa wanasoma, wamekusanywa pale; na wale ambao bado wako mashuleni wanakuja kufanya mafunzo kwa vitendo pale. Kwa kweli hili jambo la kizalendo tunawapongeza sana. Bado naendelea kuwasisitiza, mifumo hii iunganishwe iseme, izungumze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii ukienda hapa Dodoma Jiji kulipia kiwanja chako, utakaa hapo masaa mawili au matatu; na wakati mwingine unaambiwa mtandao umeshuka, mtandao sijui umefanya vitu gani. Hii siyo sawa, watafute *backup* ya kudumu. Tumesema kwenye Kamati lakini narudia humu tena kwamba hii mifumo tunayoitengeneza tuwe na *backup* ya hakika. Serikali inapoteza pesa nyingi, lakini tunawasumbua wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe mwenyewe ukienda hapo Dodoma Jiji sasa hivi utakuta foleni ya kutosha pale. Jambo hili halifai, Serikali inakosa pesa kwa sababu ya kukosa *backup.* Kwa kukosa *backup* inatoa mianya ya watu kuweza kucheza na hii mifumo na kutumia fedha za Serikali. Mfano, mfumo wa *GoT-HoMIS* ukienda kule umeme ukizimika hawana backup ya kuweza... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso. Wakati huo Mheshimiwa Tadayo na Mheshimiwa Charles anajiandaa. Mheshimiwa Hhayuma na Mheshimiwa Tadayo wajiandae.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye hoja iliyopo mbele yetu. Nianze mchango wangu

katika kipengele cha kwanza kuhusiana na watumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba watumishi wa umma ndiyo injini ya nchi. Kama ambavyo tunatambua umuhimu wa injini katika magari yetu vivyo hivyo watumishi wa umma ni muhimu katika nchi hii kwa sababu wao ndiyo wapanga mambo yote na watekelezaji wa mambo yote hapa nchini na bila wao hakuna mafanikio yoyote ambayo sisi wanasiasa kwa namna moja au nyingine tunaweza kujivunia nayo. Hivyo basi, hawa watumishi wa umma wanatakiwa kwa umuhimu huo kujengewa mazingira yote muhimu na rafiki ya kuhakikisha kwamba wanapofanya kazi zao wanafanya kazi katika mazingira ambayo yanaleta matokeo tunayotarajia sisi wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni pamoja na watumishi wa umma wote ambao wana-qualify kupandishwa madaraja na vyeo Serikali haina budi kuhakikisha watumishi hawa kwa wakati madaraja yao na vyeo vyao vinapandishwa. Tumesikia kupitia taarifa ya Waziri amesema kati ya Julai 2021 na Machi 2022 watumishi laki 190,781 walipandishwa vyeo na madaraja, lakini hajatuambia kati ya mahitaji mangapi. Huwezi tu kusema umepandisha hawa lakini hamjatuambia ni wangapi wana-*qualify* kupandishwa madaraja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni vyema sana Waziri ukatuambia wanao-*qualify* ni wangapi na kwa awamu hii mmepandisha wangapi. Kwa hiyo tusijifiche kwa kutoa hizi takwimu tu zikaonekana ni nyingi kumbe uhitaji ni mkubwa sana huko kwa watumishi ambao wanapaswa kupandishwa vyeo na madaraja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, uhaba wa watumishi wa umma, kama ambavyo nimeanza kwa kuelezea umuhimu kama kuna uhaba wa watumishi wa umma *automatic* ufanisi wa mambo katika nchi hii hauwezi kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema, mahitaji halisi ya watumishi wa umma hapa nchini ni milioni 1,232,089 lakini waliopo mpaka sasa takwimu zinaonyesha ni mia 679,995 kuna upungufu wa laki 558,134 sasa tuna upungufu wa laki 558 *plus* lakini ajira zilizotangazwa juzi ni 32,000 katika kada zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuone tu kwamba bado tuna uhitaji mkubwa sana wa watumishi wa umma. Swali linakuja hivi ni kwanini ni kwamba labda hatuna watumishi ambao ni *qualified?* Lakini si kweli. Kwa mujibu wa taarifa ya *TCU* wanaohitimu Vyuo Vikuu, nina takwimu hapa za miaka mitatu; 2018, hiyo ni Vyuo Vikuu tu sijachukuwa takwimu za vyuo vya kati, Vyuo Vikuu wanamaliza na kuingia kwenye soko la ajira ni 49,154 kwa mwaka 2018, 2019 ni 51,000, 2020 elfu ni 48,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni kwamba, kama tuna upungufu ukitaka kusema hatuna wanao-*qualify* sio kweli kwa sababu tafiti za *TCU* itakuonesha ndivyo sivyo; na maana yake kwa miaka mitatu tunazalisha wahitimu laki 148,853. Kati ya hao laki 148,853 wenye *degree* ya kwanza ndio wengi zaidi ambapo kwa mwaka 2020 tu tunatoa walio na *degree* ya kwanza 34,168. Katika ya hao 1,468 ambao wanaongoza ni wale waliosoma *degree* ya kwanza ya *education,* ambao kwa mwaka 2020 tu tumewatoa wahitimu 14,644, wa *degree* tu ya kwanza ya *education*. Halafu ajira tulizozitangaza kwenye *specific* elimu kwa maana ya walimu wa sekondari na msingi ni elfu 9,800 *out of* tunaowazalisha wenye *first degree* ya *education* ambao ni 14,664.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni ukweli kwamba bado mahitaji ya ajira na upungufu uliopo ni lazima vioanishwe ili tuone kwamba tunapunguza upungufu uliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hili suala la ajira linakuwa kama zimamoto. Hivi kwa nini Serikali haina mpango maalum, kwamba katika mwaka mmoja wa Mwaka wa Fedha, inakuwepo kabisa, tuna mpango katika mwaka

mmoja wa fedha ni lazima tuajiri kiasi fulani, inabaki ni utashi wa awamu hiyo...

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa nchi.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani katika hili kabla sijapata muda wa kujibu baadaye nafikiri nilitolee taarifa, kwamba Serikali haiajiri kwa utashi. Bunge lako Tukufu ndilo linalotupitishia bajeti hapa kila mwaka, na katika kila bajeti ya mwaka tumekuwa tunasema tunaajiri idadi gani ya watumishi. Bajeti ya mwaka 2021/2022 ndiyo ajira hizi ambazo tutakamilisha na nyingine 32,000 ambazo tutazitoa na tumeshazitangaza, kati ya ajira elfu 44 *plus* zilikuwa zote kwenye bajeti na kamati ya USEM nadhani wao wanajuwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mwaka huu wa fedha unaokuja 2022/2023 tumeweka, nimesoma hapa kwenye bajeti, tumeweka bajeti ya watumishi 30,000. Kwa hiyo naomba niseme kwamba hatuajiri kwa utashi ama mtu anaamka tu, hapana. Kwa hiyo tusipotoshe. Serikali inaajiri, na kuna vigezo ambavyo vitafikia idadi hizo ambazo za watumishi tunaotakiwa kuajiri katika hilo naomba niliweke sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa taarifa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Paresso unapokea taarifa.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei hiyo taarifa. Hakuna ambaye hafahamu nchi hii awamu ya tano ajira zilizotolewa ni kidogo na wakati mwingine zilikuwa hazipo kabisa, huo ndio ukweli. Halafu tuliondoa watumishi hewa wengi na hatukuajiri, nani ambaye

hajui? Tunamshukuru leo Rais Samia angalau hizi japo ni chache lakini zimetoka na wananchi wameziona na wamezisikia, huo ndio ukweli. Kwa hiyo taarifa siipokea ukweli utabaki hivyo kama ulivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kushauri lazima kuwepo na mpango, kwamba Serikali kila mwaka ni lazima, kwa sababu unaangalia wahitimu tunaowatoa kwenye vyuo vikuu ni wengi, hao mwisho wa siku wanaenda. Kwa hiyo tuna wahitimu tunaowatoa kuna wanaostaafu lakini hatuajiri tunasubiri tu, tunaangalia hatuna mpango hatuna utaratibu hatuna chochote tunasubiri tufanye hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nilindie muda wangu mawaziri wana nafasi ya kujibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Paresso hebu keti kwanza Mheshimiwa Naibu Waziri hebu keti kwanza. Mheshimiwa Paresso hili Bunge linakutana kila mwaka kujadili bajeti, linapitisha ndiyo hoja ya Waziri pale. Kwa hiyo unapoenda kuajiri ili uajiri lazima u-*create* nafasi iwepo, iwe wazi utafute bajeti utafute fedha halafu unatangaza.

Kwa hiyo, hoja aliyoitoa Mheshimiwa Waziri tulidhani pengine imeeleweka vizuri. Ninakuruhusu kuendelea kuzungumza lakini *you take into consideration* la sivyo nitatumia mamlaka ya kiti changu.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, no mimi hiyo taarifa siipokei na huo ndio mchango wangu na hayo ndio maoni yangu mawaziri watapata nafasi ya kuchangia katika hayo.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendele kuchangia na muda wangu ulindwe.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nollo nimekuona taarifa

**TAARIFA**

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe tu taarifa mzungumzaji, kwamba kuajiri si kwamba ni jambo la kila wakati unalifanya unategemea na *national wages.* Kwa hiyo unaweza ukadhani kwamba Serikali inabana isiajiri; kuajiri inategemeana na *GDP* kuna *percentage* yake. Kwa hiyo unaweza kuona kwamba Serikali haitaki kuajiri zipo *economics* ambazo zinafanya kwamba na kuajiri uende kwa stahili hiyo *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Endelea Mheshimiwa Paresso ukumbuke muda wako unakaribia kwisha kwa hiyo uanze ku-*wind up (kelele)*

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba muda wangu ulindwe.

**MWENYEKITI:** Unapokea taarifa

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio hicho ninachotaka kusema kwamba hata anachoeleza Mheshimiwa Nollo haya yanayosemwa yawekwe kwenye mipango na watu wajue, kwamba *wage bill* ni kiasi gani *according to wage bill* tunaweza kuajiri kiasi gani huo ndio ukweli na ndicho ambacho tunatamani kukisikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikizungumzia suala la utawala bora. Utawala bora ni pamoja na kuhakikisha sheria kanuni mifumo na taratibu inafuatwa. Katika nchi hii watanzania wengi wapo wamekuwa *clustered* kwenye vijiji, na katika vijiji kuna taratibu ya kuendesha mikutano mikuu ya vijiji na kufanya maamuzi ya miradi mbalimbali ya maendeleo, ya mapato na matumizi na kila kitu. Sasa, kumeibuka utamaduni, kwamba mikutano mikuu ya vijiji siku hizi haifanyiki, mikutano mikuu ya vijiji kwa mujibu ya sheria kusoma mapato na matumizi haifanyiki, mipango mbalimbali ya miradi maendeleo katika vijiji haifanyiki; sasa, huu ndio utawala bora ambao tunapaswa kuusimamia na wananchi wakaulewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nchi hii kuna baadhi ya watendaji wa kata na vijiji na wenyeviti wa vijiji, baadhi si wote, wanageuka miunguwatu kwenye maeneo yao, wananchi hawawezi kuwahoji. Baadhi ya watendaji wa vijiji leo wanafanya majukumu ya kutengezea watu tuhuma, wao ni polisi wanakamata wao ni mahakama wanahukumu, wao wanapokea faini. Yaani wao ni *final* kwenye vijiji na kata zao. Hii haiwezi kukubalika, huu si utawala bora. Ni lazima sasa Serikali mkomeshe huu utamaduni unaotaka kujengeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona jana kwenye mitandao ya kijamii mwananchi mmoja amekatwa panga kwa sababu alikuwa anahoji mapato na matumizi kwenye Mkutano Mkuu wa Kijiji. Sasa ni haki ya mwananchi, ni lazima hao watu wajue kwamba mabosi wao ni wananchi wa Tanzania, wanaweza wakawahoji *as long I am-provoke* na kwamba havunji sheria hivyo ana wajibu wa kuhoji mapato na matumizi na wale wenye mamlaka kwenye vijiji lazima wahitishe mikutano kwa mujibu wa taratibu. Tunaomba hili lisimamiwe kwa dhati kabisa ili wananchi wafurahie kuwa Watanzania. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana nilimwita Mheshimiwa Samweli Xaday Hhayuma Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo wakati huo Mheshimiwa Salma Kikwete na Mheshimiwa Livingstone Lusinde wanajiandaa.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana Mwenyekiti kwa kunipa nafasi. Mimi nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayofanya lakini hasa kwa kuangalia maslahi ya watumishi na kwa kumteuwa Mheshimiwa Waziri kwenye nafasi ya kuwaangalia watumishi wa nchi hii. Watanzania wana imani naye watumishi wana imani naye na uthibitisho ni jinsi alivyopigiwa makofi hapa ndani wakati anaenda kusoma hotuba yake ya bajeti jana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia niwapongeze na wasaidizi wake Naibu Waziri, na watumishi wengine wizarani kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. Vilevile tuipongeze sana

Serikali yetu kwa kutoa ajira ya watumishi 32,000, hii itapunguza upungufu wa watumishi kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mheshimiwa Tabasamu aliongelea kidogo jambo la mazingira magumu ya watumishi kwenye baadhi ya maeneo yetu. Tuna maeneo nchi hii ukimpeleka mtumishi hakuna nyumba hata za kupanga, acha zile ambazo zimejengwa kwa ajili ya watumishi. Ninachoiomba Serikali yangu maeneo kama hayo watumishi hawa wapewe posho ya mazingira magumu ili watumishi waweze kubaki kwenye maeneo hayo ili wawe tofauti na wale ambao wako mijin. Wakipewa fedha kwa kuangalia mazingira magumu wanayoishi watumishi hawa watabaki kwenye mazingira hayo. Kuwe na tofauti kati ya wanaokaa mjini na wale ambao wanaenda kwenye mazingira ambako hata nyumba za kupanga hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye utumishi wa umma kumekuwa na changamoto mtumishi anapoenda kusoma. Kwanza Serikali haisomeshi watumishi wengi kwa sababu ya kibajeti, lakini watumishi hawa wanajilipia ada wenyewe hakisharudi kwenye eneo lake la kazi ile elimu yake aliyopata kutambuliwa kwa wakati inachukuwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wengine utakuta mtu ana nafasi, *either* Mkuu wa Idara au yawezekana ni Mwalimu Mkuu, akirudi kazini nafasi yake hiyo imeshachukuliwa na mtu mwingine, yeye atakaa benchi na wala hakuna *consideration* kwamba huyu amesoma. Ile elimu aliyopata badala ya kuhitumia ana kaa miaka mitatu yuko *bench* au yuko *frustrated.* Hatutumii watumishi wetu vizuri. Kwahiyo naomba eneo hili tuliangalie vizuri

Mheshimiwa Mwenyekiti, limeongelewa sana suala la mafunzo kazini. Kumekuwa na utamaduni tu kwamba walioko ngazi za juu kila siku wanatoa maelekezo. Sasa badala ya kuwa tuwe na utaratibu wakutoa tu maelekezo hasa sekta ya elimu tuwe na utaratibu wa kukaa na hao watumishi kufanya mafunzo kazini ya namna ya kuboresha utendaji wao. Si lazima mafunzo hayo yawe ya gharama kubwa lakini

yakatengenezwa mfumo wa angalau hata kwenye ngazi ya kata kila mwaka wanakuwa na mafunzo ya namna gani wanaweza wakaboresha utendaji wao wa kazi ili kuwapa motisha watumishi hao, kwamba wao wanafanya kazi lakini tunawaangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusu watumishi wetu wanaoelekea kustaafu. Unakuta mtumishi amepandishwa daraja lakini mshahara wake haanzi kulipwa kwa wakati, ule ambao ni wa daraja husika. Mtumishi huyo anastaafu tofauti ile haijawahi kulipwa, anaanza kudai sasa mafao yake na anakuta mafao hayo yamepunjwa sana. Mtumishi huyo atahangaika atazunguka kote ili kupata haki yake, nah apo inakuwa ni usumbufu mkubwa na sisi Wabunge tunapata changamoto kubwa sana kwenye eneo hilo. Naomba tuangalie na tutengeneze mifumo ambayo inawezesha kujua kwamba mtumishi huyu baada ya muda fulani atastaafu na hivyo taratibu zake zote ziandaliwe ili anapostaafu mishahara yake yote iwe imekuwa sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kumekuwa na changamoto ya kuwalipa mafao yao kwa wakati. Mtu amezoea kupokea mshahara labda tuseme laki tano kwa mwezi, anastaafu halafu anakuta mwezi wa kwanza hamna kitu, wa pili hamna kitu na hata mwezi wa tatu hamna kitu. Tunawatesha watumishi wetu wanaostaafu. Na hata malipo yale ya kila mwezi baada ya kustaafu hayaanzi kwa wakati. Kwa hiyo hili eneo tuliangalie kwa umakini mkubwa kwasababu tunawatesa watumishi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao watumishi ambao wamestaafu siku za nyuma, posho wanazolipwa au mafao yao ni madogo mno na kazi walizofanya ni sawasawa na watumishi ambao wanastaafu siku za hivi karibuni. Tuwaangalie, kwasababu fedha tunazowapa haziwasaidii kitu chochote kwa hali ya maisha iliyopo sasa. Wale wastaafu wetu ambao wamestaafu siku za nyuma tuwaangalie namna ya kuwaboreshea mafao yao ili nao waweze kuishi kama watu waliotumikia nchi yao kwa uhaminifu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kumekuwa na suala hili la uhakiki wa wastaafu. Uhakiki huu utakuwa unafanyika mara nyingi Makoa Makuu ya Mkoa ambako ni mbali. Mtu kwenda kuhakikiwa anaingia gharama kubwa ilhali malipo yenyewe anayolipwa ni kidogo. Kwa namna hii tunawatesa wastaafu wetu, wengine wameshaanza kuwa wazee. Sasa, tuwasaidie kwenye kuwahakiki maeneo karibu na wanakoishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi baada ya kusema hayo niendelee kupongeza, watumishi wa Tanzania wanayo matumaini makubwa, na mimi ninaamini Waziri wakati wa Mei Mosi watumishi watacheka ahsante sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante nilimwita Mheshimiwa Josefu Anania Tadayo.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kupata nafasi ya kuchangia hotuba hii ya bajeti ya Wizara ambayo mimi nasema ni wizara nyeti sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu tumeanza kuchangia jana mpaka leo imetolewa michango mingi yenye umahiri na weledi mkubwa sana hasa kwa upande wa masuala ya utumishi. Na katika michango hiyo pamoja na hotuba ya Mheshimiwa Waziri tumebaini jinsi ambavyo kazi kubwa imefanyika katika kurekebisha suala zima la utumishi wa umma na kuwajengea watumishi mazingira mazuri ya kazi na matumaini ya kuendelea kufanya kazi katika mazingira mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo katika hili nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake, kazi waliofanya ni kubwa na Watanzania wameiona. Lakini kipekee kabisa nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa sababu wizara hii iko chini ya ofisi yake, kwa hiyo haya yote yaliyofanyika yana m-*reflect* yeye mwenyewe, jinsi ambavyo amekuwa mtu wa kujali na jinsi ambavyo amekuwa mtu mwenye nia ya kuifikisha nchi yetu mahali pazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba nichangie upande wa utawala bora kwa sababu ni jambo ambalo ni *cross cutting,* linakwenda kila Wizara. Hawa watumishi tunaowazungumzia popote pale walipo wana wajibu wa kutumika kwa kuzingatia misingi ya utawala bora na hakuna taasisi wala idara yeyote ambayo inaweza ikafanya kazi nje ya mfumo wa utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili kwanza nitambue jinsi ambavyo tumefanya vizuri, na si kwa viwango vyetu sisi, tumesoma kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwamba tumepanda ngazi katika kiwango cha *Corruption Perception Index* na hata kwenye *Rule of Law Index* tumepanda. Sasa tathmini hizi ambazo zinafanywa na mashirika ya kimataifa yaani hakuna namna ya kusema kuna mtu amejipendelea hapo, zimefanyika kwa viwango vya kitaaluma na kitaalam, kwa hiyo tunastahili kuipongeza Serikali kwa hilo na pia sisi wenyewe kujivunia kwamba tunakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utawala bora katika nchi ambayo ina katiba iliyoandikwa *(written constitution)* unaanzia na kuishia kwenye utawala wa sheria; yaani utawala ambao kila mtu, ikiwa ni pamoja na dola yenyewe, inapaswa kutenda kazi zake kwa mujibu wa sheria na kwa kutii sheria, hakuna aliye juu ya sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia sheria si kila sheria ni sheria, kwamba hata zile za wakati wa Idi Amin anaamka kule kwake anasema leo weka watu hawa kwenye karandinga tukawatupe baharini nayo ni sheria hapana. Sheria inayozungumziwa katika utawala wa sheria ni ile sheria ambayo imetungwa na chombo halali kama sheria zetu ambazo zinatungwa na Bunge hili, na imetungwa kwa mfumo wa uwazi ambao inashirikisha hata wadau kupata maoni ya wadau na kadhalika kwa mfumo ambao ni shirikishi, na ni sheria ambayo inaweza kutumika kwa ajili na dhidi ya mtu yeyote yule hata dola yenyewe kama ambavyo nimekuwa nikizungumza; na pia ni sheria ambazo zinaendana na misingi ya haki za binadamu, ile misingi ya kimataifa; na katika hili bado tumefanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili bado tumefanya vizuri kwa nini nasema tumefanya vizuri. Mwaka 1984 *Bill of Rights* ule mkataba wa Haki za Binadamu uliingizwa katika Katiba yetu, baada ya hapo ikatokea kipindi karibu cha miaka 10 ambapo Idara mbalimbali zilianza kurekebisha Sheria zao ili ziendane na *Bill of Rights* na pale ambapo hawakufanya hivyo wananchi binafsi waliweza kufanya hivyo kupitia Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtakumbuka kesi kama ya Daudi Pete ambayo ilifanya marekebisho kwenye Sheria ya Dhamana, mtakumbuka Sheria ile ya *Government Proceedings Act* ambayo ilikuwa inakataza wananchi kuishitaki Serikali mpaka wapate kibali cha Waziri wa Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1992 kuna mtu mmoja ni Mwalimu anaitwa Peter Ng'omango alikwenda Mahakamani wakaifuta ile Sheria. Ilipofika mwaka 1994, Bunge hili likaona sasa tuwarahisishie zaidi wananchi kazi kwamba wanapotaka kurekebisha sheria siyo lazima waende wakaishambulie ile Sheria Mahakamani kwamba inakiuka Katiba, ikatungwa ile Sheria ya *Basic Rights and Duties Enforcement Act,* ambayo kwa mujibu ya Sheria ile ya Mwaka 1984 nafikiri ni Sheria Na. 33, mtu yeyote ambaye haki yake imenyimwa au anaona kwamba haki yake itanyimwa ana haki ya kwenda Mahakamani na akaipinga ile Sheria na ile Sheria ikafutwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sheria hii imetumika kurekebisha Sheria nyingi sana ambazo watu walikuwa wanaona zinawanyima haki na hata juzi juzi kesi ambayo bado nadhani iko kwenye mawazo ya watu ni kesi ya Ndugu Rebecca ambapo alikwenda Mahakamani kupinga vile vifungu vya Sheria ya Ndoa ambayo ilikuwa inaruhusu watoto wa kike kuolewa chini ya umri na ile sheria Mahakama ikaitamka kwamba inakiuka Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema ni kwamba Katiba yetu, Sheria zetu na mifumo yetu iko ambayo inatuwezesha kupata haki zetu kwa mujibu wa Katiba, lakini

tatizo linakuwa wapi? Tatizo ninakuwa uelewa tu ndiyo tatizo. Kwa hiyo, tunapopanga bajeti zetu na kuleta hapa Bungeni ni vizuri sana tukazingatia suala la *training* na kujenga uelewa kwa upande wa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya zile bajeti zinazopita kwenye Kamati yetu ya Katiba na Sheria kwa kweli tuling'ang'ana sana na walioleta bajeti kwamba jamani bajeti ya *training* ni ndogo, bajeti ya mafunzo ni ndogo mambo ya kujenga uelewa, wakati ule tunaambiwa ni ukomo wa bajeti, nafikiri sasa ukakomoe maeneo mengine tusikomoe suala la *training* ambalo kwa kweli ni muhimu sana. Unaweza ukawa na sheria nzuri, unaweza ukawa na Katiba nzuri lakini kama watu hawaifahamu na hawaifahamu jinsi ya kuitumia kufikia haki zao inakuwa unafanya kazi bure, unakuwa na karatasi za bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Waheshimiwa Wabunge ni vizuri tukajengewa uwezo kwenye maeneo ya kimkakati ili tunapokwenda kwenye mikutano ya hadhara tuweze kuwaelimisha watu wetu ili waweze kujua jinsi ya kufikia haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mambo madogo mdogo ambayo yanawakerakera wananchi ambayo kama tu mafunzo yangekuwa yanafanyika kwa wananchi wenyewe na kwa wale Watendaji tusingekuwa na tatizo. Kwa mfano, mtu anakwenda anataka dhamana ana kitambulisho cha Taifa cha *NIDA* ambacho kimepatikana kwa mifumo ya hali ya juu lakini anaambiwa kalete barua ya Mtendaji. Sasa anakwenda kufuata barua ya Mtendaji anakuta Mtendaji siku hiyo kafiwa kaenda mazikoni, anarudi anakuta *OCS* ameshaondoka, mtu analala ndani bila sababu wakati kitambulisho cha Taifa kimejitosheleza kufanya hiyo kazi. Wengine wanaofanya hivyo ni kuelewa awaelewi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la dhamana unaambiwa kalete barua ya mtu ambaye ameajiriwa Serikalini. Sasa upo pale umekamatwa, uende ukatafute

mfanyakazi wa Serikali, *by the time* unarudi muda umeisha mtu anakosa dhamana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Jimbo langu pale kuna jambo moja lilitokea hapo ni la kuchekesha tu ambalo ni lakusikitisha kwa kweli, kwenye Kata ambazo zilishambuliwa na Tembo, Kata ambazo zina matatizo ya Tembo Kata ya Kwakoa, Kigoligoli na Toloa walikwenda watu kulipwa kifuta jasho, sasa anakuja mtu anakitambulisho kimeandikwa kwa mfano Zaituni Athumani Mbarouk, sasa lile jina lilivyochapwa huko Wizarani kuletwa kwake limeandikwa Zaituni Athumani Mbaraka anaambiwa sasa nenda kaape Mahakamni kubadilisha hii Mbarouk na Mbaraka ili upate hela yako, wanakwenda kuapa Mahakamani anarudi tayari watu wameshaondoka na mpaka leo hawajarudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo mengine ni uelewa tu wa hawa tu ambao kwa kweli kama wangepewa mafunzo, wakajengewa uwezo, nadhani kwamba tusingefika hapa, haya matatizo madogo madogo tungeyaondoa, tunaweza tukawekeza kwenye haya makubwa tuka-*shine* tukapata na sifa, lakini haya madogo ni muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilimuita Dkt. Pius Stephen Chaya, Mheshimiwa Salma Kikwete na Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde ajiandae.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichukue nafasi hii nikushukuru sana kwa kunipa nafasi kuchangia kwenye Wizara nyeti, kipekee nimshukuru sana Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi ambayo anaendelea kuifanya hususan katika ku-*promote* utalii wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Waziri wetu Mheshimiwa Jenista pamoja na ndugu yao Deo Ndejembi kwa Wizara ambayo wamepewa, hatuna mashaka kabisa

na hawa wawili, Mheshimiwa Jenista tunamfahamu, tunafahamu utendaji wako tunaamini kabisa upele umepata mkunaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hoja kubwa mbili, hoja ya kwanza nataka nitoe uhalisia wa upungufu wa watumishi na nita-*site* mfano wa Manyoni DC, hoja ya pili vilevile nitoe ushauri kwa Serikali juu ya maboresho ya ile *program* yetu ya ya Maboresho ya Utumishi wa Umma *(Public Services Reform Program)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wenzangu wote wamesema kwamba tunao upungufu mkubwa sana wa Watumishi wa Umma kwenye kada mbalimbali. Nitatolea mfano kwenye Halmashauri yangu ya Manyoni, kwa upande wa Manyoni upande wa walimu wa shule za msingi, tunao upungufu wa zaidi ya asilimia 60 hadi sasa na ukizingatia tunazo shule 20 mpya za UVIKO ambazo zimejengwa nadhani hili Waziri wa TAMISEMI atakuwa amelichukua, kwamba kuna shule mpya ambazo Mama Samia ametujengea mpya ambazo tunategemea mwakani zianze kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Manyoni upande wa shule za msingi tuna zaidi ya upungufu wa asilimia 60 wa walimu wa shule za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa Sekondari tuna upungufu wa zaidi ya asilimia 33 wa Walimu wa Shule za Sekondari. Jambo la kusikitisha ajira zilizotoka mwaka juzi au mwaka jana, tulipata walimu 11 tu ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni, nadhani utaona sasa tuna upungufu wa zaidi ya Walimu 600 lakini *rate* ya kuajiri ni Walimu 11.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tuna *very serious problem* upande wa watendaji wa vijiji kati ya vijiji 58 nilivyonavyo ni vijiji 39 ambayo ni sawa na asilimia 67 vina Watendaji wa Vijiji. Tuna Vijiji 19 ambavyo vimekaa zaidi ya miezi Sita ambayo ni sawa sawa asilimia 33 havina Watendaji wa Vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii maana yake ni nini? Mama Samia amepeleka fedha nyingi sana za miradi vijijini, tunategemea hawa Watendaji wa Vijiji ndiyo wasimamie hii miradi, hatuna watendaji wa vijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa afya tuna upungufu zaidi ya asilimia 60 ya watumishi wa afya, *(Human Resource for Health)*, hili ni tatizo kubwa na waliopo ni kama asilimia 38.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu upande wa utumishi ni kwanza, nadhani tunahitaji kuhuhisha mfumo wa ajira za Watendaji wa Vijiji. Huko nyuma Watendaji wa Vijiji wengi walikuwa wanatoka kwenye maeneo husika sasa hivi tunamchukua Mtendaji wa Vijiji Kigoma anakwenda kufanya kazi Bagamoyo, ndiyo ndugu yangu Mheshimiwa Tabasamu ameeleza pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeshauri Mheshimiwa Waziri uangalie upya, kama inawezekana Watendaji wa Vijiji watoke kwenye maeneo ya karibu na ile halmashauri husika. Hii itapunguza hulka ya Watendaji wa Kijiji kuhama pia *tuta-improve retention*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kuhusu utoaji wa vibali mbadala *replacement*. Wakati Waziri anakuja *ku-windup* nitapenda kujua *standard operating procedure* ukomo, hivi kwa mfano, samahani labda mtumishi amefariki *replacement* yake inatakiwa ichukue muda gani *policy maxmum* ni vizuri tukalijua hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ni kuhusu ile *program* yetu ya kuboresha utumishi wa umma. Tulikuwa na *program* nzuri sana ilianza 2002 awamu ya kwanza, ikaenda 2007 awamu ya pili, kutoka 2007 ikenda 2012 ikaisha, kuna maboresho makubwa sana yalifanyika katika utumishi wa umma. Swali langu la msingi ile *program* tangu ife nini mpango wa Serikali kuja na uendelevu wa *Interventions* ambazo zilifanywa na *program* ya kwanza na ya pili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wadau mbalimbali ambao wamekuwa na *interest* kubwa sana ya kusaidia Serikali, wakiwemo *World Bank*, *USAID, GIZ, EU* na wengine, ni nini mkakakati wa Serikali wa kuwa-*engaged* hawa wadau ili tuje na a *new program* ambayo itasaidia kuendeleza *intervention* za *program one* na *program two*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni maeneo nyeti sana, tumeona ripoti ya *CAG* bado kunachangomoto nyingi sana kwenye utumishi wa umma. Suala la *accountability* lakini kuna suala la *ethical issues,* suala la utendaji, suala la *performance management,* haya mambo yanahitaji kuboreshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila siku kuna uteuzi unaendelea, kwenye upande wa *leadership* viongozi wanatakiwa wanolewe, hii *program* ndiyo itakuwa muarobaini wa kuboresha utumishi wetu na utumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya nakushukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Salma Kikwete wakati huo Mheshimiwa Lusinde anajiandaa.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia Wizara hii ambayo ni Wizara muhimu sana katika ustawi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda nimpongeze Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa na nzuri ambayo anaifanya ndani ya Taifa letu na nje ya mipaka yake. Leo hii dunia yote inatambua kwamba Rais wa Tanzania yupo na anautangaza utalii wa nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, niipongeze Wizara ya Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora ambayo inaongozwa na Dada yetu mpendwa Mheshimiwa

Jenista Mhagama kwa kweli anafanyakazi nzuri, kazi hii anayoifanya si kwamba ameanzia hapa bali ameanzia kwenye maeneo yote ambayo alikabidhiwa dhamana ya kushughulikia shughuli hizo. Hongera sana Mheshimiwa Mama Jenista Mhagama, endelea kufanya hivyo Taifa linakutegema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo napenda nichangie kwenye eneo la watumishi tu. Eneo hili ni eneo muhimu. Kwanza, naungana na wenzangu wote, Waheshimiwa wote ambao wamechangia eneo hili kwa kuona na kutambua kwamba mtumishi ana haki yake ya msingi amefanya kazi kwa wakati wake, na anapostaafu anatakiwa atambuliwe kwamba alichangia Taifa hili katika eneo moja au jingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha huo leo hii kwanza mimi namshukuru Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kwa nini namshukuru kwa sababu yeye aliniteua kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia vile viti 10. Kutokana na hilo leo hii naweza kusimama hapa na kuzieleza changamoto, hapa nataka nieleze wastaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wastaafu hawa wapo katika eneo maalum ambao ni Wenza wa Viongozi. Wake wa Marais, Wake wa Mawaziri Wakuu na wake wa Makamu wa Rais. Ninayaeleza haya kwa sababu na mimi nataka niseme nilikuwa ni Mke wa Rais wa Awamu wa Nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu na suala la kustaafu mara Rais anapochaguliwa ili aweze kushika kijiti na kuongoza Taifa. Mke wa Rais anatakiwa astaafu asiendelee kufanyakazi, hatakaa kana kwamba alikuwa ni mtumishi wa umma, unatakiwa kuanzia wakati ule ustaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mfano mmojawapo nilitakiwa niache kazi yangu ya Ualimu niendelee na shughuli nyingine. Sasa kwa muktadha huu kuacha kazi siyo jambo

baya lakini kinachotakiwa kifanyike ajue huyu Mke wa Rais au Mke wa Makamu au Mke wa Waziri Mkuu stahiki zake zipo wapi? Stahiki zake ni nini mara baada ya kustaafu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kama akistaafu ni lazima huyu Mke wa Rais basi apate mafao yake yale mapema au haraka kadri inavyowezekana. Sasa itokee Mke Rais huyu, kama huwiwi ina maana kwamba kuanzia siku ile inabidi ukae nyumbani uendelee na shughuli za nyumbani wakati wewe ulikuwa aidha mtalaam kwenye eneo husika, kwa maana hiyo utaalam wako wote ule unatoweka na inakuwa basi, ukiwiwa sana ndiyo unaweza ukasema hebu nianzishe *NGO. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ukianzisha *NGO* ile hakuna mtu anayeku-*support,* ni wewe mwenyewe binafsi uhangaike kona zote, kuhakikisha kwamba unapata rasilimali ili uweze kuendesha ile *NGO*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu au ushauri wangu, tengenezeni utaratibu maalum wa kisheria kwamba, huyu Mke wa Rais mara au mwenza kwa mfano leo si mke wa Rais leo ni mwenza Mama leo ndiyo Rais, Baba ndiyo mwenza wake huyu Baba ina maana anaachishwa kazi leo na akiachishwa kazi anafanya nini? Tengenezeni yale mazingira mazuri ili tunapomaliza ule muda tujue tuna kitu gani ambacho tunatakiwa tukifanye.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Ofisi ya Rais, Utawala Bora ni imani yangu kwamba, tutatengeneza utaratibu au sheria inayomuhusu mke wa Rais au wenza nini baada ya hapo kiendelee kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo muhimu sana siyo kwangu mimi bali ni kwa vizazi vijavyo na vijavyo kujua stahiki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ahsante sana Mheshimiwa Mama Jenista Mhagama kwa kazi kubwa na

nzuri unayoifanya Mwenyezi Mungu akubariki, Mwenyezi Mungu ambariki Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kazi iendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia 100. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Salma Kikwete kwa mchango uliojikita kwenye hoja moja na imeelewa vizuri sana, tunakushukuru sana Mheshimiwa.

Waheshimiwa Wabunge, nilimuita Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde, wakati huo Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni, Mheshimiwa Constantine John Kanyasu na Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga ajindae.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hotuba ya Mheshimiwa Waziri Jenista Mhagama kutoka Wizara ya Utumishi na ambao kwa kweli wapo chini ya Mheshimiwa Rais mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza na *TASAF* niigusie kidogo ili baadae sabufa ikifunguka nisije nikasahau jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Waziri nilimuomba watu wa *TASAF* pale Mvumi kuna kitendo kibaya sana kilifanywa pale, walengwa wa *TASAF* wanagawiwa fedha zao halafu mgambo wakasimama dirisha la pili, halafu wakaanza kuwachangisha mchango kwamba nishike mkono wanachangia elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo nimemlalamikia Mheshimiwa Waziri na Naibu wake bahati nzuri nawashukuru sana wamelifanyia kazi na nimeona barua kutoka kwa Mtendaji Mkuu wa *TASAF* kwamba zile pesa zirudishwe kwa wale walengwa wa Kijiji cha Mvumi *Mission* na walengwa wote wa Wilaya ya Chamwino ambao walikatwa fedha zao kwa mchango ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli nilitaka kushangaa sana mgonjwa badala ya kupewa *drip* halafu kuna watu wengine wenyewe ndiyo wanamtoa maji sasa. Sasa niombe Mheshimiwa Waziri tamko liwe la haraka utakapojibu hapa, hebu jambo hili lifanyike haraka ili wale walengwa warudishiwe pesa zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nina mambo machache sana, moja ni mgawanyo wa ajira. Tukisema tutegemee mtandao peke yake jamani nataka niwaambie sijui kuna nini kinatokea hata kwenye mtandao, mtandao wakati mwingine unaruka watu maskini, huwezi kuamini mimi nitakupa ushahidi hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna mgao wa *net,* yaani pale Mvumi mission wote wenye uwezo wa kati majina yao kwenye mtandao yamesomwa nikiwepo Mbunge kupata *net* ya bure lakini vipofu na wasioona wote hawamo mtandao umewaruka. Sasa hili la ajira tukisema tuombe *online* kuna vijana wafamilia maskini hawatakaa wapate. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri, kwa sababu Taifa hili tunafahamiana, hizi ajira zitolewe kiwilaya au zitolewe kijimbo. Ukizishusha kama zilivyo ukasema Jimbo fulani limepata ajira nane Mbunge na watu wake pale na sifa wanazo, wataajiriwa watu ambao tunawafahamu, lakini kila zikitoka ajira watu unaowajua kwenye Jimbo lako hawamo na wenye sifa hawamo. Jamani nina mashaka na mtandao unakwepa watu maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninalotaka kulizungumza, tukiwa mgawango wa ajira kiwilaya au kijimbo tutamaliza hayo matatizo kwa sababu nchi nzima itaajiriwa mara moja utakuwa umewapata watu kutoka nchi nzima.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Dah, kaka yangu yaani leo niko vibaya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lusinde, Kanuni inasema kwa idhini ya Spika atatoa taarifa, kwa hiyo sijaidhinisha bado.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya naendelea, ndiyo nimesema aniache kidogo leo nina mambo mazito, Mheshimiwa Tabasam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ninalotaka kulizungumza hapa, kipaumbele cha ajira wapewe wale ambao wanaojitolea. Kuna watu wanajitolewa, wana miaka mingi wanafanya kazi ya kujitolea kwenye kila Idara, hao ndiyo wapewe kipaumbele cha kuajiriwa kwanza, lakini tukiwaweka kwenye kapu moja, wanaojitolea wanakosa wanapata watu wengine. Nchi yetu ina wastaafu.... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tabasam.

**TAARIFA**

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mchangiaji, mtandao wenyewe leo ni siku ya tatu umezimwa, unapatikana mijini tu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lusinde, endelea.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Sasa niwaombe watoa taarifa wengine watulie, nataka kuzungumza mambo makubwa ya nchi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lusinde.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepokea.

**MWENYEKITI:** Unaipokea, ahsante, endelea.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana, watu wanaofanya kazi ya kujitolea ndiyo wapewe kipaumbele cha kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ina wastaafu aina nyingi sana, ina wastaafu ambao wametumikia Serikali, lakini bahati mbaya sana ina wastaafu ambao hawajawahi kufanya kazi popote, yaani yeye anazaliwa, anatakiwa ajifundishe kilimo anaingia kazini, anaingia kusoma, akishamaliza kusoma anaomba kazi hapati, kila akiomba kazi hapati, kwa hiyo kilimo hajui, kuchunga hajui na kazi aliyosomea hana. Huyu tunamweka kwenye kundi gani? Hawa katika uzee ndio tunashauri wapewe kiinua mgongo cha wazee ili waweze kuishi, kwa sababu Tanzania ni ya kwao na sisi ndiyo tumewanyima hiyo ajira. *Qualifications* anazo lakini mpaka anazeeka hajawahi kuzitumia mahali popote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nataka niende kwenye suala la Utawala Bora. Nchi yetu imeweka vizuri sana masuala ya Utawala Bora kisheria lakini kuna baadhi ya vyama, kwa mfano pale Zanzibar *ACT-Wazalendo* tunashirikiana nacho kwenye Utawala Bora, sisi tuna Rais, tuna Serikali, wao wana Makamu wa Kwanza wa Rais, lakini nimemsikia Kiongozi Mkuu wa *ACT-Wazalendo* Zitto, anamnanga Mheshimiwa Magufuli kana kwamba Zitto hashiriki kwenye Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili nataka niliseme, Mheshimiwa Magufuli aheshimiwe, Zitto aelewe kwamba suala la kufiwa ni suala kubwa. Haiwezekani tuache kwenye utawala bora kulizungumza suala la Magufuli kusemwa vibaya na mimi sitaacha. Mheshimiwa Zitto anatutaka tunaompenda Mheshimiwa Magufuli tukazikwe naye. Zitto ndugu zangu amewahi kufiwa na mama yake, mimi sitaki kuingia huko, mama wa Zitto ni mama yangu mimi, ametangulia, mimi nimewahi kufiwa na baba yangu, lakini *ACT* wamewahi kufiwa na Makamu wa Kwanza wa Rais, Zitto analazimisha sisi tumseme vibaya Maalim Seif, hatuwezi, hatuwezi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii ninapoongea hapa Waislam mmefunga, dini inakataza kuwasema vibaya marehemu, Zitto ni Muislam anajua. Zitto ametukosea sana Watanzania, Zitto atuombe radhi Watanzania, Zitto

amemkosea sana mama Magufuli, Zitto ameikosea sana familia ya Magufuli. Hili jambo siyo sawa. Ndugu zangu tusifikiri kwamba kumsema vibaya Magufuli kutatusaidia, hawezi kujibu, hayupo. Kama ulikuwa na tatizo naye maliza utakuja kukutana naye kwa Mwenyezi Mungu. Mtu akishatangulia, kitabu chake kinafungwa tunamwachia Mwenyezi Mungu kuja kutoa hukumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inakuwaje watu mnakuwa waoga Viongozi wakiwepo hamsemi, wakiondoka ndiyo mnasema, huu ni uoga uliyopitiliza. Mtu mmoja tu alisema kwa vitendo kwamba yeye hawezi kufanya kazi na Magufuli, Nyalandu aliachia ubunge hapa akaondoka, lakini wote tuliobaki hapa ni watu wa Magufuli na tumefanya naye kazi na tulikuwa tunamsifu. Hivyo ndivyo ambavyo tunatakiwa tumsifu Mheshimiwa Samia na ndiyo kazi tunayofanya hapa, tusiweke unafiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaambie, hawa watu ambao sasa hivi wanamsema vibaya Mheshimiwa Magufuli na kumsifu Mheshimiwa Samia ni wanafiki wakubwa. Mheshimiwa Samia akiondoka watamsema vibaya hivyo hivyo, hivyo hivyo, ni bora mimi Lusinde ambaye niko wazi na siwezi kuacha, haiwezekani!

Kwa hiyo nchi yetu ili iendelee na utawala bora hawa watu tunashirikiana nao, Viongozi waliokufa wale ni watu wazito, Maalim Seif amefanya kazi kubwa, Mheshimiwa Magufuli amefanya kazi kubwa. Sasa ukisema kwamba wanaompenda Mheshimiwa Magufuli wakazikwe na Mheshimiwa Magufuli maana yake nini? Hii ni kashfa kubwa sana. Zitto aliombe radhi Taifa hili, awaombe radhi familia ya Magufuli na asirudie tena kufanya mambo ya kipuuzi kama hayo. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Lusinde.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ngoma imeisha, sasa sabufa ndiyo lilikuwa limefunguka.

**MWENYEKITI:** Hitimisha hoja yako kwa dakika moja, dakika zako zimeshakwisha.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilimwita Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja hii muhimu ya Waziri wa Utumishi. Kwanza kabisa nachukua fursa hii kumpongeza Waziri mwenyewe, lakini pia kumpongeza Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wote. Kipekee kabisa niwapongeze watumishi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama umewahi kuwa mtumishi kidogo tu unafahamu hali halisi iliyopo huko. Watumishi wa Tanzania wanafanya kazi kwenye mazingira magumu, nami nafahamu watu wengi wamejaribu kuchangia hata chanzo cha kuhama, mimi Jimbo langu ni la vijijini, unaweza ukaenda kwenye zahanati ambayo iko kijijini kabisa lakini unakuta mtoto wa kike ana miaka 23 anafanya kazi huko na yupo huko anafanya kazi vizuri. Kwa hiyo kipekee kabisa niwapongeze watumishi wa Tanzania wanajitolea na wanafahamu hali halisi ya nchi yetu, niwapongeze sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu hapa ni moja tu. Naomba niendelee kuongelea kuhusu changamoto ya upungufu wa watumishi tulionayo. Hili tatizo ni la Kitaifa, lakini naomba nitoe mfano kwa Wilaya ya Chemba na hasa kwa watumishi wa afya. Nilimsikia Daktari Chaya, jirani yangu Manyoni yeye ameongeza watumishi wa afya, angalau yeye anafika asilimia 50. Mimi kwenye Kada ya Afya nina asilimia 27 tu. Mahitaji ya watumishi kwa ujumla ya Kada ya Afya ni

838, lakini tulionao ni 173, sawasawa na asilimia 22 tu. Mnaweza mkafikiria ni kwa namna gani sasa unaweza kuhudumia hawa watu wetu walioko huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme maneno kadhaa, sisi tuna vituo vya Afya vinne, tuna kituo cha Afya kipya sasa hivi ambacho tumejengewa na *KOICA* kipya kabisa ambacho kimejengwa kama Hospitali ya Wilaya. Hata hivyo, hivi tunavyoongea hakina mtumishi hata mmoja na hatuwezi kukifungua kwa sababu hakuna watumishi, lakini tumejengewa na wafadhili. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, kituo hicho kipo kule Soya na katika maeneo ambayo tulifanya vibaya kwenye kura ilikuwa ni kwa sababu hiyo. Tukaenda kutafuta Mfadhili huko akatoa bilioni 1.2 amejenga Kituo cha Afya. Kituo cha Afya kipo tayari na wamenunua kila kitu na vifaa, lakini hakuna watumishi, hakuna namna ambavyo tunaweza kukiendesha kile Kituo cha Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe Waziri wa Utumishi lakini pia nimwombe Waziri rafiki yangu Mheshimiwa Bashungwa pale aangalie kwenye watumishi hawa wanaoajiriwa, watupelekee kule. Hospitali ya Wilaya ipo tayari, lakini nataka niwaambieni Wilaya ya Chemba hakuna Daktari wa Meno hata mmoja, yaani wilaya nzima pamoja na kuwa tuna Vituo vya Afya vinne, tuna Hospitali ya Wilaya, tuna Vituo vya Afya viwili ambavyo viko tayari havina Madaktari, lakini Wilaya nzima ukitaka kwenda kutibiwa meno lazima uende Kondoa au lazima uje Dodoma. Niwaombe sana, niwaombeni sana hawa wanaowaajiri angalieni sana Wilaya ya Chemba. Ni kweli Wilaya ya Chemba ilikuwa sehemu ya Kondoa, sasa kila kitu kipo lakini watumishi hatuna. Nataka niombe hili lizingatiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili na la muhimu sana, tuangalie juu ya ikama ya uwiano, yaani unaweza ukashangaa sana kwamba hizi Wilaya zingine sijui ziko wapi. Utakuta wakati Wilaya ya Chemba ina asilimia 22 ya Watumishi wa Kada ya Afya, zipo Wilaya zina asilimia 88, sasa hii haiwezi kuwa sawa hii, yaani Tanzania hii Wilaya moja ina asilimia 22, Wilaya nyingine ina asilimia 87 na watumishi hao

hao wanaajiriwa na Serikali, hii haiwezi kuwa sawa. Ni lazima tuangalie njia nzuri ambayo walau tutagawana watumishi hawa pamoja na kuwa kuna upungufu kila mmoja apate walau kwa kiwango kile ambacho kinastahili. Hilo lilikuwa la muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, sina mambo mengi, nafahamu kuna shida kwenye Kada ya Elimu lakini angalau kwenye Kada ya Elimu tuko asilimia 49, upungufu uliyopo ni kama asilimia kama 51, hivyo tuangalieni huku ambako Wilaya zetu zimeanzishwa juzi juzi na Wilaya za vijijini na ni ukweli kwamba wakati mwingine unaweza ukashangaa sana wanasoma taarifa za namna gani kwenye Afya Wilaya fulani imefanya, halafu unalinganisha Wilaya ambayo ina asilimia 22 ya watumishi unailinganisha na Wilaya ambayo ina asilimia…

**MWENYEKITI:** Weka *mic* yako vizuri Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasema kwamba, unataka kulinganisha wilaya hiyo na wilaya ambayo kimsingi haina watumishi wa afya wala watumishi wa elimu. Niwaombe sana sana, nimesimama hapa kwa ajili ya ombi hilo maalum Kituo cha Afya Soya ambacho tayari kimekamilika, kimejengwa na wafadhili wa *KOICA,* watuletee watumishi wa afya ili hospitali ile ifunguliwe na tulishamwomba na Waziri Mkuu aje aifungue. Sasa anafunguaje wakati hakuna hata Daktari mmoja. Pia tumeshawatumia *database* kule *TAMISEMI* wanafahamu kwamba kuna idara ambazo kabisa hatuna Madaktari kama nilivyosema Idara ya Meno. Niwaombe sana, waliangalie hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Monni kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, wakati huo Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga na Mheshimiwa Iddi Kassim pamoja na Maganga wajiandae.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naomba pia niseme kwanza naunga mkono hoja. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Utawala na TAMISEMI kwa hiyo sehemu kubwa ya mijadala hii tumeijadili na tumemshauri Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili kama walivyosema wenzangu, naomba pia nitumie nafasi kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayofanya hasa kwa juhudi kubwa anazozifanya sasa hivi za kuitangaza Tanzania huko nje. Niliwahi kusema kwenye Bunge hili kwamba tuliwahi kusafiri na Kamati ya Bunge kwenda mji mmoja China, tulipofika hawaijui kabisa Tanzania na wakawa wanashangaa ukiwaambia Tanzania mpaka wa-*google* waangalie Tanzania iko wapi. Kwa hiyo kwa Mheshimiwa Rais kwenda kwenye vyombo vya kimataifa sehemu kubwa ya watu wasioijua Tanzania wataanza kuifahamu Tanzania, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumza suala moja kuhusu umuhimu, kwanza kuipongeza Serikali kuhusu ajira mpya zilizotangazwa, lakini umuhimu wa uwepo wa kanzidata kama ilivyozungumzwa na mchangiaji mmoja jana. Tumeshauri sana jambo hili kwenye Kamati, nataka nitoe mfano kule kwangu kuna Kijiji kinaitwa Mgusu, ili mwananchi wa Mgusu aweze kuhudhuria *interview* moja Dar es Salaam au Dodoma anahitahi karibu siku saba. Moja atatoka Mgusu kuja kulala Geita na pale atalipa shilingi 20,000, atalala *guest* shilingi 20,000, atatoa nauli kwenda Dar es Salaam shilingi 50,000, akifika Dar es Salaam siku mbili kabla atakaa *guest* atalipa shilingi 50,000, 50,000. Kwa hiyo mpaka siku anafanya *interview* ameshatumia 300,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtanzania huyu atafanya *interview,* ataambiwa hakuchaguliwa atarudi. Kwa hiyo mwananchi, huyu Mtanzania ambaye anatafuta kazi anahitaji takribani 400,000 mpaka 500,000 katika kila *interview* moja inayotangazwa na Serikali. Ili aweze kupata kazi au asipate kabisa kama alivyosema Mheshimiwa Lusinde atahudhuria *interview* zisizopungua 10. Wapo watendaji,

Watendaji tu wa Mitaa wameenda mikoa karibu 20 kutafuta utendaji wa mtaa na kila akienda jina lake halimo. Vile vile zinatangwa ajira hapa *TRA* wanatakiwa 1,000 wanaomba 10,000 na wote 10,000 wanaitwa, yakisomwa majina hayumo. Inatangazwa Uhamiaji, wanatangaza nafasi 400, wanaomba na kuitwa 8,000, yakisomwa majina hayumo. Matokeo yake huyu mtu anayekuja kwenye *interview* Uhamiaji amehudhuria *interview* karibu 10. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi nchi hii haiwezekani mimi niliyefanya leo *interview* nikabaki kwenye *database* kwa miaka miwili au mwaka mmoja. Jibu la Wizara ni kwamba wanafanya kwa miezi sita, miezi sita haitoshi Mheshimiwa Waziri anao mfano, tumefanya interview mwezi wa 11 za *TRA* juzi wametangaza zingine, miezi minne, lakini wameita watu wote hawajaita ambao walifaulu. Ukiangalia kwenye orodha walikuwa wanataka watu 400, walifaulu zaidi ya watu 2,000. Matokeo yake ni nini? Kila unapoita zinazokwenda kuajiriwa ni zile *fresh mentals*. Kwa sababu mtu akitoka chuoni anaweza kujibu maswali ya *interview* vizuri kuliko mtu aliyemaliza mwaka juzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikupe mfano, mimi ni Mhasibu na wengi humu ni *professionals,* tukichukuliwa leo kwenda kwenye usaili, kozi uliyosomea unahitaji mwezi kujiandaa, lakini hutajibu sawa na mwanafunzi aliyetoka chuoni jana. Matokeo yake ni nini? Aliyemaliza chuo mwaka 2017, 2018, 2019, 2020 anachanganywa kikapu kimoja na wa mwaka huu, anayefaulu ni wa mwaka huu, wa mwaka jana anabaki mtaani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi niiombe Serikali kwa sababu nina uhakika hatuna *first in, first out*, wanaohudhuria kwenye usaili wakifaulu wawekwe kwenye kumbukumbu tuepuke kuwa na mtu anastaafu kabla ya kufanya kazi, amesema hapa Mheshimiwa Lusinde. Hii inatokeaje huko nje, kwanza tuna shida moja tumeweka *carders* nyingi kwenye *Universities* ambapo sina uhakika kama kuna *research* imefanyika kuangalia ni kozi gani ni muhimu. Mwingine kasoma sijui *public* sijui nini, mwingine sijui *public*

nini, kwa hiyo huko mtaani watu wana vyeti vingi, hakuna ajira, hakuna kazi, kila akisoma tangazo la ajira kozi aliyosomea haimo. Waliojaa mtaani huko *Procurement*, sijui Uhasibu, sijui nini, *public* sijui, lakini akisoma ajira hayumo, matokeo yake wanaotangazwa hayumo, wanaoajiriwa hayumo, miaka 45. Ndiyo maana mwaka jana, mwaka juzi tulijikuta kwenye uchaguzi wa CCM Jimbo moja wamechukua fomu watu 60 asilimia 80 walikuwa ni *graduate* hawajapata kazi. Ushauri wangu hapa kwa Mheshimiwa Waziri, nafahamu alilichukua jambo hili, tuwe na hii kanzidata, mtu akihudhuria *interview* mara moja tu-*communicate,* tumuulize bado una interest na kazi hii. Kama kazi hiyo hana *interest* nayo hatuna sababu ya kumsafirisha tena kumleta Dodoma, inakuwa ni kero. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wote unaowaona wanakuja Dodoma kufanya *interview* Wabunge tunachangia nauli. Sasa nataka tujiulize, una watu 20 wanakuja hapa, wakifika wanakwambia sisi tumemaliza *interview* hatukuchaguliwa wote, tunaomba nauli ya kurudi nyumbani, unatoa wapi pesa hiyo? Naomba jambo hili lichukuliwe *serious* sana, lakini tufanye utafiti kuangalia soko la ajira nchini limekaaje ni ajira zipi ambazo tuhamasishe watu wasome. Watu wanasoma wanamaliza hawana pa kwenda, wanadaiwa mikopo na tumetunga Sheria hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la pili, tumeiona *PCCB,* ipo kwenye Kamati yetu, tunawapongeza kwa kazi nzuri wanazofanya. Nataka kujiwekeza kwenye jambo moja tu, wakati wa uchaguzi *PCCB* ni *very active* na inakuwa *very, very active* kwa Wabunge walioko madarakani. Sasa huwezi kumaliza rushwa kwa kumvizia mtu mmoja unayemjua peke yake. Nilishuhudia uchaguzi ulioisha kila unapokwenda wewe upo *monitored* lakini mko 40, wale wengine hakuna anayewatafuta. Sasa tuwe na utaratibu, tuna vyombo vingi, wagombea wanajulikana, kama wapo watu wanataka, kwa mfano ukiangalia kuna nchi ambazo wagombea wanajulikana, waanze kufuatiliwa mapema. Ukimsubiri mtu siku ya uchaguzi alishamaliza kampeni, utafanya kazi ya zimamoto na utajikuta siku moja umepata

Viongozi wote hawana sifa kwa sababu wameshinda kwa rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Constantine John Kanyasu. Nilimwita Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, wakati huo Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi pamoja na Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga wanajiandaa.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja hii muhimu ya Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora. Kwanza nitoe shukrani zangu za dhati kwa Wizara hii lakini pia kwa Mheshimiwa Rais kwamba baadhi ya mambo tuliyoyaomba mwaka jana kwa upande wa Jimbo langu yameanza kutekelezwa, hasa ujenzi wa Ofisi ya TAKUKURU ambao walikuwa wanakaa kwenye godauni, sasa umeanza tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo napenda kushukuru, ni kwamba tumeshawasilisha sasa ombi letu la ukarabati wa zahanati kupitia Mfuko wa *TASAF*. Zahanati ya Kijiji cha Mkalanga na Zahanati ya Kijiji cha Winome ambazo wananchi ndio wameibua miradi hii ili zile ziweze kukarabatiwa na kukamilika kupitia Mfuko wa *TASAF*. Naomba kupitia kiti chako basi Wizara hii iweze kuzifanyia kazi angalau kwenye bajeti hii ili zahanati hizi mbili ziweze kukarabatiwa na kwa umahiri wa Mawaziri pamoja na Watendaji wa Wizara hii, nina hakika ombi hili litapokelewa kwa mikono miwili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuzungumzia mambo machache, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa, kwa hiyo, mambo mengi kwa kweli tumekuwa tukishauri kwenye Kamati. Jambo la kwanza ambalo tumekuwa tukiendelea kushauri, nami ningependa kulisisitiza hapa ni kuhusu watumishi wanaojitolea kwenye sehemu mbalimbali. Watumishi hawa wanajitolea kwa muda mrefu, wengine miaka sita wengine nane wengine saba, hasa

walimu na wale wa kwenye sekta ya afya, na wengine wanajitolea kwenye mazingira magumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hakuna mfumo maalum wa kujitolea, japo mahitaji ya kujitolea yapo, tulitoa ushauri utengenezwe mfumo maalum unaowatambua watu wanaojitolea ili inapofika wakati wa kuajiri tuwe na hiyo *database*. Kwa sababu, siku hizi mtu anakwenda tu anaongea na Mkuu wa Shule na anaanza kujitolea, au anaenda Zahanati, anaanza kujitolea. Hii haitoi fursa sawa. Kwa sababu, mtoto wa masikini anaweza akaenda pale akakataliwa, lakini mtoto wa Mtendaji wa Kata au Mwenyekiti wa Kijiji, akapata fursa kwa mamlaka au mtoto wa mtu mwingine mwenye mamlaka. Kukiwa na mfumo mzuri wa kujitolea ambapo tunajua mahitaji yapo, utasaidia kufanya *acceleration* wakati wa kuajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba hii haipo, naomba iangaliwe namna itakayokuwa *fair,* ya kuwafanya wale waliojitolea muda mrefu kwenye hizi ajira waweze kupata kipaumbele. Jambo la pili ambalo ningependa kulisema na tumelizungumza pia hata kwenye Kamati, ni suala zima la mafunzo. Utakuta kwenye maeneo mengi wanaohudhuria mafunzo ni viongozi katika ngazi za Wilaya, labda wakuu wa Idara na wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao Watendaji wa Kata, na kwa mujibu wa taratibu na Kanuni za muundo, wao ndio kama viongozi katika Kata; na wale watendaji wengine awe Afisa Kilimo au Afisa Mifugo, wanaripoti kwao. Jambo la kwanza, pamoja na kwamba vitendea kazi hawapewi, unakuta wa Mifugo wamewapa, labda wa elimu wamepewa pikipiki, yeye bosi wao hana hata baiskeli. Hilo linaweza likawa linaangukia TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mafunzo sasa. Tulishauri na ninaendelea kushauri kwamba mtu hawezi kutoka Chuoni au huko aliko akaanza kufanya kazi zile bila kupata mafunzo maalum. Tulishauri Chuo cha Utumishi wa Umma kiweze kutoa hayo mafunzo ili watumishi hawa wa

ngazi ya Kata na hatimaye wa ngazi za Vijiji waweze kuwa na umahiri wa kutenda kazi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa Watendaji wa Kata kwa kuwa tumesema ni Wakurugenzi katika ngazi ya Kata, waweze kujua wajibu wao wa Ukurugenzi katika ngazi ya Kata; wanawajibika kufanya nini? Kwa sababu, wakati huo utakuta kwenye Halmashauri kuna Masijala na nini; nenda kwenye ngazi ya Kata, hata *Folio* kwenye *file,* huyu mtu hajawahi kufundisha na haelewi. Kwa hiyo, haya ni mambo ya muhimu sana ambayo tungependa yatiliwe mkazo kwenye bajeti, hasa kwa ajili ya Chuo cha Utumishi wa Umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo naomba, hili ni wasilisho la ombi langu ni kuhusu *Watumishi Housing*. Sasa hivi ujenzi wa nyumba nyingi unaendelea mijini. Nitaje mfano kama Kilolo; Mji wa Kilolo ni Mji unaokua. Watumishi wengi pale kila siku tunafukuzana nao kwa sababu wanataka kuishi Iringa Mjini na ukiangalia ni kwa sababu pale Kilolo hakuna nyumba hata za kuweza wao kupanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napendekeza, hizi Wilaya ambazo zimejengwa kwenye maeneo ambayo hayakuwa Miji, zipewe kipaumbele kwa kujengewa nyumba na *Watumishi Housing* ili miji ile kwanza iweze kukua, na pia kuleta tija kwamba watumishi watakaa pale, kwa sababu, vinginevyo utakuwa unawabana watumishi kukaa kwenye sehemu ile, lakini sasa hakuna makazi ambayo wanaweza kukaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Watumishi *Housing i-plan* vizuri ili tuweze kuwa na makazi ya kutosha hasa kwenye eneo hilo nililolitaja la pale Wilaya ya Kilolo ambapo Mji ule ni mdogo na unahitaji sana huduma hiyo. Jambo la mwisho ambalo ningependa kuchangia ni kuhusu upungufu wa watumishi. Wilaya ya Kilolo kama zilivyo Wilaya nyingi za vijijini ina upungufu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeweza kusoma takwimu nyingi, lakini kwa sababu ya muda niongelee kwenye sekta ya afya. Ili angalau tuweze *ku-operate,* Zahanati ambazo zimemalizika kujengwa na Vituo vya Afya tulivyomaliza kujenga, tunahitaji watumishi 39. Kwa hiyo, nikitaja yale maelfu, najua huenda yasiwe na tija sana. Hawa 39 watatusaidia angalau kwa kuanzia na hawa wanaweza kupelekwa kwenye Vituo ambavyo, ni kama Zahanati ambazo hazijaanza kabisa kama Zahanati ya Mbawi, Masege, Lugalo, Ilole, Mlafu, Ibofwe, Ikuka na Idunda Vituo vya Afya vya Ng'uluwe na Nyalumbu ambavyo hivyo nilivyovitaja, vimekamilika, lakini sasa hatuwezi kuanza kufanya chochote kwa sababu hakuna watumishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni kwa sababu najua kuna ajira hivi karibuni, basi ninaomba kwamba yale maombi yetu yatakapoletwa ieleweke kwamba hizi ninazozitaja zinahitaji kwa kiwango kikubwa sana *attention* ya karibu na kama...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Justin Lazaro kwa kuzungumza huku unaangalia kiti ili kikikupa alama kwamba muda umeisha ukaweza kuona.

Nilimwita Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii nami kuchangia kwenye hotuba hii ya Utumishi. Kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kutoa kibali cha *promotion* kwa wafanyakazi wote nchini kwa bajeti tatu mfululizo kwa maana ya 2018/2019, 2020/2021 na 2019/2020. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapozungumzia leo habari ya watumishi, sitapenda kuacha kutoa pongezi nyingi sana kwa Waziri Mkuu wetu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa, kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya na harakati zake za kuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha ya kwamba anawasemea watumishi na kutetea maslahi ya watumishi nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza dada yangu Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya na kaka yangu Mheshimiwa Ndejembi, wanafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuchangia mambo machache sana kwa siku ya leo. Wamezungumza hapa suala zima la mafao, sitataka kulirudia, lakini nataka nikazie tu kwamba, hata kwenye Jimbo langu la Msalala, suala zima la mafao kwa wastaafu limekuwa ni changamoto kubwa sana, hasa kwenye familia ambazo wamepoteza watu wao ambao wanastahili kupewa hayo mafao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatolea mfano leo kwenye Kata ya Burige kuna mama mmoja alifiwa na mume wake Mtendaji wa Kijiji, leo hii tunazungumza ni zaidi ya miaka kadhaa sasa, bado hajapatiwa mafao ya mume wake ili yaweze kumsaidia katika harakati za kusomesha watoto wake na kulea familia yake. Kwa hiyo, naendelea kuomba na kusisitiza Wizara waone namna gani wanaweza kuboresha mfumo huu wa mafao ili wastaafu waweze kupatiwa mafao yao kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua hapo zamani tulipokuwa na Mfuko wa *LAPF* na *PSSF* tunaona changamoto hizi zilikuwa ni chache sana, lakini sasa baada ya kuundwa mfumo huu changamoto zimekuwa ni kubwa sana. Kwa hiyo, naendelea kumwomba dada yangu Mheshimiwa Jenista Mhagama kuhakikisha ya kwamba wanalitilia suala zima la mafao ya wastaafu waweze kupata kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kuzungumzia suala zima la upungufu wa watumishi. Katika Jimbo langu la Msalala tuna upungufu wa watumishi takribani 500. Kama alivyochangia Mheshimiwa Mbunge mwenzangu hapo, kwamba sisi tunaotoka katika Majimbo ya vijijini, hali ya mazingira katika maeneo yale ni ngumu sana. Watumishi hawa wanaishi katika mazingira magumu mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao upungufu mkubwa wa watumishi, wengi wao wanahama katika maeneo yale kutokana na mazingira magumu ya pale. Siungani na Mheshimiwa Tabasam kwa hoja aliyoisema hapa kwamba wanatakiwa wahame kwa sababu wanatakiwa waolewe. Nasema mazingira magumu na mikopo ndiyo inayowafanya watumishi katika maeneo yetu hasa katika kada ya Ualimu, Afya na maeneo mengine waondoke katika maeneo yale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ije na mfumo, ikiwezekana waweze kutafuta hata taasisi moja, ambayo itaweza kuwatafutia mikopo isiyokuwa na riba. Watumishi hawa hasa walimu katika maeneo yetu wanakopa sana *VICOBA* kutokana na hali ngumu ya maisha iliyoko kule. Leo hii utaniambia kwamba mwalimu anakwenda kufundisha darasani, lakini kila wakati anapigiwa simu za madeni na riba kubwa ambazo yeye mwenyewe katika mshahara hawezi kupokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nakuomba dada yangu Mheshimiwa Jenista Mhagama uangalie namna gani ya kutafuta, ikiwezekana uongee na Taasisi za kibenki, ambazo zitaweza kuweka mfumo mzuri kuwasaidia hawa watumishi wetu huko waweze kupata mikopo yenye riba nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba upungufu wa watumishi katika Jimbo la Msalala ni mkubwa sana, na nizungumzie katika Idara ya TAKUKURU. Wilaya ya Kahama ina Halmashauri tatu, lakini nimefanya utafiti, Wilaya nzima, tunao watumishi 10 tu wa TAKUKURU. Katika watumishi 10 hao,

ni wanne tu ambao wanafanya kazi za kwenda kufanya *investigation* huko katika Halmashauri hizi. *(Makofi)*

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Cherehani.

**TAARIFA**

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mchangiaji anachangia katika Wilaya ya Kahama na katika Jimbo la Ushetu pia Mheshimiwa Rais anapeleka fedha nyingi sana, lakini hatuna watumishi wa TAKUKURU wala Ofisi ya TAKUKURU; pia, anavyoongea mchangiaji nataka nimpe taarifa kuwa katika Jimbo la Ushetu tumemaliza Zahanati sita na Kituo cha Afya kimoja, lakini hatuna watumishi hata mmoja kwa ajili ya kuwahudumia wananchi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, unapokea taarifa?

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napokea taarifa hii ya Mbunge mwenzangu kwa sababu ndio Mbunge ambaye tunatoka kwenye Wilaya moja. Wilaya ya Kahama ina Majimbo matatu kwa maana ya Ushetu, Msalala na Kahama Mjini. Kama ninavyosema, tuna watumishi 10 tu wa TAKUKURU na watumishi hao 10 wa TAKUKURU ni wanne tu ambao wanafanya shughuli hizo za tafiti na katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Jimbo la Msalala, Mama Samia Suluhu Hassan ameweza kutupatia kwenye bajeti ya 2021 zaidi ya takribani shilingi bilioni 24 kwenye miradi ya afya, kwenye miradi ya umeme na kwenye miradi ya elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo hivyo kwenye Jimbo la Mheshimiwa Cherehani Ushetu nako fedha zimekwenda

nyingi. Ni saa ngapi sasa hao wafanyakazi wanne tu wa TAKUKURU wataweza kusimamia miradi ile? Nimemwona Mkurugenzi wa TAKUKURU hapa ndugu yangu Salum yuko hapa, Mheshimiwa Waziri tuongezeeni na ikiwezekana mtuletee Ofisi kwenye Halmashauri zetu. Idadi hii ya watu 10 ambayo imetajwa hapa ndiyo idadi sahihi ya kwenye kila Halmashauri, lakini sisi tutaangalia Halmashauri tatu, zote tuna wafanyakazi 10 tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, atuongezee na ikiwezekana atuwekee ofisi za TAKUKURU kwenye kila Halmashauri; kwa maana ya Halmashauri yangu ya Msalala, Halmashauri ya Ushetu na waliopo wabaki Halmashauri ya Kahama Mji. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Nicodemas...

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilimwita Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga wakati huo wafuatao wanajiandaa: Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Amandus Julius Chinguile.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hotuba ya Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora. Awali ya yote napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu tena kwa siku ya leo kuweza kusimama mahali hapa kuwawakilisha wananchi wangu wa Jimbo la Mbogwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye hoja kulingana na muda. Wilaya yangu ya Mbogwe ina upungufu

wa watumishi 467 kwenye nyanja mbalimbali; walimu pamoja na kitengo cha afya. Namwomba Waziri wa Utumishi na Utawala Bora aangalie Wilaya yangu ili kusudi iweze kupata watumishi 467 ili wananchi wangu wa Mbogwe waweze kuhudumiwa kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo zipo changamoto zinazowakabili watumishi hasa kwenye upande wa afya. Unakuta mgonjwa amekuja huyu mtumishi anakwenda kumhudumia lakini hakuna vifaa tiba. Daktari anakutana na mgonjwa ambaye ameumia kwa ajali mfano ya bodaboda, hana vitendea kazi. Kwa kuwa, Wizara hii inahusika na watumishi, ni vyema Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri mtenge muda wa kuwaona kwanza watumishi hawa matatizo yao. Ni shida gani zinazowakabili katika upande wa utumishi wao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo changamoto nyingi kwa watumishi. Mimi nimekaa nao, nimekuwa mwanachama sana wa kupiga nao *story* watumishi ili kujua shida gani inayoweza kuwakabili kwenye kazi zao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la uhamisho, Mheshimiwa Tabasam pale amezungumza japokuwa watu wameshindwa kumwelewa vizuri. Naomba nifafanue hiyo hoja. Suala la ndoa ni amri kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwamba kila mtu atakuwa na mwenzake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kumekuwa na tabia, mtu anapata uhamisho kwenda Mtwara kutoka kwa mfano, Bukoba; ina maana ndoa hiyo inakuwa ya *ku-scratch scratch,* hakuna ndoa pale tena. Maana katika taratibu za ajira jinsi zinavyotolewa hizi ruhusa ya kwenda kusalimia watu wako nyumbani ni kwa mwaka sijui siku 14 na vile vile akitaka mtu aende sasa kwenye familia yake, Serikali inatoa nauli tu bila kuangalia kwamba huyu mtu anaishi Mtwara, anatakiwa alale Dar es Salaam kesho yake ili aamkie kwenda kwenye familia yake, kunakuwa hakuna bajeti kama hiyo. Kwa hiyo, hilo Serikali iliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala moja la hawa madereva. Mwaka jana wakati naingia humu nilizungumzia habari ya madereva. Katika sekta hii ya utumishi, madereva wanapata taabu sana. Ajali hazitaisha bila kuwasemea hawa watu. Kuna baadhi hata ya Waheshimiwa, wanakaa na madereva hawasemeshani ndani ya gari. Lililopo, dereva hapo anakuwa anafikiria tu jinsi gani ampige chini bosi wake ili kusudi maisha haya yaendelee. *(Makofi)*

*Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuta dereva halipwi mshahara, hana mkataba wa kufanya kazi, anavyopelekwa dereva, yaani bora hata kuku au ng'ombe, yaani anaburuzwa tu. Unakuta Mbunge ametoka hata Bungeni bila kujua dereva huyu amekula, wala nini; kana kwamba yeye sio binadamu, ni kama anatumia remote. Inaniuma sana kwa kuwa maisha haya ya udereva na mimi nilishayaishi. Kwa hiyo, hii sekta sasa ione sababu, na Mheshimiwa Waziri…(Makofi)*
**[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, unao mfano wa Mbunge ambaye anafanya hivi? Maana umetaja Wabunge hapa.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana, siyo vizuri kumtaja mtu. Watajijua tu wale wenye roho mbaya, wataweza kuacha.

**MWENYEKITI:** Basi ifute hiyo; kwa upande wa Wabunge, ifute hiyo.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya, naifuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee tu kwa kuwatetea hawa madereva. Kuna dada yangu pale aliongelea suala la madereva wale wanaosafiri na magari makubwa *(transit),* wanapata taabu sana kwenye nchi hii, lakini hawa madereva wana chama na wana uongozi wao wa Kitaifa, nimekaa nao. Ukiwasikiliza madai yao ni ya msingi. Wanapopewa malori siku ya kuachishwa kazi hawaandaliwi kwamba lini mkataba wa ajira utasitishwa. Hawa madereva

wana familia zao, wanalisha kupitia haya magari, lakini pale anapomdai tajiri mshahara wake, tajiri anamsingizia *lose* pamoja na mambo mengine ili kuweza kumfukuza huyu dereva. Kwa hiyo, kwenye sekta hii haijakaa vizuri, naomba Wizara hii kwa vile inahusika, iweze kuliangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, kwenye Halmashauri yangu nina wasomi wengi sana, hawajapata ajira. Mheshimiwa Lusinde amezungumza. Naomba sasa kama kuna uwezekano tufumue huu mfumo wa kuajiri kwa *computer,* maana *computer* hazichukui watu wa kijijini. Kuna walimu wengi vyeti vinaoza majumbani, hawapati ajira. Kuna madaktari wengi wamesoma, wako vijijini, wengine walishakata hata tamaa kabisa kuingia kwenye *online* hizi, maana hata kama *uki-apply* haupati kazi unakuta imefyatua tu watu wengine wa Dar es Salaam, Arusha lakini Mbogwe haionekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kwa ushauri wangu, hizi ajira ziwe zinatolewa kila Halmashauri ili wasomi hawa tuliowasomesha kama Serikali waweze kuajiriwa. Kama kuna ugumu sana, Serikali muwe wawazi tu, kama nafasi zilishajaa kabisa hakuna haja hata ya kuwalazimisha watu kusoma sasa. Maana unamlazimisha mtoto anapomaliza Darasa la Saba akasome, atafute ajira, halafu kazi zinakuwa hazipatikani. Watu hawa wanakuwa hawajui kusoma, hawajui kulima na kufanya kazi zile nyingine ngumu. Wamefanya kazi yao ya kusoma na wamehitimu vizuri, lakini ajira hazipatikani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iliangalie suala hili la kuajiri watu upya. Wapo watu wanajitolea miaka na miaka, wengine wana miaka hadi 15 wanajitolea kwenye mashule kufundisha pamoja na kufanya mambo mengine, lakini hawapati ajira kabisa. Kwa hiyo, namwomba Waziri ajaribu kuliangalia hili suala ili kwenye Halmashauri zetu katika hizi ajira ulizozitangaza 3,200...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** ...ziweze kupatiwa ufumbuzi, kila Halmashauri *at least* watoke watu mia mbili mia mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Nicodemas Maganga. Nilimwita Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo sasa aweze kuchangia.

**MHE. BAHATI K. NDINGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kupata fursa. Nami nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, *management* yote ya Wizara na taasisi zake kwa kazi nzuri ambazo wanaendelea kufanya katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nita-*base* kwenye vitu viwili kuishauri na kutoa maoni yangu kwenye Wizara hii. Kwanza ni Chuo chetu cha Utumishi wa Umma na vile vile mafunzo kwa Watumishi wa Umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaona kuna upokwaji mkubwa wa taasisi hii kufanya majukumu yake, kwa sababu chuo hiki kilianzishwa kwa ajili ya kuwafunda watumishi wa umma, lakini sasahivi tumekuwa na utaratibu wa kawaida kabisa kwa mtumishi kuingia ofisi ya umma pasipo kupitia kwenye chuo hiki, na ndiyo maana tunayaona haya ambayo yako kwenye mitandao. Utaona si dhambi sasahivi kuona *document* ya Serikali ambayo imendikwa siri kwenye *Instagram,* tunaona kabisa unaingia kwenye ofisi ya umma mtu amevaa kama anaenda disco, ni kawaida kabisa kwa sababu wameacha kukitumia ipasavyo Chuo cha Utumishi wa Umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo zamani ilikuwa kwamba, ili mtumishi yeyote aanze kazi ni lazima apite kwenye chuo hiki kufanyiwa *induction program.* Kwenye *induction program* utaelezwa mipaka yako kwa nafasi yako,

bosi wako umuheshimu vipi, mipaka yako inaishia wapi. Sasahivi ugomvi mwingi ulio kwenye taasisi mbalimbali ni kwa sababu watu hawapikwi kwenye chuo hiki. Mtu anaona jambo hili napaswa kufanya mimi pasipo kufanya huyu. Kwa hiyo mgongano ni mkubwa. Ni lazima Wizara ikipe msisitizo chuo hiki kuwafunda watumishi wa umma, la sivyo vitu vya kwenye mitandao na tabia za ajabuajabu za kwenye utumishi wa umma hazitakoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii kwenye hili suala la *training* tunaona TAMISEMI wanaajiri, wanapeleka watumishi wao Chuo cha Hombolo. Chuo cha Kodi wakiajiri wanapeleka watumishi wao chuo chao cha kodi. Wakiajiri bandari wana chuo chao cha bandari, kila taasisi zina vyuo vyao, lakini kule wakienda ukiangalia *program* wanazozisoma si za utumishi wa umma, wanasoma *program* za kama *job description* zao. Mfano kama bandari utakusanyaje kodi, utafanya hivi, Hombolo vilevile wanafanya hivyo. Sasa utumishi wa umma haupati fursa ya kuwafunda wale watumishi wa-*behave* vipi kwenye nafazi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe *coordination* ndani ya Serikali. Hawa watumishi wanavyowekwa kwenye hivi vyuo; kama wakiwa Hombolo mfanye *coordination* mchukue chuo hiki kina wataalam wengi waende wakawape *training* ya utumishi wa umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kuhusu mafunzo kwa watumishi. Ni mashahidi humu ndani ili gari hata liwe zuri ni lazima ufanye *service.* Unakuta mtumishi wa umma anakaa *five years,* haendi hata kwenye mafunzo, Kwa sasa mambo yanakwenda yanabadilika, *technology* zinabadilika. Ni lazima mafunzo nyawe si hiyari yawe ni lazima na wawepo na *program* maalum, kila baada ya muda fulani watumishi wawe wanaenda kwa kupokezana kupata mafunzo mafupi ili kuwajengea uwezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifanya hivyo tutapunguza matatizo mengi ambayo yanawakumba watumishi wa

umma na utumishi; lakini vilevile Mheshimiwa Waziri ni lazima uwe na wivu na utumishi. Utumishi wowote ndani ya nchi hii uko chini yako. Wewe ndiye unayeteuwa kwenye idara nyingine, Wizara nyingine; kwa hiyo ni lazima kuhakikisha kuna *coordination* ya kutosha. Hata kama TAMISEMI wanaajiri, lakini wale waishaajiriwa ni watumishi wa umma, lazima wafanye kazi kwa kufuata misingi ya utumishi wa umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nakushukuru kwa nafasi. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo kwa mchango wako mfupi, lakini umeeleweka.

Nilimuita Mheshimiwa Halima Mdee. Wakati huo Mheshimiwa Amandus Julius Chinguile anajiandaa.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Na mimi niungane na wote ambao wanazungumzia utumishi wa umma, wanazungumzia wafanyakazi wanapoajiriwa, suala la umri; ukisema umri miaka 25 wakati Wabunge wengi hapa wanasema tuwaangalie wale ambao walikuwa wameshaanza kujitolea, *then* nadhani itakuwa hai-*make sense.* Kwa hiyo, naamini Waziri wakati anajibu yale masharti ya umri yatakuja kutolewa kulingana na mazingira yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, yamekuwa yakizungumzwa masuala mengi sana kuhusiana na kustaafu. Waziri Jenista atasema yeye anahusika na watumishi wa umma, lakini vilevile atasema masuala ya kustaafu yako Wizara ya Vijana kwa sababu inasimamia mifuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ni ukweli hivi vitu haviwezi kutenganishwa. Nimesema mtumishi anaanza pale anapoajiriwa, pale anapofanya kazi, pale anapostaafu. Sasa unapokuwa na mtumishi sasahivi yuko kazini halafu hajui mustakabali wake baada ya ajira, akiwa mtu mzima wakati

viungo vya mwili vimechoka hana uwezo wa kufanya kazi, hiyo si sawa. Na kwa sababu Serikali ni moja ninatarajia kabla Mheshimiwa Jenista hajajibu Waziri anayehusika na mifuko atueleze Watanzania hali ya mifuko ya umma ikoje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana kazungumza Mheshimiwa Bulaya hapa, akasema, tathmini iliyofanyika inaonesha mfuko wa *PSSF* uko *below average,* una hali mbaya. Unatakiwa kwa wastani kwa kiwango cha chini iwe asilimia 40, leo iko asilimia 22, tunataka mtujibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipitia Taarifa ya *CAG* kidogo. Shirika la Reli, kwa mfano, unaambiwa makato ya Mfuko wa *Pension* kwa Watumishi wa Umma ya thamani ya shilingi bilioni 99.6 hayajapelekwa *PSSF.* Yani kuanzia mwaka 2015 mpaka mwaka 2021 watumishi wa Shirika la Reli, shirika la umma, makato yao hayajapelekwa. Hivi mtasema hamtakiwi kujibu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunajenga reli ya *SGR.* Reli ya *SGR* ikikamilika na matawi yake yote ambayo hili Shirika la Reli ndilo linasimamia itaigharimu Taifa shilingi trilioni 32, *SGR* na matawi yake yote. Hivi kweli tukiwaambia kwa nini msiwajibike kutoa taarifa hapa ili watumishi wa nchi hii wajue hali yao? Tunataka Waziri wa Kazi ukija hapa, hii ni Serikali, tunazungumza na Serikali, mmelipa trilioni mbili sijui *point* moja hatifungani sio *cash.* Tunataka ile trilioni 2.58 iliyobaki ilipwe sasa ili mfuko uwepo kwenye uhai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Jenista niliwahi kuuliza hapa, kwa sababu mfuko huu unalipa wale wafanyakazi kabla yam waka 99 waliokuwa hawachangii. Kwa hiyo, hatushangai Wabunge wanavyosema wastaafu wanastaafu mafao yanachelewa kwa sababu lile kapu halina hela, huo ndio ukweli.

Kwa hiyo tunataka Mheshimiwa tujibiwe, hiki kikombe ulikikimbia ulivyoondoka ile Wizara, hiki kikombe tunataka kijibiwe leo na Serikali kwa sababu tunazungumza na Serikali. Hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Wakala wa Ndege Mheshimiwa Jenista. Wakala wa ndege uko chini yako, *ATCL* wanasema sababu ya kushindwa kufanya kazi ni kwa sababu wanawalipa Wakala wa Ndege tozo ya kukodi na pesa ya marekebisho ya ndege, ukarabati wa ndege. Na wanasema zimelipwa milioni 159, wanasema hivi wanawalipa nyie fedha za ukarabati, lakini ikija kwenye ukarabati hamtoi pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Jenista ukurasa wa 41 wa hotuba yako inasema wazi kabisa...

**MWENYEKITI:** Unaongea na Kiti ee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naongea na...

**MWENYEKITI:** Unaongea na Kiti. Usimu-*address* Waziri.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naongea na wewe ndiyo, huku namu-*address* Mheshimiwa Jenista Mhagama. Unasimamia Wakala wa Ndege, kwenye mipango yako ya mwaka huu, unasema wazi kabisa utafanya matengenezo ya ndege ya viongozi wakuu, utafanya matengenezo ya ndege ambayo ni aina ya *Forker 50,* hakuna ndege yoyote kati ya hizi ambazo ni zile ndege 16 za *ATCL,* hapa ndipo ulipo mzizi wa fitina.

Sasa nataka ukinijibu uje ueleze kwa namna gani zile fedha ambazo kwa akili ambayo kwa kawaida hai-*make* mantiki mmekodisha ndugu zenu shilingi bilioni 159 ambazo kati ya hizo milioni 59.4 ni za matengenezo ya ndege. Kwa nini mnaliachia shirika la ndege likarabati na kufanya matengenezo ya ndege zake peke yake? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mwisho, na si kwa umuhimu. Tunaambiwa kwamba...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilimuita Mheshimiwa Amandus Julius Chinguile, wakati huo mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa ni Mheshimiwa Askofu Josephat Mathias Gwajima.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa nafasi. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uhai, lakini kipekee nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya kwa ajili ya kuboresha maisha ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Dada yangu Mheshimiwa Jenista Mhagama na Naibu Waziri, Mheshimiwa Deo Ndejembi, kwa kweli, wanafanya kazi nzuri. Na mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa, yako mambo mengi tumewashauri, lakini tumejadiliananao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijielekeze moja kwa moja kwenye upungufu wa watumishi. Kwenye Jimbo langu la Nachingwea kwa mfano, kwenye elimu ya msingi mahitaji ni watumishi 1,319 waliopo ni 788, upungufu ni 531. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye elimu sekondari. Mahitaji ni 786, waliopo ni 412, mapungufu ni 374. Na afya vilevile nae neo la utawala kwa maana ya maafisa watendaji wa kijiji na wa kata. Eneo hili tulitolee macho kwa ukubwa wake na hasa maeneo haya ambayo ni mikoa ya mipakani, Lindi, Mtwara na maeneo mengine. Twendeni tuyape kipaumbele cha makusudi kabisa. Na hapa ndipo tunapokuja sasa kuona namna ambavyo wenzetu wanaoomba kwa mfumo huu wa mtandao akipangiwa kwenda Nachingwea anasema niko tayari, lakini akifika baada ya miezi mitatu, baada ya muda anasema sasa baba ni mzee kwelikweli, amezeeka baada ya mwaka mmoja? Haiwezekani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, anachagua kwenda Nachingwea ni kwa sababu, nafasi iko Nachingwea, lakini akishapata *check number* basi anakumbuka sasa kumbe naweza nikaomba kwa sababu sheria ipo na inamruhusu yeye kuomba uhamisho baada ya muda fulani. Kwenye hili, mimi nishauri Serikali yangu, tuone namna ambavyo tutatoa kipaumbele kwa wale wenye sifa ya kufanya hizi kazi wanaotokea kwenye maeneo haya; na hii itatusaidia, wale vijana wako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii imejaliwa wasomi kwelikweli katika kila kata, kila wilaya, wasomi, ma-*graduate* ni wengi kwelikweli wapo. Ni Serikali tu kuweka utaratibu mzuri wa kuwatumia hawa ma-*graduate* ili tusipate upungufu huu kwa sababu ya watumishi wengine kuhama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwa wale makaimu. Nilitoa taarifa hapa kwa Mbunge mwenzangu, sasa naona nilielekeze hilo. Kwa mfano, Halmashauri yangu ya Wilaya ya Nachingwea ziko idara na vitengo vinne kuna makaimu, lakini kibaya zaidi yuko kaimu anakaimu zaidi ya miaka 11, hii haikubaliki. Sasa hapa utamleta sasa mtumishi ambaye wewe umeona ana sifa kutoka eneo lingine, huyu mtu nimesema hapa tunampa ugonjwa wa sonona, tunamsababishia *pressure* na magonjwa mengine yasiyoambukiza, hii si sawa. Na kama ni *vetting* tunamuacha miezi sita ya kisheria, anakwenda mwaka, anakwenda miaka miwili… *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge ni vizuri hilo jina ulilosema anakaimu miaka 11 ukawapatia pia Mawaziri badae.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitafanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inapomletea sasa mkuu wa idara kutoka eneo jingine na yeye awe chini yake kwa kweli, unamuacha kwenye mazingira magumu sana huyu mtumishi. Hii si sawa na haikubaliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelekezo yako nimeyapokea nitafanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni juu ya wastaafu, kuna suala la uhakiki. Hili ni kizungumkuti, kila mwaka wanakwenda kuhakikiwa mkoani; ni jambo jema kuhakiki kama wazima au la, lakini suala la kutoka huko vijijini waliko kwenda mkoani jambo hili ni gumu na hawa wastaafu walio wengi hali zao ni ngumu kwelikweli. Hapa Waheshimiwa Wabunge wenzangu wamesema... *(Makofi)*

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa, Mheshimiwa Kuchauka.

**TAARIFA**

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nampa Taarifa muongeaji, hili suala la kwenda kuhakikiwa mkoani limekuwa ni janga kwelikweli. Mtu anatoka Kijiji kwa mfano Mpigamiti, kilometa zaidi ya 30, aje Liwale Mjini kilometa 50, atoke Liwale Mjini kwenda Lindi ambako ni kilometa 360. Huyo mstaafu huyo ana umri wa miaka 80 au mwingine ana miaka labda 75 hivi, unamtakia kweli maisha mema?

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mzigo huu. Kwa hiyo, nampa Taarifa anachikisema ni sahihi kabisa kwamba, huu mzigo tunaubeba sisi Wabunge. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa unapokea Taarifa?

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea kwa mikono miwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii si sawa na bahati nzuri hao wastaafu walio wengi wamechoka sana. Tuone namna ya kuwawekea mazingira rahisi sehemu ambayo ya kuhakiki, wanaweza kufanya kule Halmashauri, lakini pia tunaweza

tukaboresha kwa namna nyingine ambayo tunaona inafaa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwenye hizi ajira mpya zinazotolewa, hili nalo ni tatizo lingine. Tatizo sio kupata ajira, tunajua na tunaiheshimu sana mamlaka, na kwakweli kubwa zaidi niipongeze Serikali kwenye eneo hili kwa kutoa hizo ajira. Kazi kubwa hiyo mmefanya tunawashukuru, lakini ni namna gani hawa vijana wanakwenda kupata hizi kazi? Ni kizungumkuti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na huu mfumo wa ajira kwa maana ya kuomba kwenye mtandao si Rafiki na hasa kwa wale vijana walioko vijijini. Huu mtandao una changamoto, unaweza ukakaa wiki nzima bado wewe unaendelea kuingia *online* na mtandao hausomi, badala yake hata muda wa kuomba hizo nafasi umeshapita. Tuone namna tutakavyowasaidia hawa vijana kweli wa Kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako Wabunge hapa wamesema ni vizuri sasa tukaona mgawanyo mzuri kwa kutumia wilaya, majimbo, namna tutakavyoona inafaa ili kila kijana Mtanzania aweze kunufaika na hizi ajira zinazotoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la mwisho, niwapongeze sana wenzetu wa *TASAF* na hasa kwenye ile miradi ambayo wameitekeleza, wanafanya kazi nzuri sana. Nimesema mimi ni mjumbe wa kamati na tumeona miradi mingi inapendeza kwelikweli; tumekwenda Zanzibar, kazi nzuri tumeiona. Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yako ya *TASAF* mimi nawapongeza sana. Kazi hii nzuri iendelee, lakini pia sasa mtolee macho na maeneo mengine ambayo hamjafika kwenye miradi ya kimkakati ikiwemo kule Nachingwea, Liwale, Rwangwa na maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako Mheshimiwa Amandus. Sasa, nimuite Mheshimiwa Askofu Gwajima aweze kuchangia.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikusukuru sana wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika hoja hii ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimshukuru Mheshimiwa Rais ambaye kwa *logic* hasa na yeye ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini pia ni Waziri wa hii ofisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujikita hasa kuongea kwa Habari ya dhana ya utawala bora. Mwaka jana siku kama hii wakati hoja ya ofisi hii imeletwa mezani niliomba Serikali kupitia aliyekuwa Waziri, Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, kwa Habari ya Masheikh wa Uamsho waliokuwa wamekaa miaka minane jela bila kupelekwa Mahakamani. Na nilipoiomba Serikali, naishukuru Serikali kwamba, ilifanyia kazi vizuri na Masheikh hawa waliachiwa. Nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiri, pia niliomba tena Serikali kwa ajili ya kutekeleza dhana ya utawala bora wakati ule, kushughulika na suala la Mashekhe waliokuwa Arusha. Masheikh zaidi ya 18 ambao nao waliwekwa ndani miaka mingi bila kesi yao kusikilizwa, nashukuru Serikali imeyatimiza hayo na Mashekhe hao waliachiwa ahsante sana nakushukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hiyo liko jambo moja tu ambalo nataka kulizungumzia leo ambalo ni dhana ya utawala bora. Mara nyingi Viongozi Wakuu kama Rais, wanapotoa matamko yenye lengo la kuijenga nchi, viongozi walio chini ambao ni wajibu wao kutekeleza matamko hayo, wanatakiwa wawe makini sana na mahiri sana katika kuyatekeleza matamko ambayo yametolewa na Viongozi Wakuu kama Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano nimnukuu Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan katika mkutano wake mmoja alisema: "*ninaomba muwapange wamachinga*" hayo ndiyo maneno aliyosema, hakusema naomba muwafukuze wamachinga, hakusema naomba muwapige wamachinga, hakusema naomba muwavuruge wamachinga. Mheshimiwa Rais alisema naomba muwapange wamachinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili lilileta mambo ya ajabu, dhana ya Mheshimiwa Rais iwapange wamachinga ilikuwa njema, nzuri yenye maana na tija kwa wamachinga wenyewe. Lakini watekelezaji walipoanza kutekeleza dhana hii, wakaanza kuwakimbiza wamachinga kuwapiga, kuwanyang'anya mali zao, bomoa mabanda yao, haikuwa dhana ya Mheshimiwa Rais na hii inaharibu dhana ya ujumla ya utawala bora kwa wale watekelezaji walio chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikupe mfano, Mheshimiwa Rais aliposema wapangeni wamachinga hakumaanisha wafukuzwe. Kupanga wamachinga siyo lazima uwaburuze ukawaweke kwenye kibanda, dhana ya machinga anamfata mteja, machinga hafuatwi na mteja hiyo ndiyo dhana ya machinga. Ukimchukua machinga ukamuweka kwenye kona siyo machinga tena, ukamuweka kwenye duka siyo machinga tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikupe mfano tena, sehemu kama Uingereza kwa mfano ukienda *Tottenham* au East London kuna nyakati ambazo wanafunga mitaa kuwaruhusu wale *vendors* wauze vitu vyao, hata wakati fulani hapa wakati wa utawala wa Mzee Kikwete ile barabara yetu ya karibu na Makao Makuu ya Chama cha Mapinduzi Jumamosi walikuwa wanafunga ili hawa watu wauze vitu vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitegemea Watendaji wenye akili yenye kupanga vizuri, wangewaza badala ya kuwafukuza wamachinga wawe angalau na *machinga's day,* waseme wamachinga fanyeni kazi yenu Jumatatu au fanyeni kazi yenu Jumanne au Jumatano kuwe na siku

mojawapo ambayo wamachinga wanaruhusiwa kufanyakazi zao ili kuruhusu utaratibu mwingine uendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukifanya kama ulivyofanya kwa wamachinga leo, nakuhakikishia wamachinga watarudi tena mitaani kama kawaida. Huwezi kuwaweka kwenye banda wamachinga na ukafikiri watakaa pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu hawa machingas ni *fans* wetu wakubwa wa uchaguzi na ndiyo wapiga kura wetu wakubwa sana tunapowavuruga leo watatuvuruga siku chache zijazo, tutavurugika kweli kweli na tusijifanye hatuoni. Kuna msomi mmoja aliwahi kusema ni afadhali kisu cha Daktari kinachopasua ngozi kwa lengo la kuponya, kuliko dawa ya kuondoa maumivu inayomponya mtu kwa muda halafu ikampeleka kwenye maumivu ya kifo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuseme ukweli, kwenye suala la machinga *we are on the wrong destination,* tumeenda vibaya na wamachinga hawa watatuhukumu siku chache zijazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kuwa kwenye Kata ya Kawe, Mikocheni, Bunju na maeneo mengine ya Jimbo la Kawe nina wamachinga wa kutosha, ninaomba nijitoe kabisa kwenye hili suala la kuwakimbiza wamachinga na kuwapeleka kona moja baada ya nyingine kwa mambo ambayo wangeweza kutengenezewa na wakakaa vizuri na wakaenda vizuri. Kwa hiyo, hapa hatujaenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nisema kuna baadhi ya watu wanamharibia Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Rais alikuwa na maana njema kabisa, wapangwe wamachinga! Kupangwa angesema wamachinga fanyeni shughuli zenu za machinga Alhamis peke yake, siku zingine mtulie nyumbani, hiyo ndiyo maana ya kupanga wamachinga. Huwezi kusema wamachinga wajipange wakati ni watu wenye njaa wanahitaji chakula, *after all* kusema ukweli hatuwezi kufikia mpangilio kwa viwango vya Ulaya, hii vurugu

mechi yetu ya wamachinga ndiyo utalii wenyewe ule kwetu huku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii *mismatch* ya machinga ndiyo yenyewe. Kwa hiyo, nataka kusema hapa hatujaenda sawa na lazima tujue lile soko la Ilala Machinga litengenezwe halina machinga mle sasa hivi, tunatengeneza masoko mengine ya machinga hayatakuwa na *matching guys* wataendelea kuzurura mitaani, kwa hiyo lazima tuwe na namna nzuri ya kuwa *handle* hawa mabwana kwa sababu nao ni Watanzania wenzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho...

**MWENYEKITI:** Naomba utumie dakika moja kuhitimisha Mheshimiwa Gwajima.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika zangu zimekimbia haraka. Naomba sasa nihitimishe kwa kusema ni vizuri viongozi wetu wakubwa wanapotoa maelekezo, watekelezaji walio chini waangalie *modality* nzuri ya kutekeleza hayo yaliyosemwa na kiongozi ili kuondoa kumfanya kiongozi aonekane ameharibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. STELLA A. IKUPA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake shupavu na mahiri unaopolekea maslahi ya watumishi wa umma kuboreshwa na kuongezeka kwa ajira kwenye kada mbalimbali ambazo zilikuwa na uhaba mkubwa wa watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Waziri na watendaji wa Wizara hii kwa jinsi wanavyomsadia

Mheshimiwa Rais kutimiza ndoto zake kwa wananchi na ahadi zilizo ndani ya Ilani ya CCM kupitia mipango mbalimbali inayoandaliwa na Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali katika ajira zinazotolewa walau iwe inatengwa hata asilimia kati ya 10 mpaka 12 kutegemea na idadi ya ajira zilizotangazwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya pembezoni kama Ukerewe yana upungufu mkubwa wa watumishi, hivyo nashauri katika ajira zinazotolewa basi maeneo haya yapewe kipaumbele. Kwa mfano, Ukerewe ina upungufu wa zaidi ya 50% ya watumishi, hivyo yaangaliwe kwa ukaribu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa watendaji wa vijiji na kata unaathiri sana shughuri za maendeleo; kwa mfano, Wilaya ya Ukerewe ina upungufu wa watendaji wa kata na vijiji 26 hali inayoathiri shughuli za maendeleo kwa wananchi. Hivyo nashauri Halmashauri zipewe haraka vibali vya kuajiri watendaji wa kata na vijiji.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala la usaili wa ajira *(interview).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nampongeza Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri, Naibu Waziri na timu nzima kutoka Wizarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuwasilisha mchango wangu kuhusiana na usumbufu wanaopata vijana wengi wanapoomba nafasi za ajira na kuitwa kwenye usaili ambapo idadi inayoitwa ni kubwa kuliko idadi inayotakiwa. Mfano idadi ya vijana wanaoitwa inaweza kuwa 5,000 wakati wanaotaka kuajiriwa ni robo ya hao tu. Hii si sahihi kwa kuwa vijana wengi wamekuwa wakitumia gharama kubwa huku ikijulikana wazi hawawezi kuajiriwa. Hivyo inawakatisha tamaa na kuwapa umaskini walezi wa

vijana hao kwa gharama wanazotumia kuhudhuria usaili na kurejea bila chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujua pia kama ajira mpya zinazingatia jinsia kwa maana ya wanawake na wanaume katika nafasi zinazotangazwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo naona ni wakati muafaka baadhi ya taasisi kama *TRA*, Bunge na Mahakama kupewa mamlaka ya kuajiri kama ilivyokuwa awali kwa kuzingatia mahitaji hivyo kuupunguzia mzigo Wizara. Naomba kuwasilisha.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Serikali, Waziri na watumishi wote kwa kazi nzuri wanazozifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa mchango wangu wa maandishi katika Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora katika maeneo yafuatayo; kwanza mishahara ya watumishi na kupanda madaraja. Kwa muda mrefu sasa Serikali haijaweza kuongeza mishahara kwa watumishi wa umma na kushusha moyo wa kufanya kazi kwa watumishi wengi. Hali ya mfumuko wa bei inaendelea kuathiri maisha ya watumishi wengi. Ili malengo ya Serikali yafikiwe ni muhimu kuangalia uwezekano wa kuongeza mishahara sanjari na mapunjo ya mishahara na madaraja ya baadhi ya watumishi ambao wamefika muda wa kupanda na kupunguza malalamiko ya watumishi wa umma.

Pili ni kuhusu mfumo wa *OPRAS* nchini; ni wazi kabisa mfumo huu ni muhimu sana kwa maendeleo endelevu, hivyo Serikali ikasimamie na kufanya kazi kwa uwazi na uwajibikaji. Hivi sasa mfumo unaonekana hauna tija kwa kuwa haujasimamiwa vizuri na kutoa matunda tuliyoyatarajia. Ni vizuri iwepo siku ya kutangaza matokeo ya tathimni ya utekelezaji wa mfumo huu kwa mtumishi mmoja mmoja na pia taasisi. Taasisi zifanyike *overall performance* na kutangazwa matokeo yao hadharani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu ni suala la Serikali mtandao; naipongeza Serikali kwa kuendelea kuimarisha mifumo ya TEHAMA na Serikali mtandao. Lakini kuna haja pia ya kufanya utafiti na tathmini ya mfumo huu unavyofanyakazi ii kupima mafanikio na kubaini changamoto zilizopo ili nchi ipige hatua kubwa.

Nne, mpango wa *TASAF;* hivi Serikali imefanya tathimini ya mpango huu na kuona haja ya kuendelea na mpango huu? Hivi sasa maeneo mengi wanalipwa watu wasioruhusiwa na walengwa wanabaki nje ya mpango. Naona ipo haja ya kuangalia mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano ni suala la rushwa nchini; sasa hivi rushwa ni kubwa sana katika miradi na zabuni katika maeneo mengi ya nchi yetu. Je, ni mkakati upi hasa ambao umeandaliwa kupunguza rushwa na kujenga nidhamu, uzalendo, uadilifu na uwajibikaji? Katika taasisi nyingi bado hali si shwari kabisa.

Sita ni kuhusu mafunzo kwa viongozi na watumishi wa umma; kwa muda mrefu wa sera ya mafunzo na utekelezaji wake bado ni kitendawili. Mafunzo mpaka sasa yanachukuliwa siyo kitu muhimu. Ni vizuri suala la mafunzo kwa viongozi wa umma, watumishi wa umma lipewe uzito mkubwa. Huko nyuma suala la *leadership competence framework* iliandaliwa na Chuo cha Utumishi wa Umma lakini hadi leo halijatekelezwa na hakuna mafunzo kwa kuzingatia *framework* hiyo. Ni vizuri Serikali ikaliangalia vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba masuala hayo hapo juu yaangaliwe na kufanyiwa kazi vizuri ili kujenga misingi ya utawala bora na utumishi uliotukuka.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano

wa Tanzania; Mawaziri na viongozi wote wa wa Ofisi ya Rais – Utumishi, kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka wa Ofisi ya Rais – Utumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Spika na uongozi wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Utumishi, kwa hotuba nzuri iliyojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha utayari wa Taifa letu katika kuboresha maisha ya wananchi na pia utayari wetu wa ushindani wa Kimataifa *(National Competitiveness).* Bajeti hii inaenda sambamba na dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 ambayo ni kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mapitio ya kipindi cha bajeti 2021/2022, Serikali kupitia Wizara ya Utumishi na Utawala Bora imesimamia kwa uadilifu na ufanisi mkubwa masuala yote ya utumishi na hasa kurudisha uwabikaji kazini iliopelekea ufanisi mkubwa hasa kwenye utekelezaji wa miradi. Jimbo la Mbeya Vijijini limenufaika kupitia miradi ya *TASAF* ambapo imebadilisha maisha ya wananchi katika vijiji husika. Pia kwa kusimamia vizuri, rushwa na upendeleo umepungua kwa kiasi kikubwa kupelekea ufanisi mkubwa sehemu za kazi na hata miradi kukamilika kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio hayo makubwa, napendekeza kuendeleza mafunzo ili kuboresha weledi wa watumishi ikiwemo upanuzi wa Chuo cha Watumishi Mbeya na eneo muafaka kwa ujenzi wa chuo kipya na cha kisasa ni Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ambapo kuna maeneo mazuri ikiwemo yaliyokuwa mashamba ya *Tanganyika Packers,* Mbalizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na upungufu mkubwa wa watumishi katika sekta mbalimbali, napendekeza Serikali iendelee kutoa ajira zaidi hasa kwenye maeneo ya kuchochea uchumi na pia sekta ya afya, elimu na kilimo. Kutokana na idadi kubwa ya wahitimu kukosa ajira na wametapakaa kila kona ya Tanzania hasa vijijini, napendekeza Serikali kuhakikisha ajira zinatolewa kwa usawa wa maeneo yote ya Tanzania kulingana na sifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na majukumu na unyeti wa mashirika ya kadhaa ya umma ikiwemo ushindani wa kupata watalaam wazuri, mashirika haya yaruhusiwe moja kwa moja kutoa ajira ili yaendane na mahitaji yao na Tume ya Ajira wawe na jukumu la ushauri/udhibiti. Taasisi kama *CAG* kisheria anatakiwa awe huru ikiwemo uhuru wa kuajiri na hata taasisi kama mabenki, *TANESCO*, Bandari, *TRA* ni muhimu wakapewa uhuru wa kuajiri kulingana sifa ila kupata watalaam wazuri kiushindani na pia kulingana na bajeti za mashirika husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maboresho ya mfumo wa *TASAF,* napendekeza pia kuboresha zaidi mfumo huo ikiwemo msukumo wa miradi ilenge maeneo yatakayochochea uzalishaji wa mali ili zisaidie jamii kwa upana mkubwa. Pamoja na maeneo ya uzalishaji, msukumo ujumuishe kuimarisha masoko ya bidhaa zitakazozalishwa katika maeneo ya mradi. Miradi ilenge kuboresha elimu na hata kusomesha watoto wanaotoka kwenye kaya maskini ya maeneo husika. Serikali iboreshe taratibu za kupata maeneo ya miradi ya *TASAF* ili kupunguza malalamiko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze mchango wangu kwa kumpongeza sana Rais Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayofanya kwa kuongeza ajira, kupandisha vyeo kwa watumishi nchini. Jambo hili linakwenda kupunguza kwa kiasi kikubwa cha upungufu wa ajira na kuongeza ufanisi katika kada mbalimbali. Ninapo kwenda kumpongeza Mheshimiwa

Rais pia niwapongeze sana watendaji walioko kwenye Wizara hii wakiongozwa na Waziri Mheshimiwa Jenista Mhagama, nawapongeza kwa kumsaidia vyema Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo sasa napenda kutoa ushauri wangu katika mambo yafuatayo; kwanza tunapo kwenda kuajiri watumishi hasa kada ya elimu na afya ni lazima kuzingatia uhitaji, jiografia na taaluma ya wahitimu kwani yapo maeneo watumishi wapya huenda kwenye ajira mpya kwa lengo la kuchukua *check number* tu na baadaye kuhamia maeneo ya mjini. Mfano Halmashauri ya Liwale tumekuwa tukipokea watumishi wengi sana lakini baada ya muda mfupi uhaba unajirudia kutokana na watumishi wengi kuhama. Lakini tunao vijana wanaojitolea kwenye shule na zahanati zetu kwa muda mrefu na wanapoomba ajira hawapati pamoja na kupata barua kutoka kwa Wakurugenzi wa Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishauri juu ya miradi ya uwekezaji inaofanywa na Mifuko ya Jamii. Ni lazima miradi hii ifanyiwe stadi za muda mrefu na makini kuepusha kupoteza fedha nyingi kwenye miradi isiyokuwa na tija. Vilevile miradi hiyo isimamiwe kwa karibu ili kupata thamani ya fedha zilizotumika. Mfano miradi ya *NSSF* iliyoko kule Kigamboni Dar es Salaam, miradi ambayo imetekelezwa si tu chini ya kiwango bali pia ni miradi isiyokuwa na tija, hivyo kupoteza fedha za taasisi husika.

Kuhusu Taasisi ya TAKUKURU kwa ujumla wake inafanya kazi vizuri pamoja na kuwa wapo watumishi wasio waaminifu bado wapo kwenye taasisi hiyo. Naiomba Serikali kufanya *vetting* ya kutosha juu ya uzalendo na uaminifu wao. Kuwepo kwa vitendo au viashiria vya rushwa kwenye taasisi yenye dhamana ya kupiga vita rushwa ni jambo baya zaidi, hivyo naomba umakini uongezeke ili kupunguza malalamiko katika jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa *TASAF;* taasisi hii lengo lake ni kuboresha au kusaidia kuinua vipato vya kaya au jamii. Je, hadi sasa Serikali imeshafanya utafiti

wa kiwango gani kujua hadi sasa ni kaya ngapi zilizonufaika na mpango huu na tayari zimeshatoka kwenye kaya maskini na kuingia kwenye kaya zenye kipato cha kati. Lakini pia hapa ningeshauri wanufaika hawa wangepatiwa vifaa au vitendea kazi badala ya fedha *cash.* Lakini ikibidi kupewa fedha *cash* basi zitoke kwa wakati na kwa usimamizi wenye weledi na umakini mkubwa, kwani yako malalamiko ya fedha hizi kuingia kwenye mikono haramu.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimpongeze Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya, pia nimpongeze Waziri na timu yake yote kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na upungufu mkubwa wa watumishi katika kada zetu mbalimbali, kwa Wilaya ya Lushoto kuna upungufu kwenye kada ya afya na elimu zaidi ya watumishi 11,000 hawa ni katika kada mbili, bado kada nyingine. Kwa hiyo, niiombe Serikali kwa kipindi hiki cha bajeti Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto iweze kupata walimu hao niliyoorodhesha hapo juu, hasa ukizingatia Wilaya ya Lushoto ina shule nyingi pamoja na vituo vya afya na zahanati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa *TASAF* unasaidia sana wananchi wetu, lakini kunakuwa na changamoto hasa kwa watu wa vijijini wengi wao kutopata fedha hizi za *TASAF* na ukikuta baadhi ya wanaopata unakuta wengi wao sio walengwa, hii inatutupia lawama sisi Wabunge. Lakini pia pesa za *TASAF* ziwe na *account* yake tofauti na ilivyo kwa sasa na pia inaleta mkanganyiko hasa pale pesa zinapoingia, zinachukua muda mrefu kuzipeleka kwa wahusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia niiombe Serikali ipeleke pesa hizi vijijini kwani huko vijijini ndiyo kuna wahitaji zaidi kuliko mjini, pia fedha hizo ziongezwe kiwango wanachopewa ni kidogo mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na malalamiko mengi kwa wastaafu wetu hawapewi stahiki zao kwa wakati

pindi wanapostaafu, unamkuta mstaafu anafuatilia mafao yake zaidi ya miaka miwili mwisho wa siku anafariki bila kupata mafao yake na ukizingatia wengi wanaostaafu hawana kazi nyingine ya kufanya. Kwa hiyo, mstaafu huyu unamkuta maisha yake yanakuwa ni ya taabu na mwisho wa siku humpelekea kuiaga dunia. Niiombe Serikali yangu tukufu iwalipe wastaafu wetu hawa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi wengi wanahama kwenye Halmashauri kwa sababu ya kupata mshahara mdogo tofauti na idara nyingine, mfano sasa hivi watumishi hao wanakimbilia kwenye mashirika kama *TANESCO, TARURA, TPDC* na *TASAF,* kwa hiyo huku wanapata mishahara mikubwa kuliko hawa wa Halmashauri, ukizingatia elimu zao ni sawa.

Kwa hiyo, niiombe Serikali iweke uwiano sawa wa mishahara ili kuondoa ubaguzi na sintofahamu na kufanyakazi kinyoge kwa hawa watumishi wa Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 1 Machi, 2022 kupitia barua yenye kumbukumbu namba JA.9/259/01A/45 lilitolewa Tangazo la kuitwa kazini kwa waombaji wa kazi wa nafasi mbalimbali waliofanya usaili kati ya tarehe 29 Desemba, 4 – 29 Januari, 2022 na tarehe 7-10 Februari. Miongoni mwa kada zilizoitwa kazini ni Shirika la Reli Tanzania *(TRC).* Vijana 359 walishachukua barua na kupangiwa kituo cha kazi. Walipopeleka *TRC HQ* waliambiwa watapigiwa simu. Mpaka sasa hakuna mawasiliano yoyote, wanaomba ufafanuzi.

Pia kumekuwa na malalamiko kwa kutoka kada ya Maafisa Tarafa kwamba majukumu yameongezeka, huku mshahara umeshuka. Hivi sasa Afisa Tarafa anazidiwa mshahara na Watendaji wa Kata anaowasimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimpongeze Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora na Naibu wake pamoja na watendaji wa Serikali katika Wizara hii kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utajikita kwenye; kwanza umuhimu wa Serikali kuanzisha mfuko maalumu wa *pension* kwa sekta isiyo rasmi ya wakulima, wafugaji na wavuvi; pili umuhimu wa Serikali kupitia upya sheria inayowafanya maprofesa kustaafu wakiwa na miaka 65 na kutokupata mikataba maalumu ya kuendelea kufundisha; na tatu, wakuu wa idara na taasisi mbalimbali kukataa kupitisha barua za watumishi wanaoomba kuhamishwa kutoka vituo vyao vya kazi kwa sababu maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, karibu asilimia 65 ya Watanzania wako kwenye sekta za uzalishaji za kilimo, mifugo na uvuvi. Kundi hili huishi maisha ya shida sana wanapofikia uzee na kukosa nguvu za kuendelea kujipatia kipato. Kwa kuwa watu hawa wako kwenye mifumo ya uzalishaji na hujipatia kipato, ni vyema Serikali ikafikiria namna ya kuanzisha mfuko maalum wa *pension* ukisaidiwa na makato maalum kutoka kwenye mauzo ya mazao kwa makundi haya ili yaingie kwenye mfuko wao maalum wa *pension.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili likiratibiwa vyema litakuja kusaidia makundi haya katika maisha yao ya uzeeni watakapokuwa hawana tena nguvu ya kufanya kazi na kujipatia kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo hili likifanikiwa na likisimamiwa vizuri, huko mbele ya safari wazee wetu waliostaafu katika kazi za kilimo, ufugaji na uvuvi hawatakuwa tegemezi wala ombaomba kwenye jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vyuo vyetu vikuu vya Serikali, kuna changamoto kubwa ya tatizo la rasilimali watu likiwa limesababishwa kwa kiasi kikubwa na kitendo cha Serikali kubadilisha utaratibu wa maprofesa kuendelea

kufundisha kwa mikataba maalum hadi wanapofikisha umri wa miaka 70.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kwa miaka michache iliyopita, zaidi ya maprofesa 91 waliondoka katika Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine kati ya Januari, 2016 na Desemba, 2020; maprofesa 111 waliondoka kwenye utumishi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Katika Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela, hakuna profesa hata mmoja wa somo la hisabati tangu aliyekuwepo alipoondoka, hapajakuwepo na mrithi wa kusaidia kusimamia *research* za mahesabu katika ngazi ya uzamivu. Hata kwenye soko la ajira si rahisi kuwapata wataalam wenye vipaji hivi na vyuo vyote vya Serikali nchini vinakabiliana na changamoto kama hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya rasilimali watu vyuo vikuu Tanzania inasababishwa pia na masharti magumu ya kuajiri wataalam kutoka nje ya Tanzania. Kuajiri wataalam kutoka nje kwenye maeneo ya kimkakati ni muhimu ili kutusaidia kwenye kukuza rasilimali yetu, na kutuunganisha na mifumo ya kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa vibali huchukua muda mrefu na husababisha walengwa kutoka nje kubadili mawazo na kuacha kuja kufanya kazi Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imejitokeza tabia ya wakuu wa idara na taasisi mbalimbali za Serikali kukataa kupitisha barua za watumishi wanaoomba kuhama na kwenda kufanya kazi kwenye sehemu tofauti kwa manufaa ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni haki ya mtumishi kuomba kuhama na kwenda kulihudumia Taifa sehemu yoyote hapa nchini anapoona ataongeza tija na maendeleo ya Taifa. Uamuzi wa mwisho wa kutoa ruhusa ya kuhama hutolewa na Katibu Mkuu - Utumishi na Utawala Bora. Wajibu wa mkuu wa idara au taasisi ni kupitisha barua ikiwa na mapendekezo yake na si kuzuia barua isifike ngazi za juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuelezea changamoto za hapo juu, naishauri Wizara yafuatayo;

kwanza Serikali ianzishe mfuko maalum wa *pension* kwa sekta zisizo rasmi za wakulima, wafugaji na wavuvi.

Pili, Wizara ya Utumishi na Utawala Bora itoe vibali vya kuajiri wanataaluma wa kutosha kuendana na idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa. Hii ni pamoja na kuajiri wataalam kutoka nje katika maeneo ya kimkakati kama yale ya sayansi, uhandisi na hesabu.

Tatu, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora wapitie sheria na kuongeza umri wa maprofesa kutumika kwa mikataba uanzie pale wanapostaafu wakiwa na miaka 65 na waendelee hadi wanapofikisha umri wa miaka 75. Hii haina hasara kwa Serikali kwani wanapostaafu mishahara yao inakuwa bado iko kwenye ikama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwaandaa hawa wataalam, Serikali hutumia gharama kubwa sana. Tunapositisha huduma zao, vyuo binafsi huwachukua bila gharama na kuwatumia kuwajengea sifa, ilihali vile vya Serikali vinadorora.

Nne, Waziri wa Utumishi na Utawala Bora atoe maelekezo kwa wakuu wa idara na taasisi za Serikali watende haki ya kupitisha barua za watumishi wanaoomba kuhama kwenye vituo vyao ili wampe fursa Katibu Mkuu mhusika kutoa uamuzi wa mwisho. Napendekeza watakaokaidi hili wachukuliwe hatua za kinidhamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Serikali kwa utendaji wao uliotukuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kulipa *promotion* za wafanyakazi, ni jambo jema, naipongeza sana Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa ninayoiona ni pale mfanyakazi anapostaafu kuna baadhi ya waajiri wanamsafirisha mfanyakazi wanapewa stahiki zao na wengine hawapewi mfano kada ya ualimu, wengine wanapewa na wengine hawapewi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ije na majibu je, stahiki hiyo ipo au imefutwa na kama ipo utaratibu wake ukoje? Nataka ufafanuzi mzuri utolewe vinginevyo nitashika shilingi. Mtumishi anapobadilisha kada anaweza kutoka kwenye mshahara wake ambao unaweza ukawa wa juu lakini kule anakoenda akashushwa mshahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli lengo la kubadilisha kada ni kutaka kupata zaidi, lakini mtu anaposhushwa kiwango cha mshahara hatuoni tuna viashiria vya rushwa na wizi katika maeneo ya kazi? Jambo hili liangaliwe namna nzuri ya kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MWENYEKITI:** tumefika mwisho uchangiaji upande wa Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawaita Waheshimiwa Mawaziri tutaanza na Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, atafuatiwa na Mheshimiwa Bashungwa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyoko mezani, kwanza nianze kwa kusema kwamba naunga mkono hoja hotuba ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ambayo imewasilishwa hapa mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuchangia tu jambo moja ambalo limejitokeza katika michango ya Waheshimiwa Wabunge kuhusiana na suala la wastaafu. Kwanza wamezungumzia suala la wastaafu kuchelewa kupata malipo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niliambie Bunge lako tukufu kwamba, mifuko yetu imeweza kulipa mafao kwa wastaafu kati ya kipindi cha mwaka 2018 ambapo Mfuko wa *PSSF* ulianzishwa hadi Machi 2022 tumeweza kulipa mafao yenye thamani ya Shilingi Trilioni Sita na Bilioni Tisini na Moja na kila mwezi Serikali inalipa fedha Shilingi Bilioni 58.75 kwa wastaafu 148,868 kwa mwezi tarehe 25 bila kukosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakiri kwamba kulikuwa na changamoto hasa kwa wastaafu ambao walikuwa wameanza kazi kabla ya mwaka 1999 ambao walikuwa hawachangii lakini wakaingia kwenye mfuko. Kwa hiyo hao walisababisha Mfuko kuelemewa kwa sababu walikuwa hawachangii lakini walikuwa wanatakiwa kulipwa na ndiyo hiyo hela ambayo mdogo wangu Ester Bulaya anaizungumzia ya Shilingi Trilioni 4.62 ambayo ilitokana na watumishi ambao walikuwa hawachangii katika mifuko lakini Serikali iliona na wenyewe wapate mafao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imetoa fedha Trilioni 2.17 ambayo imewezesha mifuko kupata nguvu na watu wote ambao malimbikizo yao yaliyokuwepo ya mifuko kwa wastaafu wamelipwa na sasa hivi watumishi wanaostaafu wanapata mafao yao ndani ya siku 60 tangu walipoleta taarifa zao za kustaafu yaani tangu tarehe ya kustaafu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna changamoto inawezekana kuna wachache ambao taarifa kama ambavyo kuna Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia mwingine anakuwa hana barua ya ajira kama nilivyosema, wale ambao walikuwepo kabla ya mwaka 1999 kweli kumekuwa na changamoto ya upatikanaji wa taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshafuatilia kundi hili waliobaki ni wachache na tunaendelea kuweka utaratibu wa kuhakikisha kwamba hata hao ambao waliingia kwenye mfuko wakati tayari wako kwenye utumishi na taarifa zao hazikuwa zimekuja rasmi, kwa kiasi kikubwa tumeshakamilisha kwa hiyo usumbufu huo hautakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uhakiki wa wastaafu, hili suala la uhakiki wa wastaafu niseme kwamba wastaafu wetu ni watu ambao wameitumikia nchi yetu kwa uadilifu na Serikali inawathamini wafanyakazi wanapokuwa kazini, na hata wanapostaafu Serikali inaendelea kuwathamini. Tayari Serikali imeshatoa maelekezo zoezi hili la wastaafu lisilete usumbufu kwa wazee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo napenda kuchukua nafasi hii kuwaelekeza *PSSSF* pamoja na *NSSF* zoezi la kuhakiki wastaafu lifanyike katika namna ambayo haitawalazimu wazee wetu kusafiri muda mrefu kwenda kwenye Makao Makuu ya Mikoa.

Kwa hiyo, hilo ni suala la usimamizi, tayari Serikali imetoa maelekezo kuhakikisha kwamba uhakiki wa wastaafu unafanyika katika namna ambayo haileti usumbufu kwa wazee wetu, lazima wazee waheshimiwe na lazima wazee walindwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine ambalo Waheshimiwa wanalizungumzia ni uhimilivu wa mifuko. Naomba nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba mifuko hii bado ni himilivu bado itaendelea kulipa mafao kwa wastaafu na deni ambalo lilikuwepo la...

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa kutoka wapi?

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Hapa

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpe taarifa Mheshimiwa Waziri. Taarifa za Serikali ya Machi 2022 ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali

amesema mifuko ina hali mbaya, siyo himilivu na iko kinyume na taratibu wa ukwasi wa asilimia 40, mlipolipa ile *pre* 99 Trilioni Mbili walau imefika asilimia 30 lakini ....

**MWENYEKITI:** Taarifa ya Serikali au taarifa ya *CAG*

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni taarifa ya *CAG* na ndiyo Serikali yenyewe.

**MWENYEKITI:** Basi rekebisha vizuri.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakupa pia taarifa kwamba *PSSSF* kwa miaka hii ya karibuni mapato yake ya michango ni madogo kuliko mahitaji ya wazee wastaafu wanaotakiwa kulipwa, iko himilivu wapi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Prof. Ndalichako unapokea taarifa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Ofisi ya Waziri Mkuu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi siipokei hiyo taarifa kwa sababu taarifa ya *CAG* ni ya mpaka Juni, 2021.

*(Hapa Mhe. Ester A. Bulaya alizungumza bila kutumia kipaza sauti)*

**MWENYEKITI:** Nani amekuruhusu uzungumze Mheshimiwa Bulaya? Hili ni Bunge endelea Mheshimiwa Profesa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU KAZI AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimeeleza kwamba tayari Serikali imetoa fedha shilingi trilioni mbili na bilioni mia moja sabini kwa ajii ya kulipia fedha za mifuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali imetoa fedha hizo ni dhahiri kwamba hata hizi ambazo zimebaki kiasi cha shilingi bilioni 2.45 Serikali itazitoa tu Serikali yetu ni sikivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hili ni deni la muda mrefu ambalo tangu mwaka 1999 lakini Serikali imeshalipia trilioni 2.17 na zilizobaki ni suala la muda tu. Kwa hiyo, suala hili litalipwa na wastaafu wataendelea kupata mafao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Profesa Joyce Ndalichako, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu. Sasa namuita Mheshimiwa Innocent Bashungwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima na afya, pili ninakushukuru sana kwa namna ambavyo unaendesha vikao nakupongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Dada yangu Mheshimiwa Jenista Mhagama pamoja na mdogo wangu Mheshimiwa Deo Ndejembi, kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya kuongoza Wizara ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, tunawapongeza sana kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuliongoza Taifa letu, pia nitumie nafasi hii kuwashukuru tena Waheshimiwa Wabunge kwa kutuwezesha kupitisha bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, bajeti ambayo tunaenda kuitekeleza kwa nguvu na jitihada kubwa tukishirikiana na nyinyi. Bajeti ya Utumishi ni bajeti ambayo inasomana kwa karibu sana na bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kwa hiyo nashukuru kupata fursa hii ili niweze ku-*clarify* baadhi ya mambo ambayo Waheshimiwa Wabunge mmeyajadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala la ajira. Katika hili ninamshukuru sana Rais wetu Mama Samia Suluhu

Hassan kwa kutupa kibali cha kuajiri Walimu 9,800, kwenye upande wa afya kuajiri Wauguzi 7,612. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu kwa kutupa kibali hiki, tunaenda sasa kuajiri vijana wetu ambao wamekuwa wakisubiri ajira kwa muda mrefu. Kwa hiyo, watapata fursa lakini pia tunaenda kupunguza uhitaji wa mahitaji ya Walimu na Wauguzi katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili Waheshimiwa Wabunge ningependa niwaondoe wasiwasi, mfumo wa kuomba ajira wa *online* kwa siku ya mwanzo kwa sababu wanaoomba ni wengi, kumekuwa kuna changamoto ya mambo ya mtandao lakini timu yangu inafanyakazi kwa jitihada kubwa kuhakikisha wanoomba huduma ya kuomba kupitia mtandao inaenda vizuri, nami baada ya kutoka hapa naenda kwenye eneo ambalo wanafanyia kazi kujiridhisha marekebisho haya yafanyike ili wale wanaoomba hizi ajira waweze kuomba kwa urahisi sana kupitia mtandao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye upande wa ajira Waheshimiwa Wabunge utaratibu uliopo na *application* ya mtandaoni imezingatia uhitaji wa ajira kwenye maeneo. Kama ni upande wa Wauguzi, kama ni upande wa Walimu imeangalia mahitaji ya nchi nzima, kwa hiyo wanapoomba inapeleka pale ambapo pana uhitaji mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ningependa mtuamini kwamba utaratibu uliopo unaenda kukidhi maeneo ambayo yana mahitaji *critical,* lakini hoja ambayo tumeipata hapa ya kwamba ajira izingatie maeneo kwa maana ya Wilaya, Majimbo ni wazo lakini naomba mtupe nafasi upande wa Serikali tulichukue tukaliangalie, tuangalie namna ambavyo linaweza likatekelezeka au kama utaratibu uliopo unaweza ukaboreshwa ili kuweza kuzingatia hilo, hilo pia tutaliangalia Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa machinga ningependa nitumie nafasi hii kutoa maelezo kwa ufupi sana, nimpongeze Mheshimiwa Kaka yangu Mheshimiwa Gwajima amelielezea vizuri, Mheshimiwa Rais wetu maelekezo

aliyoyatoa kwa wamachinga ni kuwawekea mazingira rafiki ya kufanyia kazi na kuwapanga kwa utaratibu ambao hatutumii msuli, kwa utaratibu ambao hatuchukui mali zao na kuzihodhi, kwa utaratibu ambao unajenga ustawi wa machinga huyu kuweza kufanya kazi kujipatia riziki, ku-*support* familia zao na kwa pamoja kama machinga waweze kusaidia katika kujenga uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni kundi ambalo tunalitambua na kulithamini kama Serikali. Serikali ya Awamu ya Sita kama nilivyoeleza kwenye bajeti yangu, pamoja na Bilioni Tano ambazo Mheshimiwa Rais ametupatia kwenda kujenga miundombinu hii rafiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa Dodoma kama nilivyoeleza tunajenga *Machinga Open Complex,* Waheshimiwa Wabunge baadhi yenu mmetembelea eneo hili, kwa dhamira njema ya Mheshimiwa Rais wetu bilioni tano ambazo alizitoa tumekuja kujenga soko hili kama mfano lakini tunataka tuende kwenye Majiji, Manispaa na baadae hata kwenye Halmashauri za Mji ambazo zina Machinga wengi ili tuweze kujenga masoko ambayo ni rafiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ningependa kutumia nafasi hii kutoa maelekezo kwa Wakuu wa Mikoa, maelekezo haya yazingatiwe na nimeshaelekeza Wakuu wa Mikoa kwenye masuala ambayo yanahisia kama machinga, bodaboda, mama lishe, tufanye *consultations* kati ya Mikoa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili *operation* ambazo zitakuwa zinafanyika tuwe tunauelewa wa pamoja ili kuhakikisha usimamizi wake wa *operation* hizi uweze kuwa ni rafiki na kwa matarajio ambayo Serikali inataka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali dhamira yake ni kuhakikisha tunaweka mazingira mazuri ya vijana wetu machinga akina Mama na Vijana ambao wanategemea sekta hii na tutaendelea kufanya sekta hii izidi kuwa Rafiki, izidi kuwa na matumaini kwa watu ambao wanaitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tunaendelea kufanya kila aina ya jitihada kujenga nyumba za watumishi, kwenye bajeti mmeona kwa mara ya kwanza bajeti ambayo tumeitenga kwa ajili ya kujenga nyumba za Walimu hasa hasa Walimu ambao wanaishi maeneo ya mbali. Jambo hili tumelizingatia kwenye bajeti na niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, kila mwaka wa fedha tutakuwa tunatenga fedha kwa ajili ya kujenga nyumba za watumishi ili kupunguza uhitaji mkubwa wa nyumba za watumishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kengele ya kwanza muda bado ninao basi. Kuhusu upungufu wa watumishi nimeshasema Mheshimiwa Rais tunamshukuru ametupatia kibali kwa ajili ya kuajiri Walimu na Wauguzi

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la upandishaji madaraja, katika hoja ambazo zimetoka kwa Waheshimiwa Wabunge tutaleta majibu kwa kila hoja, kwa kila Mbunge aliyechangia ikiwemo takwimu, lakini tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu, kwa kipindi ambacho amekaa madarakani mwaka mmoja amepandisha madaraja kwenye Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa, pia kwenye *arrears* tumekuwa tukishirikiana vizuri na Ofisi ya Rais, Utumishi kukusanya *arrears* na kuwapelekea Hazina ili kuhakikisha malimbikizo ya mishahara kwa watumishi wetu yanalipwa. Kwa hiyo, jambo hili tutaendelea kushirikiana ili tuweze kuhakikisha wenye haki ya kupandishwa madaraja lakini pia wenye haki ya kulipwa malimbikizo wanapata haki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimeshakubaliana na Dada yangu Mheshimiwa Jenista Mhagama, baada ya kuhitimisha hotuba yake na nitumie nafasi hii kuwaomba sana Waheshimiwa Wabunge tumpitishie bajeti ili akaweze kutekeleza haya mengi mazuri ambayo yamesheheni katika bajeti yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekubaliana baada ya leo Wizara mbili zitakaa, Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Utumishi tujipange vizuri kwa mambo ambayo mmetuelekeza humu.

Tujipange vizuri katika kutekeleza bajeti zetu mbili kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge pamoja na kuchangia maeneo ambayo yamehusu Ofisi ya Rais, TAMISEMI niwahakikishie Mheshimiwa Dada Jenista ni *role model* wa Wabunge wengi sana humu na tunajivunia yuko hapo. Kwa hiyo, kwenye mambo ambayo mmezungumza hapa nasi kwa vile mlituunga mkono, mkapitisha bajeti yetu kwa kishindo, muamini Wizara hizi mbili kwa kweli tuna ushirikiano wa karibu, changamoto ambazo mmezitaja tutashirikiana katika kuhakikisha zinatekelezwa kwa manufaa ya wananchi wetu wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie na suala la posho za Watendaji wa Kata. Nitumie nafasi hii kuwaelekeza Wakurugenzi wote nchini

**MWENYEKITI:** Hilo nakuongezea dakika moja liongee vizuri hilo la Watendaji wa Kata.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Serikali ilitoa posho ya madaraka kwa Watendaji wa Kata 100,000 kwa mwezi na tukaelekeza Wakurugenzi kuhakikisha kila mwezi Mtendaji wa Kata anapata hii 100,000 iweze kumsaidia katika majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Halmashauri, Watendaji wa Kata wamekuwa wakifuatilia kana kwamba hii ni hisani. Kwa hiyo nitumie nafasi hii kuwaelekeza Wakurugenzi kote nchini kuhakikisha kila mwisho wa mwezi Mtendaji wa Kata anapata hii 100,000 akiwa kwenye Kata yake, kuondokana na adha ya kutoka kwenye Kata kwenda kwenye Halmashauri kudai hii posho kana kwamba ni hisani. Hii siyo hisani ni haki ya Watendaji wetu kwa hiyo, Wakurugenzi zingatieni hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hili kwenye bajeti ijayo tunatambua kazi nzuri ambayo Watendaji wa Kata wanafanya, tutatenga bajeti kwa ajili ya kuwapa usafiri, katika hili nitumie nafasi hii kumshukuru sana Rais wetu Mama

Samia Suluhu Hassan tunaona hata Wizara za kisekta Mheshimiwa Rais ametoa vibali kwa ajili ya kuhakikisha Maafisa Kilimo kwa upande wa kilimo wanapata usafiri, Maafisa Ugani na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwenye bajeti itakayokuja ya 2023/2024 tutahakikisha Watendaji wa Kata na wenyewe tunawapa kipaumbele katika kuhakikisha wanapata usafiri ili waendelee kufanya kazi nzuri ambayo wanaifanya ya kuisimamia Serikali ngazi za Kata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge shughuli zilizopangwa kutekelezwa katika Saa Tatu mpaka Saa Saba zimekamilika, hivyo naahirisha shughuli za Bunge mpaka Saa Kumi Alasiri.

*(Saa 7.05 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge Lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Tukae.

Wachangiaji wote wamekwisha, sasa tunaingia upande wa Serikali, Mheshimiwa Naibu Waziri dakika tano au tatu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupatia afya njema na amani na furaha katika kipindi chote hiki cha mijadala ya Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Vilevile nitumie nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuniamini na kuniacha katika Ofisi yake yeye kumsaidia. Pia nitumie fursa hii kumshukuru Waziri wangu ambaye amekuwa mlezi, mwalimu na kwa muda mfupi Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama

ambaye nimefanya naye kazi kwa kweli nimejifunza mengi sana, namshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii vile vile kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Chamwino hapa Mkoani Dodoma kwa kuendelea kuwa na imani na mimi kama Mbunge wao na niendelee kuwaahidi kwamba sito waangusha na nitaendelea kuwatumikia vema siku zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika shukrani mwisho lakini si kwa umuhimu, kwamba *in a particular order* pia nimshukuru mke wangu kipenzi Subira na wanangu kwa kuendelea kuwa wavumilivu katika kipindi hiki ambacho naendelea na shughuli mbalimbali za siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile niwashukuru wajumbe wa Kamati ya USEMI wakiongozwa na Mwenyekiti wetu, Mheshimiwa Abdallah Chaurembo; Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Denis Londo; na wajumbe wote wa Kamati ya USEMI kwa kuendelea kutupa miongozo mbalimbali, ushauri mbalimbali na kufanya nao kazi vizuri siku hadi siku. Mwisho kabisa niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano wao na kutushauri inapobidi na vile vile kwa michango yao ambayo walikuwa wanaitoa katika kipindi hiki cha bajeti yetu ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nikienda kwenye hoja ambazo zimezungumzwa sana humu na Waheshimiwa Wabunge, nitajikita katika kuzungumzia hoja kubwa ambayo imegusa kila Jimbo la Mbunge humu ndani na katika nchi yetu, ni suala zima la *TASAF.* Katika kuzungumzia *TASAF* nitaanza kwanza kuelezea ili tupate uelewa wa pamoja wa namna ambavyo walengwa hawa wanapatikana, kwa sababu kwenye michango ya Wabunge nimeona sintofahamu ya walengwa hawa wanavyopatikana. Mfumo ulivyowekwa wa kuwapata walengwa wa kaya hizi ni kwamba wanatambuana wenyewe katika mikutano yao ya Serikali ya Kijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wanapoitana wanaanza utambuzi wa kujua nani anastahili kuwa katika mpango huu wa *TASAF* na nani ana uwezo wa kutosha wa kutoingia katika mpango huu wa *TASAF*. Baada ya utambuzi ule, ndipo waratibu wale katika ngazi zile wanachukua majina yale na kuweza kuyaingiza kwenye mfumo na majina yale kisha kwenda Makao Makuu na sasa kuwa *authorized* na malipo kuanza kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nipende tu kulitaarifu Bunge lako kwamba mpango huu wa *TASAF* unaanzia chini kwenda juu na si juu kwenda chini. Kaya hizi tunazozizungumzia ni 1,277,000, nchi nzima, ni kaya ambazo kabla ya mpango huu wa *TASAF* kuanza zilikuwa hazina uhakika wa milo mitatu kwa siku. Mpango huu umekuja ili kuweza kuwapa *safety net* ya maisha yao kuweza kuwanyanyua na kuwapa uhakika wa kula yao na uhakika wa kesho yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio maana huwa tunasisitiza na kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wawe mabalozi wa mpango huu wa *TASAF* na kila wanapokwenda Jimboni waweze kuzungumzia mpango huu. Pia kuhimiza wale walengwa yaani kaya zile kuhakikisha kwamba wanazitumia fedha hizi kufuga, fedha hizi kulima ili pale wanapopata uwezo wa kuwa na mifugo mingi, ndipo sasa wataweza kununua bima ya afya na kuweza kukidhi mahitaji mbalimbali ya siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango huu umekuwa na mafanikio makubwa sana. Kwa dakika tano sitoweza kuzitaja au sitoweza kutaja mafanikio yote ya mpango huu wa *TASAF,* lakini mpango huu umekuwa na mafanikio makubwa ambapo ukitembelea maeneo mbalimbali nchini, ukawasikiliza walengwa na kuona vile walivyokuwa wakiishi kabla ya kuingia kwenye mpango na baada ya kuingia kwenye mpango, utaona jambo lililofanywa na Serikali ni jambo kubwa sana. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa mchango wako mzuri. Sasa namwita mtoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru sana. Pia kwa moyo wa dhati kabisa, nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, ndugu yangu Mheshimiwa Ndejembi. Kwa kweli namshukuru sana Mheshimiwa Rais ambaye amekuwa na imani na huyu kijana mchapakazi, mahiri kabisa na naomba tu niseme, kwa kweli nimeridhika sana kufanya kazi na huyu kijana, ni msaada mkubwa kwangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru pia watendaji wote kama nilivyosema mwanzo ndani ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa kazi kubwa ambayo tumekuwa tukiifanya kwa ushirikiano, taasisi zote na Watendaji Wakuu wa Taasisi zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa leo wala hatutaki kupiga maneno wala porojo, tunachotakiwa sasa ni kutoa maelezo ya Serikali na hasa kuhusiana na hoja ambazo zilijikita katika mjadala kwenye siku hii ya leo. Nianze kwanza kwa kuwashukuru na kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote, katika kuchangia kwako wamedhihirisha kabisa wapo hapa kwa niaba ya ustawi wa wananchi. Ustawi wa wananchi ni pamoja na huduma bora kwa wananchi zinazotolewa na watumishi wa umma nchini, lakini hatuwezi kupata huduma bora zinazotolewa na sekta hii ya watumishi wa umma nchini kama vile pia hatutakuwa na watumishi wa umma wa kutosheleza mahitaji yanayohitajika katika sekta mbalimbali nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, sisi kwa mwaka huu wa fedha tumejipanga kuyashughulikia yote, tunaongozwa na dira ya maendeleo, mpango wa maendeleo, Ilani ya Uchaguzi lakini

vile vile maono ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, yeye katika utumishi wa umma amesimama katika kuhakikisha haki na stahiki za watumishi wa umma zinalipwa kwa kuzingatia taratibu na sheria. Sasa jambo hilo hata sisi watendaji lazima tulifuate. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Mheshimiwa Rais ametuhimiza tusimamie utumishi wa umma ili kuhakikisha pamoja na Serikali kutekeleza wajibu wake wa kuzingatia haki na stahiki za watumishi wa umma ni lazima tujipange kuwa na mifumo itakayowasaidia watumishi wa umma hawa pia na wao wawajibike kwa Serikali yao, lakini wawajibike kwa hiyari bila kulazimishwa na waweze kuwahudumia Watanzania wote vizuri kwa viwango vinavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tumekubaliana sasa ni *win win situation* watumishi wa umma waje hapa, Serikali ije hapa, tuzungumze, lakini mwisho wa siku ni ustawi wa Taifa hili kwa ujumla wake. Kwa hiyo naomba niwahakikishie watumishi wa umma nchini, tutapata muda wa kujibu hoja chache kwenye siku hii ya leo, lakini Waheshimiwa Wabunge tumechukua hoja zote tutazijibu kwa maandishi na naomba niwahakikishie wale Wabunge wanaowawakilisha wafanyakazi, lakini Wabunge wote mnaoiwakilisha sekta hii ya utumishi wa umma tutapata pia fursa ya kukutana na vyama vya wafanyakazi, tutaeleza haya yote yaliyoibuka kwenye mkutano huu na kuyatolea majibu kwa kina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nipite kwenye maeneo machache sana kwa kuzingatia muda ulionipa. Naona katika mjadala wa leo kulikuwa na mambo kadhaa ambayo ukiyachukua kiujumla ndio kilikuwa ni kilio kikubwa cha Waheshimiwa Wabunge kwenye mjadala wetu kwenye Wizara yetu, jambo la kwanza lilikuwa ni suala hili la kupanda vyeo na madaraja kwa watumishi wa umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme, pamoja na ushauri na nini tulioupokea lakini tuna kila sababu ya kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Samia Suluhu Hassan, tunakumbuka Serikali ya

Awamu ya Tano ilifanya kazi yake ya *clean data* za watumishi hewa, watumishi waliodanganya na vitu vya namna hiyo kwa muda mrefu madaraja hayakupanda lakini Mheshimiwa Rais alipoingia tu madarakani na kwa bajeti hii iliyopita, akaamua kufanya maamuzi ya kuhakikisha fedha zinatolewa na tukawa tumekwisha kupandisha madaraja na vyeo watumishi 190,781 na juzi nimesema kabla ya tarehe 30 Juni watumishi wengine 92,000 lazima wapande madaraja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nimewasikiliza sana Wabunge na hasa nimewasikiliza pia wale ambao wanawawakilisha wafanyakazi, lakini na wote waliokuwa wanawawakilisha watumishi wa umma wakasema hoja yetu hapa tunalo lile kundi lililoachwa nyuma mwaka 2015, 2016 na 2017. Hawa watumishi tunafanya nao nini, kwa sababu na wao katika kipindi kile ambacho tumeamua Serikali sasa tusafishe *data* za watumishi wa umma tulikuwa na watumishi takribani 67,244 ambao kuna wengine walikuwa wameshapata barua mkononi za kupanda vyeo, zile barua zikafutwa na upandaji wao wa vyeo ukasimamishwa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hao ndio watumishi ambao wengine wanakaribia kustaafu lakini haki yao ya kupanda vyeo haijatekelezwa kama ilivyotakiwa kwa mujibu wa kada zao na kwa mujibu wa bajeti zilizopangwa. Hapa kwenye jambo hili hatuna mjadala wa kumpongeza Mheshimiwa Rais, lakini hoja inabaki kwa hao watumishi ambao walikuwa *stranded* baada ya hayo mambo kuwa yametokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge mwaka 2020/2021, tulifanikiwa kuwapandisha watumishi 16,025 tu kati ya hao 67,244. Kwa hiyo tuna watumishi 51,219 ambao hawajui hatma yao, watumishi hawa pia kuna wenzao waliopanda madaraja kwa utaratibu wa kawaida sasa wametofautiana nao madaraja, wenzao wameshaondoka wao wamebaki wana-*hang* hawajui hatma yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme hivi, tumekubaliana ndani ya Serikali na tunamshukuru sana Kiongozi Mkuu wa Nchi, Mheshimiwa Rais wetu tulichoamua sasa ni lazima tuondoe hayo manung'uniko watumishi hawa tunasema wafanye kazi kwa hiyari, lakini watafanyaje kazi kwa hiyari kama hawajatekelezewa hiyo stahili yao. Mtu anayetaka kula ni lazima afanye nini?

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Ni lazima aliwe.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Hapana, ni lazima anawe mikono, Mheshimiwa Paresso ni lazima anawe mikono. Kunawa mikono kunathibitisha utayari wake wa kula.

Mheshimiwa Naib Spika, utayari wa kula inaonesha kwamba kuna umakini na sisi Serikali tumesema tutakuwa makini kwenye jambo hili. Naomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge, tulichokipanga sasa tutafanya nini? Tumeamua kwenye hawa watumishi 92,000 wale ambao wanakaribia kustaafu katika kipindi hiki kifupi ni lazima tutawa-*consider* kwenye hawa watumishi 92,000 tuweze kuwasawazisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hiyo namba ambayo nimeisema wa watumishi 51,219, tutakwenda kuwatambua wale wanaokaribia kustaafu kabla ya tarehe 30 Juni tuanze na hao kusudi wasije kuumia kwenye mafao yao huko baadaye. Hata hivyo, kwa mwaka ujao wa fedha mmenisikia hapa Mheshimiwa Rais ameidhinisha mafungu ya fedha kwa ajili ya kazi hiyo, naomba niwahakikishie tunajipanga kuwapandisha kwa mseleleko ili tuondoe adha na kadhia hii kubwa ambayo watumishi hawa wameipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba niwaambie hatutaki matabaka ndani ya Serikali tumeamua sasa hatutaki matabaka tunataka kila mtumishi anapofikia wakati wa kupandishwa daraja, basi iwe inafanyika hivyo, kwa hiyo tunataka tuondoe hizi kadhia ya nyuma hizi

Waheshimiwa Wabunge na naomba mumpigie sana Makofi Mheshimiwa Rais na Serikali yake jambo hili tumeamua kulichukua kwa uzito mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wameeleza sana hapa ndani upungufu wa watumishi, ndugu zangu tunakubali tuna upungufu wa watumishi, lakini hatuishi katika kisiwa, upungufu huu wa watumishi umeendelea katika mataifa mengine mbalimbali, lakini sio sababu kwa Serikali yetu, kutokuhakikisha kwamba tunajitahidi kuondokana na tatizo hilo la watumishi. Waheshimiwa Wabunge naomba kwa dhati ya moyo wangu, kwa kweli tumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu. Hapa wote tumekuwa mashahidi na mmeona tulipanga bajeti ya watumishi 44,096 na tulipofika mwaka 2020/2021, tukawa tumeajiri wachache na ndio maana tumetangaza hizo ajira 32,000 *plus* ili tuhakikishe kwamba tunakamilisha ahadi ya Serikali ya Watumishi 44,096, tukaanze kupunguza huo upungufu katika maeneo yetu mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimewaambia hapa kipaumbele imebidi twende na hicho ambacho Wabunge wanaowawakilisha wananchi wao, tumejenga madarasa ya UVIKO, tumejenga vituo vya Afya na Zahanati, twende tukaanze kuhakikisha vituo hivyo vyote vinatoa huduma na visikae bila kutoa huduma. Tutakwenda pia kwenye sekta nyingine, kwa mfano sekta ya kilimo, mmeona tumezindua mkakati wa kilimo na Waheshimiwa Wabunge wamesema Bunge hili ni la mkakati wa kilimo, huko pia tutakwenda kuzingatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwahakikishie kwamba, tumejipanga, lakini tunafanyaje, suala la ajira sasa litaendana na kufanya *HRO audit* ama *main power audit*, *main power survey,* tujue humu ndani ya nchi tumejipangaje hawa watumishi ndani ya Taifa letu. Niwape mfano mmoja tulifanya tu utafiti kidogo wakati tunafanya hii *main power audit* kwenye eneo la majiji makuu na hasa sekta ya uhasibu, tukawauliza haya majini hivi mahitaji yetu ya Wahasibu mnaowahitaji ni wangapi? Wakatuambia wanataka

Wahasibu 526. Tukawauliza mnao wangapi wakatuambia waliopo katika kipindi hicho walikuwa 351. Sasa sisi tukaenda kuwasiliana na Wizara ya Fedha, tukawauliza hivi kwa utaratibu wa haya majiji wanahitaji Wahasibu wangapi wakatuambia wanahitaji wahasibu 317 tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tukagundua kwamba tungewapa hawa 500 na kitu wangekuwa na *extra* 209 katika maeneo yao ya kazi. Wakishakuwa na *extra* 209 ndio tutabaki tunalaumu kwamba Wahasibu hawatoshi kumbe kuna kada fulani watumishi wapo wengi hawazingatii ikama iliyokuwa inatakiwa, kama walitakiwa wawili hapa tungeweza kujikuta kwamba wapo watano ama sita, kwa hiyo basi mtawanyiko na msambazo wa watumishi hauendani na mahitaji katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, wametuambia, huko vijijini walimu wachache, lakini nendeni kwenye shule za mjini, walimu wapo wengi. Hata kwenye kada nyingine tofauti tofauti, naomba mtuunge mkono tunafanya hii *HR Audit* vizuri, *survey* inafanyika vizuri, mwisho wa siku tunataka sasa kuwa na majibu halisi ya kuona nini kifanyike kusudi hiki kidogo tulichonacho kiweze kumhudumia kila Mtanzania katika eneo alilopo na kwa ufanisi wa hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, labda eneo lingine ni *recategorization* limesemwa sana hapa. *Recategorization* tunaitazama katika sura tatu zifuatazo: ya kwanza, mtu anaweza kufanyiwa *recategorization* kama mwajiri anaona katika sekta yake kuna uhitaji wa mtumishi; labda kwenye Halmashauri wanahitaji Afisa Manunuzi na hayupo, lakini kuna Mwalimu anayeweza kwenda kusomea Uafisa Manunuzi na akaja kusaidia. Mwajiri atamwandikia kumwomba, naye akikukubali na akaenda shule, akirudi, mshahara wake itabidi aendelee nao kwa sababu mwajiri alikuwa na hilo tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba waajiri wote kama watumishi hao wameangukia kwenye kifungu hiki cha

kwanza, ni lazima wafanyiwe *recategorization* na wawekwe kwenye ikama na ni lazima haki itendeke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili, ni mtumishi kuomba kujiendeleza kwa kuruhusiwa kwa maandishi na mwajiri wake, naye mwenyewe kuomba kwa maandishi, lakini kwenye kada ile ile ya kwake. Kama ni Mwalimu ana *Degree,* anaenda kufanya *Masters,* kama ana *Diploma* anaenda kufanya *Degree,* kama ana *Masters,* anaenda kufanya *Ph.D* katika kada yake ile ile, huyo naye akirudi ni lazima afanyiwe *recategorization* na mshahara wake uendane na madaraja yatakoendana na kisomo chake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo watumishi waendeshaji kama ma-*PS*, madereva na watu wa namna hiyo; hawa sasa wakienda kusoma na kurudi, wana kibali cha kufanyiwa *recategorization* ili mradi tu walipata kibali cha kwenda kufanya hivyo. Sasa shida inakuja, kwa watumishi ambao wamesoma fani tofauti, wanaenda kusomea kada na fani nyingine tofauti halafu wanatakiwa wafanyiwe *recategorization,* sasa hapo ndipo pana shida ndugu zangu...

**NAIBU SPIKA:** Dakika moja, malizia.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunawaomba waajiri wote hawahakikishe kwamba wanaposhughulikia masuala ya *recategorization,* wazingatie miongozo na taratibu tulizozitoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna suala la watumishi wa Darasa la Saba, kama utanipa muda wa dakika mbili tu nadhani hili lilikuwa limezungumzwa sana.

**NAIBU SPIKA:** Dakika moja na nusu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Haya, dakika moja

na nusu naipokea kwa unyenyekevu mkubwa. Hadi sasa Watumishi wa Darasa la Saba walioondolewa kimakosa 4,380 wamesharejeshwa kwenye utumishi. Kwa nini wamerejeshwa? Hawa ni wale ambao waliajiriwa kabla ya tarehe 20 Mei, 2004. Kwa hiyo, sifa yao ya ajira ilikuwa ni darasa la saba.

Kwa hiyo, kama waliondolewa kimakosa na pia kama hawakughushi, kwa sababu wengine waligushi vyeti hapo katikati na wakajiona kwamba ni *form four.* Sasa kama walighushi, hao hatuwahitaji, lakini kama hawakughushi, wanatakiwa warudishwe. Huo ndiyo utaratibu na mpaka sasa hawa 4,380 wamesharudi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watumishi wengine ambao waliajiriwa baada ya tarehe 20 Mei, 2004, baadhi ya waajiri hawakuzingatia utaratibu, wakawaajiri tena darasa la saba badala ya kigezo cha *form four;* na hao nao waliondolewa. Sasa tulisema hivi, hao walioondolewa wanatakiwa kurudi kazini, lakini kama wametekeleza kile kigezo cha kujiendeleza. Kwa hiyo, tuliwaagiza wajiendeleze na watumishi 954 wamejiendeleza na wamesharudi kazini na wapo kazini mpaka sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaomba wale ambao wanataka kurudi na wamejiendeleza, waendelee kuwasiliana na Ofisi zetu. Kama hawakujiendeleza, kwa sababu hicho ndiyo kilikuwa kigezo, waajiri tunawaagiza waendelee kufuata maelekezo na nyaraka tulizowapelekea wazisome ili waweze kutenda haki kwa hao watumishi. Hata hivyo, hawa nao tutawarudisha kazini na watapata haki zao kama nao hawakughushi vyeti. Kuna wengine walighushi vyeti pamoja na kwamba waliajiriwa kwa sifa hiyo, lakini wakaghushi vyeti. Sasa kama walikuwa wameghushi vyeti, hilo nalo hatutaweza kulizingatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, maelezo zaidi tutaendelea kuyatoa na ninaomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ya muda, itatupasa

tufanye *Press* maalum ya kuyaeleza haya mambo yote kwa ukubwa na upana wake kadri inavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika,...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri toa hoja.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa huu muda, tulikuwa na mambo mengi ya kueleza, lakini kwa sababu ya muda, basi niishie hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono. Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Tukae. Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA PILI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 32 – Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora**

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resources Management......*Sh. 14,094,942,500

**MWENYEKITI:** Nina jina moja tu hapa la mshahara wa Waziri Mheshimiwa Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Niwe mkweli, leo dada yangu umejibu vizuri. Mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni. Sikusudii kushika shilingi, nahitaji *commitment* yako kwenye suala la madeni ya watumishi. Najua wanadai shilingi bilioni 430, mmelipa shilingi bilioni 91, najua mmetenga shilingi bilioni 103 na haya madeni ni ya muda mrefu. Nahitaji *commitment* ya Serikali kuhakikisha lile deni la kwanza linalipwa na hiki kinachotengwa kwa ajili ya madeni ya watumishi kipewe kipaumbele, yalipwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo jambo jema watumishi wakawa na madeni kwa Serikali ambapo ni haki yao; malimbikizo ya mishahara, malimbikizo ya posho mbalimbali. Kwa hiyo, nahitaji *commitment* ya Serikali, na ningefurahi sana kama Waziri wa Fedha angekuwepo, maana tunaweza kukubana wewe, yeye haleti pesa kwenye Wizara yako kwa ajili ya kuwalipa hawa watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nahitaji *commitment,* hiki tulichokitenga kitoke ndiyo kipewe kipaumbele. Ni hilo tu dada yangu. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kama Mheshimiwa Ester anasema leo tumejibu vizuri, hiyo kwanza ni *commitment* ya kutosha kuonesha kwamba tuko *serious* na mambo ambayo tunakwenda kuyafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme hivi, yale madeni ya mishahara ambayo yanakwenda moja kwa moja kwenye Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma nadhani Waheshimiwa Wabunge mmesoma taarifa zangu zangu zote, mmeisoma *speech* yangu, tumeshatenga mpaka

na kwenye bajeti. Kwa hiyo, hayo yote tunakwenda kuyalipa na wala hakuna mjadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Mheshimiwa Bulaya amezungumza madeni mengine ya posho na mambo mengine, sasa hayo madeni mengine ya posho; likizo na vitu vingine, ni madeni ambayo yameenda kwenye sekta zinazohusika. Tutawasiliana na sekta husika, wale ambao hawajasoma bajeti watakapokuja, basi tutaendelea kushauriana ndani ya Serikali kuhakikisha kwamba watumishi wanapata hizo haki na wanalipwa hizo stahiki zao.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts Unit*.........Sh. 478,351,700
Kifungu 1003 - *Government Communication Unit*......................................Sh. 239,162,700
Kifungu 1004 - *Procurement Management Unit*..Sh. 279,515,000
Kifungu 1005 - *Internal Audit Unit*.......................Sh. 245,915,500
Kifungu 1006 - *Planning Division*..........................Sh. 525,152,000
Kifungu 1007 - *Legal Service Unit*.......................Sh. 233,911,500
Kifungu 2001 - *Policy DevelopmentDivision*......Sh. 869,645,000
Kifungu 2002 - *Management Service Division*....Sh. 845,021,400
Kifungu 2003 - *Establishment Division*..............Sh. 1,177,790,900
Kifungu 2004 - *Ethic Promotion Division*.............Sh. 547,618,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Kuhusu Utaratibu, Kanuni?

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kuhusu utaratibu, kanuni ya 76 lakini nikirejea kanuni iliyovunjwa au ambayo haijakidhiwa matakwa ya Kanuni ya 134 ; Akidi na Utaratibu katika Kamati za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiniruhusu nisome Kanuni ya 134 (1) inasema; "Masharti ya Kanuni ya 90 yatatumika kuhusu Kamati za Bunge Zima, ila tu kama idadi ya Wabunge waliohudhuria itakuwa bado haifikii nusu ya Wabunge wote..."

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusoma hapa, tunapitisha vifungu lakini hata nusu ya Wabunge hatujafika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tuna *quorum* toka asubuhi na tunaendelea nayo. *(Makofi/Kicheko)*

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

Kifungu 2005 - *Human Capital Management Division*................................Sh. 1,426,074,000
Kifungu 2006 - *Performance Contracting*.........Sh. 537,464,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Kuhusu Utaratibu.

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisome Kanuni ya 90(1) ambayo unaivunja. Kanuni ya 90 (1) inasema;... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa umeanza tu, Mwenyekiti umevunja....

Kaa chini, kiti hakivunji kanuni. Kuna utaratibu wa kupeleka malalamiko ya Kiti, siyo hapa. Kaa chini.

Tuendelee Katibu. *(Kicheko)*

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

Kifungu 3001 - *Human Resource Development Division*................................Sh. 6,602,141,126

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima, kaa chini tafadhali.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Lakini unavunja utaratibu!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, kaa chini.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 3004 - *Division of Salary and Remuneration*.................Sh. 555,826,100

Kifungu 4002 - *Management Information System Division*...................Sh.10,882,849,574

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 20 – Ofisi ya Rais - Ikulu**

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resources Management*......Sh. 29,828,203,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 30 – Ofisi ya Rais, Sekretariati ya Baraza la Mawaziri**

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resources Management*.....Sh. 568,725,075,000
Kifungu 1002 - *Finance and Accounts Unit*.......Sh. 805,784,000

Kifungu 1003 - *Government Communication Unit*......................................Sh. 968,588,000
Kifungu 1004 - *Procurement Mgt. Unit*...............Sh. 568,455,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MHE. SALUM MOHAMMED SHAAFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Utaratibu, kanuni ipi?

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. SALUM MOHAMMED SHAAFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kanuni hii, kifungu cha 90 naomba uniruhusu nikisome; Akidi kwa kila kikao...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, *ruling* ya Mwenyekiti, ilishatolewa, kaa chini. Mheshimiwa kaa chini.

**MHE. SALUM MOHAMMED SHAAFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Endelea Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

Kifungu 1005 - *Information and Communication Technolgy Unit*........................Sh. 313,118,000
Kifungu 1006 - *Procurement Management Unit*..Sh. 616,850,000
Kifungu 2001 - *Cabinet Secretariat*....................Sh. 2,997,266,000
Kifungu 2002 - *Government Communication*.....Sh. 370,970,000

Kifungu 2003 - *Good Governance*......................Sh. 981,860,000
Kifungu 2004 - *Public Service Appeal*................Sh. 858,707,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 33 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma**

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resources Management*......Sh. 2,464,478,000
Kifungu 1002 - *Finance and Accounts Unit*........Sh. 432,669,000
Kifungu 1003 - *Planning Monitoring and Evaluation Unit*.......................Sh. 528,393,000
Kifungu 1004 - *Government Communication Unit*................................................Sh. 203,595,000
Kifungu 1005 - *Procurement and Management Unit*........................................Sh. 226,671,000
Kifungu 1006 - *Internal Audit Unit*........................Sh. 219,137,000
Kifungu 1007 - *Information and Communication Technology Unit*.......................Sh. 325,751,000
Kifungu 1008 - *Legal Services Unit*........................Sh. 250,269,000
Kifungu 2001 - *Public Leaders Ethics Enforcement Division*...................................Sh. 513,751,250
Kifungu 2002 - *Public Leaders Ethics Prom. Div.* ...Sh. 511,572,000
Kifungu 2004 - *Zonal Office Northern Zone*........Sh. 343,873,000
Kifungu 2005 - *Zonal Office Sothern Zone*..........Sh. 329,293,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MHE. SALUM MOHAMMED SHAAFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Utaratibu.

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. SALUM MOHAMMED SHAAFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu Kanuni ya 134, naomba uniruhusu niisome.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 134 (1): "masharti ya kanuni ya 90 yatatumika kuhusu Kamati ya Bunge Zima...

Naendelea Mwenyekiti, ila tu kama idadi ya Wabunge waliohudhuria itakuwa bado haifikii nusu ya Wabunge wote. Baada ya kipindi kilichowekwa na kanuni ya 90(3) Mwenyekiti ataondoka kwenye kiti, Bunge litarudia na Katibu atahesabu idadi ya Wabunge waliohudhuria na kama idadi yao itakuwa bado haifikii nusu ya Wabunge wote, basi Spika ataahirisha Bunge."

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Kaa chini. Inaelekea kuanzia asubuhi wewe ulikuwa hujaingia humu ndani. Kaa chini. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Hii ni Kamati ya Matumizi. Mheshimiwa *Chief Whip.*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisimama kumpa taarifa mzungumzaji kwamba suala la kuhusiana na utaratibu wa hoja aliyokuwa anaizungumza, kiti kilitoa uamuzi, na ninaomba nisimamie, ninaomba nisimamie Kanuni ya 78 ambayo inasema, uamuzi wa Spika kuhusu suala lolote la utaratibu, mwongozo au taarifa itakuwa ndiyo mwisho. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Esther Matiko. Jamani michango yote ilikuwa ni kuhusu mishahara ya watumishi, sasa mishahara inapitishwa mnalalamika. Tuendelee Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

**Fungu 33 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma**

Kifungu 2006 - *Zonal Office – Central Zone*.........Sh. 449,444,250
Kifungu 2007 - *Zonal Office – Eastern Zone*........Sh. 454,574,250
Kifungu 2008 - *Zonal Office – Southern Highlands*................................Sh. 489,259,000
Kifungu 2009 - *Zonal Office – Lake Zone*.............Sh. 475,287,000
Kifungu 2010 - *Zonal Office – Western Zone*.........Sh. 344,108,000
Kifungu 2011 - *Zonal Office – Dar es Salaam*........Sh. 697,924,250

*(vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUngu 67 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma**

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resources Management*.......................Sh. 2,253,832,515
Kifungu 1002 - *Finance and Accounts Unit*........Sh. 233,588,000
Kifungu 1003 - *Planning, Monitoring and Evaluation Unit*.......................Sh. 150,384,000
Kifungu 1004 - *Government Communication Unit*.......................................Sh. 107,800,000
Kifungu 1005 - *Legal Services Unit*......................Sh. 138,280,000
Kifungu 1006 - *Procurement Management Unit*..Sh. 173,760,485
Kifungu 1007 - *Management Information Systems Unit*............................Sh. 342,311,000
Kifungu 1008 - *Internal Audit Unit*..........................Sh. 109,316,000
Kifungu 2001 - *Recruitment Management Division*..................................Sh. 932,611,000
Kifungu 2002 - *Quality Control*............................Sh. 621,966,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 94 – Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma**

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resources Management*.......Sh. 1,924,117,838
Kifungu 1002 - *Finance and Accounts Unit*........Sh. 299,167,816
Kifungu 1003 - *Planning, Monitoring and Evaluation Unit*.......................Sh. 344,330,000
Kifungu 1004 - *Internal Audit Unit*.......................Sh. 122,258,000
Kifungu 1005 - *Procurement Management Unit*..Sh. 114,088,000
Kifungu 1006 - *Legal Services Unit*.......................Sh. 199,738,000
Kifungu 1007 - *Government Communication Unit*.....................................Sh. 140,970,000
Kifungu 1008 - *Information and Communication Technology Unit*.......................Sh. 260,462,682
Kifungu 1009 - *Guid. Formulation, Dissertation and Research*........................Sh. 277,866,000
Kifungu 2006 - *Appeals and Complains Department*......................Sh. 1,152,394,664
Kifungu 2007 - *HR Standards and Compliance Department*.........................Sh. 846,431,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 04 – Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa**

Kifungu 1001 - *Administrative and Human Resources Management*......Sh. 1,432,007,986
Kifungu 1002 - *Finance and Accounts Unit*.........Sh. 139,076,000
Kifungu 1003 - *Planning, Monitoring and Evaluation Unit*......................Sh. 104,577,000
Kifungu 1004 - *Information And Communication Technology Unit*.....................Sh. 221,969,852
Kifungu 1005 - *Legal Services Unit*.............................Sh. 400,000
Kifungu 1006 - *Internal Audit Unit*.........................Sh. 98,570,000
Kifungu 1007 - *Government Communication Unit*....Sh. 300,000
Kifungu 1008 - *Procurement Management Unit*..Sh. 123,393,148
Kifungu 4001 - *Archive Management Division*.....Sh. 290,378,014
Kifungu 4002 - *Records Management Division*....Sh. 648,054,000

Kifungu 4003 - *Records Center Division*..............Sh. 265,119,000
Kifungu 4004 - *The Founders of the Nation Centre Division*........................Sh. 180,946,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**KITABU CHA NNE**

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 32 – Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora**

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resources Management*.......Sh. 4,500,000,000
Kifungu 2002 - *Management Services Division*....Sh. 150,000,000
Kifungu 2004 - *Ethic Promotion Division*..............Sh. 150,000,000
Kifungu 2005 - *Human Capital Management Division*......Sh. 0
Kifungu 2006 - *Performance Contracting*..........Sh. 160,000,000
Kifungu 3001 - *Human Resources Dev. Division*....Sh. 100,000,000
Kifungu 4002 - *Management Information System Division*.....................Sh. 3,010,200,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 30 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri**

Kifungu 1003 - *Policy and Planning Unit*.......Sh. 164,092,535,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 33 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma**

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resources Management*........Sh. 2,800,000,000
Kifungu 1003 - *Planning, Monitoring and Evaluation Unit*........................................Sh. 115,000,000

Kifungu 1004 - *Government Communication Unit*.............Sh. 0
Kifungu 1007 - *Inf. and Comm. Technology Unit*...Sh.164,300,000
Kifungu 1008 - *Legal Services Unit*........................Sh. 89,550,000
Kifungu 2001 - *Public Leaders Ethics Enforcement Division*.................................Sh. 155,600,000
Kifungu 2002 - *Public Leaders Ethics Promotion Division*.................................Sh. 145,550,000
Kifungu 2004 - *Zonal Office – Northern Zone*......................Sh. 0
Kifungu 2005 - *Zonal Office – Southern Zone*......................Sh. 0
Kifungu 2006 - *Zonal Office – Central Zone*........................Sh. 0
Kifungu 2007 - *Zonal Office – Eastern Zone*........................Sh. 0
Kifungu 2008 - *Zonal Office – Southern Highlands*.............Sh. 0
Kifungu 2009 - *Zonal Office – Lake Zone*.............................Sh. 0
Kifungu 2010 - *Zonal Office – Western Zone*.......................Sh. 0
Kifungu 2011 - *Zonal Office – Dar es Salaam*.......................Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 67 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma**

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resources Managemen*..........................Sh. 0
Kifungu 1007 - *Management Information Systems Unit*.........................Sh. 3,658,000,000

*(Vifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 94 – Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma**

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resources Management*.........................Sh. 0
Kifungu 1008 - *Information and Communication Technology Unit*......................Sh. 300,000,000

*(Vifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 04 – Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa**

Kifungu 4001 - *Archive Management Division..*Sh. 1,260,000,000
Kifungu 4002 - *Records Management Division...*Sh. 150,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

*(Bunge Lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Tukae. Toa mhoja.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 123 (3)(a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 ninaomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi zake. Naomba sasa Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mhesimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono. Sasa nitawahoji. Kwamba Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora wa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Wanaoafiki waseme ndiyo, wasiofiki waseme siyo.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*
*(Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 Yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri hongera sana, wewe na Naibu wako na timu yako ambayo mmekaa huku mmefanya kazi nzuri sana. Taifa linawategemea sana na kwa kweli *you deserve* makofi mengi kutokana na unyeti wa Wizara yako. *(Makofi)*

Waheshimiwa tuna wageni wa Bunge. Mgeni wa Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said ambaye ni mtoto wake, ndugu Juma Idd Ame Mzambia, karibu.

Wageni watatu wa Mheshimwa Noah Lemburis Saputu Mollel, Mbunge ambaye ni wapiga kura wake kutoka Rumeru Magharibi, Mkoa wa Arusha Mwinjilishi Baraka Mollel, Mwalimu Elizabeth Lengai na Mwalimu Philomena Lucas. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge kuna tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge. Katibu wa Bunge anawatangazia Wabunge wote kwamba Maadhimisho ya Sherehe ya Miaka 58 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar yatafanyika siku ya Jumanne tarehe 26 Aprili, 2022. Sherehe hizo Kitaifa mwaka huu zitafanyika katika ukumbi wa mkutano Jakaya Kikwete hapa Dodoma kuanzia saa moja asubuhi hadi saa saba mchana. Mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wabunge wote mnaalikwa kuhudhuria sherehe hizo muhimu kwa Taifa letu. Ratiba kamili na upatikanaji wa kadi za sherehe mtajulishwa mara taratibu zitakapokamilika. *(Makofi)*

Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania, Mheshimiwa Shally Josepha Raymond anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge wanawake kuwa kesho tarehe 23 kutakuwa na semina kwa ajili ya Wabunge

wanawake wote. Semina hiyo itafanyika katika ukumbi wa Msekwa kuanzia saa tatu na nusu asubuhi.

Waheshimiwa Wabunge niwashukuru kwa michango yenu na kwa kazi kubwa mliyofanya. Sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka siku ya Jumatatu saa tatu asubuhi.

*(Saa 10.55 Jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu, Tarehe 25 Aprili, 2022, Saa Tatu Asubuhi)*